UKOLONI MAMBOLEO NA UT ANDA WAZI KA TIKA T AMTHILIA TEULE

NA

ANDREW KAIRI MWIRABUA

NAMBARl: C50 *ICE* /13894 *12009*

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA IDARA Y A KISW AHILI NA LUGHA ZA

KIAFRlKA KATIKA CHUO CHA KENYATTA ILl KUTOSHELEZA BAADHI YA

MAHITAJI YA KUTUZWA SHAHADA YA UZAMILI KA TIKA KISW AHILI.

MEr 2014.

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

# IKIRARI

MTAHINIWA

Tasnifu hii ni kazi yangu asili na wala haijapata kutolewa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

JINA: ANDREW KAIRI MWIRABUA

C50/ CE/ 13894/ 2009

SAHIHI: ........................ TAREHE ........................

WASIMAMIZI

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta .

DKT. R.M. Wafula

Idara ya Kiswahili na lugha za Kiafrika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

SAHIHI ........................ TAREHE ........................

BW. P. M. MUGAMBI

Idara ya Kiswahili na lugha za Kiafrika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

SAHIHI ........................ TAREHE ........................

# I(UTABARUKU

Kazi hii nitamtabarukia mke wangu mpenzi na rafiki, Evangeline Gakii kwa wajibu alioutekeleza kwa kunichochea kuendeleza masomo yangu na kwa kushughulikia .mahitaji ya nyumbani nilipokuwa nimebanwa na masomo. Aidha kwa mchungaji wangu, Kasisi Martin Koome kwa himizo lake la kuendeleza masomo yangu. Pia namtabarukia mama yangu Ruth Ciolimbere kwa kunihimiza katika yote.

# SHUI<RANI

Ningependa kuwashukuru watu wote waliochangia ufanisi wa utafiti huu kwa nj ia moja au nyingine. Siwezi kudai kwamba jitihada zangu pekee zingewezesha kufua dafu bila mchango wa wengine wengi. Tasnifu hii isingekamilika bila ushauri na usaidizi wao. Si rahisi kuwataja wote bali nitawataja baadhi yao.

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha njema na kuniwezesha kutimiza ndoto yangu ya kupata shahada ya uzarnili, katika somo la Kiswahili. Daima aliniepusha na majaribu mengi ambayo yangenizonga akili na kujibu sala zangu kimuujiza wakati nilipoelekea kutamauka.

Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Daktari Wafula Richard na Bw. Mugambi Peter, kwa mawaidha mazuri, ushauri na uongozi mwema wakati wote nilipohitaji kuonyeshwa njia. Ushauri wao na mwongozo thabiti umeniwezesha kufanikisha kazi hii. Daima nitaishi kuwakumbuka kwa wema wao.

Shukrani maalumu ziwaendee wahadhiri walionifundisha na kunifungua macho katika ulimwengu wa wasomi kwa njia za kipekee. Wao ni ProfKitula King'ei, Dkt. Mwita Chacha, Dkt. Ngugi Pamela, Dkt. Masinde Edwin, Dkt. Wafula Richard pamoja na wahadhiri wengine wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. Walijitolea kuhakikisha kuwa nimepata shahada hii ya uzamili.

Pia shukrani ziwaendee wenzangu tuliosoma nao kwa ushirikiano wa karibu. Wao ni: Mucee Franklin, Ombaye Robert, Abieri Martha, Makau Joseph, Mwenda Japhet, Lomatoro Joel, Masiolo Hilda, Ndwiga Peter, Kiplangat Nehemia, Webukha Walter,

Mwangi Leah, Rachel Apondi, Muthoni Josephine, Shiholo Margaret, Khaemba Daniel, Millicent Onyango, Kyalo Justus na Muema Joyce. Mungu awabariki zaidi kwa ushirikiano wenu mwema ulionifanikisha katika kazi hii.

Shukrani zaidi ni kwa familia ya Mweteri Isaiah kwa kunichukua kama ndugu yao. Wamenifadhili kwa njia nyingi na Mungu awabariki sana. Shukrani nyingi ni kwa mke wangu Evangeline Gakii kwa kuvumilia sana na kuchukua jukumu la kuwalea watoto peke yake wakati nikisoma na pia kwa kunitia moyo wa kuendelea. Aidha nawashukuru watoto wangu Karwitha Janice, Mwende Joy, Mukiri Victory na Mwakairu Jane kwa uvumilivu mwingi wakati waliponihitaji.

Mwishowe shukrani ni kwa walimu ninaofundisha nao na marafiki wote walionipa moyo wa kuendelea na masomo: mwalimu Joy Kagendo, Kawira Hellen na Kariuki. Mungu awabariki zaidi. Nyote niliowataja na hata wale zikuweza kuwataja Mungu awabariki zaidi.

# IKISIRI

Utafiti huu umechunguza jinsi ukoloni mamboleo unavyodhihirika katika muktadha wa utandawazi kwa kurejelea tamthilia mbili teule: *Posa za Bikisiwa (2008)* ya S. A. Mohamed na K. King'ei na *Sudana (2006)* ya Alamin Mazrui na K. Njogu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Baada Ukoloni. Utafiti ulifanyiwa maktabani. Mtafiti alisoma makala mengi yaliyohusiana na mada ya utafiti ili kupata data iliyokusudiwa. Mtafiti pia alifanya utafiti wa nyanjani kwa kuwahoji watunzi. Vilevile, mtafiti aliwahoji wataalamu na wanafunzi wenzake. Aidha mtafiti alichanganua tamthilia hizi mbili teule ili kupata data iliyokusudiwa ili kutimiza matakwa ya utafiti huu. Data iliyokusanywa ilirekodiwa na kuchanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na nadharia ya Baada Ukoloni. Data zilizokusanywa zimewasilishwa kwa njia ya maelezo. Kazi hii imewasilishwa kwa sura tano. Utafiti huu umeonyesha kwamba utandawazi ni mbinu mpya ya kisasa ya kuendeleza ukoloni mamboleo dhidi ya mataifa maskini.

YALIYOMO. UKURASA

Ikirari ........................................ (i)
Kutabaruku ........................................ (ii)
Shukrani ........................................ (iii)
Ikisiri ........................................ (v)
Yaliyomo ........................................ (vi)
Istilahi muhimu ........................................ (ix)
Akronimu na vifupisho ........................................ (x)
SURA YA KWANZA ........................................ 1
1.0. Utangulizi ........................................ 1
1.1. **Usuli** ........................................ 1
1.2. Suala la utafiti ........................................ 8
1.3. Maswali ya utafiti ........................................ 9
1.4. Malengo ya utafiti ........................................ 9
1.5. Sababu za kuchagua mada ........................................ 10
1.6. Upeo na mipaka ya utafiti ........................................ 12
1.7.0. Misingi ya nadharia ........................................ 13
Nadharia ya baada ukoloni ........................................ 13
1.8.0. Yaliyoandikwa kuhusu mada ........................................ 18
1.8.1. Utafiti wa awali ........................................ 18
1.8.2. Maandishi ya kijumla ........................................ 22
1.9.0. Mbinu za utafiti ........................................ 26
1.9.1. Mbinu ya nyanjani ........................................ 26
1.9.2. Utafiti wa maktabani ........................................ 26
1.9.3. Uteuzi wa sampuli ........................................ 27
1.9.4. Ukusanyaji wa data ........................................ 27
1.9.5. Uchanganuzi wa data ........................................ 28
1.9.6. Uwasilishaji wa data ........................................ 29
1.1.0. Kiishilio ........................................ 29

2. SURA YA PILI ..................•. ........................................................ 29

**2.0 Utangulizi** .................................................................... ".29

2.1 Alamin Mazrui ..........................................•..................................... 29

2.2 Kimani Njogu ..................•..................................................•......... 32

**2.3 Said A.** Mohamed ................................................................. **36**

2.4 Kingei G. Kitula ..........................................•............................... 40

2.5. Waandishi na ukoloni marnboleo kama utandawazi .... ................................................. 42

2.6. Kiishilio ...................................................................~ ............................................ 43

3. SURA YA TATU: .........................•............................................... 44

Maudhui ya ukoloni mamboleo katika utandawazi .•.......................•........•........ 44

3.0 Utangulizi .................' .............................•......................................... 44

3.1 Muhtasari wa tamthilia ....•..••.•....•...•.....•............................•.•. ..••. ... . ... 44

3.2 Maudhui ya ukoloni mamboleo katika utandawazi .......................•.•............ 47

3.3 Mtindo kama mkakati wa kuendeleza ukoloni mamboleo na utandawazi ........•...... 52

3.3.1 Mpangilio wa tamthilia ...•........•............ 0.................... ................................ 53

3.3.2 Usimulizi .........•....•......••...............................................•...•......... 56

3.3.3 Matumizi ya nyimbo na ushairi ........................................................................... 57

3.3.4 Kuchanganya ndimi ....•.....•..•........•.... ........................................60

3.3.5 Tamathali za usemi ........•............................................ ......................................... 62

3.4. Kiishilio ... . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .
. . . . . . . . . . ...................................................................................................69

SURA YA NNE: ........................ ....................................................................... .......70

4.0. Utangulizi . ............................... .........•........... ............................................ .......70

4.1. Vipindi vya kihistoria katika tamthilia . .•....... ............................................•... ..... 70

4.1.1. Kipindi cha utumwa .............., ...................................................................... ........70

4.1.2. Kipindi cha ukoloni mkongwe ........................................................................ ........71

4.1.3. Kipindi cha ukoloni rnamboleo ...................................................................... ........76

4 . : di h d . 79
.1.4. ipm 1 c a utan awazi ........................................................................................ .

4.2. Maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi ..................................•....... 81

4.3. Mtindo kama mkakati wa kuendeleza ukoloni
mamboleo na utandawazi ....... . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . ........... ..
91

4.3.1. Mpangilio wa tamthilia ........................................................................................91
4.3.2. Usimulizi 92
.
4.3.3. Matumizi ya j azanda ..........................................................................................93
4.3.4. Matumizi ya taswira ............................................................................................ 95
4.4. Kiishilio ........................................................................................................................96
5. SURA YA TANO .................•........•..........•.....................•............. 97
5.0. Utangulizi ................................................................................................................ 97
5.1. Muhtasari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .
. . . . . . . . . . . . . . . .. 97
5.2. Matokeo ya utafiti ...........................................................................................99
5.3. Mchango ..................................................................................................................106
5.4. Matatizo
.....................................................................................................................................
107
5.5. Mapendekezo .............................................................. 108
Marejeleo ............................................................................................................ 109
Viambatanisho
Kiambatanisho cha kwanza: Ratiba ......................................................................... **113**
Kimbatanisho cha pili: Makadirio ........................................................................... **114**
Kiambatanisho cha tatu: Hojaji . .......................................•................................. **115**

**ISTILAID MUHIMU**

i. Utamaduni Mseto - Utamaduni unaoibuka kutokana na maingiliano ya tamaduni za kigeni na zile asilia. Ni mchanganyiko wa tamaduni mbalimbali.

ii. Ulimwengushaji - kufanya ulimwengu kuwa na utamaduni sawa hasa utamaduni wa Kimagharibi. Ni kupokezwa tamaduni za kigeni kupitia mfumo wa utandawazi.

iii, Dunia Ya Tatu - Nchi ambazo hazijaendelea sana katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo. Hizi ni nchi ambazo hazina uwezo wa kiuchumi kujiendeleza. Ni nchi maskini ambazo zinajumuisha mataifa mengi ya Bara la Afrika.

AKRONIIVIU NA VIFUPISHO

1. CHAKAMA : Chama Cha Kiswahili Cha Afrika Mashariki.
2. CRAKITA : Chama Cha Kiswahili Cha Taifa.
3. NOMA : National Online Media Association.
4. K.B.C : Kenya Broadcasting Corporation.
5. C.P.E : Certificate of Primary Education.
6. C.S.C : Cambridge School Certificate.
7. IMF : International Monetary Fund.
8. W.T.O : World Trade Organization.
9. IDRC : International Development Research Centre.
10. M.A : Master of Arts.
11. U.S.A : United State of America
12. C.S.C : Cambridge School Certificate.
13. RA.T : British American Tobacco.



W· ·IVITT41INIVFR&ITY LIB . 'AM

# SURA **YA KWANZA.**

## **1.0** Utangulizi

Katika sura hii, tumeshughulikia mambo ya kimsingi kama vile usuli wa utafiti, swala la utafiti, maswali ya utafiti na malengo ya utafiti. Vile vile, sababu za kuchagua mada na umuhimu wake, up eo na mipaka ya utafiti, misingi ya nadharia na udurusu wa maandishi yanayohusiana na suala la utafiti yalishughulikiwa. Aidha, sura hii imehitimishwa kwa kufafanua mbinu za utafiti na mbinu za uchanganuzi zilizotumiwa.

## **1.1** Usuli

Ubeberu na ubepari si dhana mpya katika historia ya maendeleo ya binadamu. Hoja hii inathibitishwa na habari chungu za ubeberu, ukoloni na harakati za kupambana na hali hizi zinaendelea katika dunia ya tatu, na hasa Afrika. Katika kile ambacho kinaoenekana kama historia kujirudia, wanasayansi ya siasa wameunda mane no kama vile ubeberu mamboleo, ukoloni mamboleo ili mradi kutofautisha ubeberu na ukoloni mkongwe katika mazingira ya sasa. Lakini ukoloni na ubeberu unabaki uleule (Joseph Mihangwa, 2007).

Mmoja wa wanafasihi mashuhuri wanaozungumzia ubeberu ni William Shakespeare ambaye kame nne zilizopita aliviandika vitabu kama *The Merchant of Venice* mwakawa 1594. Kitabu hicho kilitafsiriwa kwa Kiswahili na Mwalimu Julius Nyerere kama *Mabepari wa Venisi*. Katika kitabu hiki, Shakespeare

anathibitisha kuwa ubepari, ubeberu na ukoloni ni dhana kongwe katika historia ya binadamu. Katika mwaka wa 1606 aliandika *The Tempest.* Hiki kitabu kilitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Mushi S.S. katika mwaka wa 1969 kama *Tufani.* Katika hadithi ya Pro spero na Caliban katika *Tufani,* Shakespeare aliigiza utekelezaji wa saikolojia ya utumwa wa kiuehumi kabla ya dhana hiyo haijawa ya kimataifa.

Pro spero ambaye ni mgeni katika kisiwa eha Caliban, anaingia kisiwani kwa lugha ya ujanja na kuwa kama rafiki wa Caliban. Caliban anachukuliwa kama mtu asiye na utamaduni. Kama ilivyokuwa kwa Prospero, wakoloni wa zama zetu walijua na kuhofu nguvu ya umma dhidi ya njama zao na ili kuishinda njama hiyo walianzisha vita vya kisaikolojia. Hapa Mwafrika aliehukuliwa kama mtu hohe hahe, mweusi, mehafu aliyekataliwa na jamii yake na mtu aliyelaaniwa. Utamaduni wa Mwafrika ulipondwapondwa na akawa hana mashiko au mizizi.

Wakoloni wa zama zetu waliwapokonya misingi ya uhai wa jamii zao na wakaanza kuzivunjavunja taasisi zao asilia na mifumo ya siasa na uchumi uliowaunganisha na kupandikiza mifumo yao. Chinua Achebe katika *Shujaa Okonkwo* (1958), anasema kuwa Mzungu alikuwa amefanikiwa kukata uzi uliotuunganisha na kuusambaratisha. Bara la Afrika liliweza kugeuzwa na kuwa eneo la mawindo ya rasilimali kwa nehi za Ulaya kwa kwanzisha na kuwarithisha mifumo ya kigeni ya uchumi, dini na elimu huku wakibebeshwa mizigo ya madeni kugharamia mifumo yao. Baada ya kupata uhuru wa bendera, Mwafrika aliendelea na kujaribu kurejesha heshima yake iliyopotea. Waliotawaliwa hawakuwa na uhuru

wa kujiamulia jinsi nchi zao zingeweza kuendelezwa kiuchumi, kisiasa, kijamii na hata kiutamaduni. Baada ya nchi nyingi za Kiafrika kupata uhuru, wanajamii wa bara la Afrika walikuja kufahamu kuwa uhuru waliopata ulikuwa uhuru wa bendera tu. Ingawaje wakoloni waliondoka, waliweza kuendeleza sera zao kwa umbali na sura tofauti.

"Ukoloni mamboleo" ni neno linalotumiwa na wakosoaji wa baada ya enzi ya ukoloni ulioelekezwa kwa nchi zilizostawi kuingilia masuala ya nchi zinazoendelea. Waasisi wa nadharia ya ukoloni mamboleo wanadai kwamba kulikuwepo na mipangilio ya kifedha iliyoanzishwa na wakoloni ambayo ilitumiwa kudhibiti enzi za wakoloni na wenzao baada ya vita vya dunia. Ukoloni mamboleo ni istilahi inayoweza kuchanganya na kukosoa ukoloni halisi sasa, (ambapo baadhi ya mataifa ya kigeni yanaendelea kusimamia nchi walizozitawala katika mfumo wa ukoloni). Katika ukoloni mamboleo mifumo ya kiuchumi kama vile biashara binafsi na makampuni ya biashara za kigeni yanaendelea kunyonya nchi maskini na kunyonya rasilimali za mataifa maskini baada ya enzi ya ukoloni. Ukoloni mamboleo ni upeo wa wafadhili wa kuendeleza utawala wao dhidi ya mataifa yanayoendelea. Ukoloni mamboleo ni kushiriki kwa nchi zenye nguvu ya kiuchumi katika mambo ya nchi zisizokuwa na nguvu za kiuchumi. Vile vile, ukoloni mamboleo ni aina ya mfumo wa kisasa unaoendelezwa na nchi zenye nguvu katika nchi maskini na kuingilia mifumo yao ya kisiasa, kiuchumi na hata kitamaduni.

Ukoloni mamboleo unadhihirika katika nyanja nyingi za maisha ya binadamu hasa katika nchi maskini za Kiafrika. Kama anavyosema Nkurumah (1957), wakoloni walitumia njia nyingi kama vile misaada ya kifedha na majeshi kuendeleza utawala wao. Ukoloni mamboleo ulitumika kama njia kuu ya kuendeleza, kueneza na kudumisha utawala wa kikoloni. Che Guevara, (1965) anasema kwamba ubeberu ulikithiri na kuendelea kudhibiti nchi zilizotawaliwa. Huu ndio anaoita ukoloni mamboleo. Wakoloni waliweza kutumia misaada ya kifedha kama njia ya kunyonya nchi maskini. Ufadhili huu uliendelea kuongeza mwanya kati ya nchi maskini na nchi tajiri ulimwenguni. Kwa kawaida wafadhili hao hutoa mikopo ya pesa kwa nchi maskini ili kuzalisha bidhaa vya kilimo, ujenzi wa barabara na maendeleo mengine. Baadaye wanaopewa mikopo hiyo hulazimishwa kuilipa mikopo. Kutokana na uvivu wa kufikiria wa viongozi wengi wa nchi maskini, umaskini na ujinga unaendelea kukithiri katika nchi zao. Viongozi hawa hukubaliana na matakwa ya wakoloni ambao kutokana na utandawazi wamehalalisha na kuimarisha ukoloni mamboleo. Wakoloni hawa huendelea kuwanyonya wananchi mbele ya macho ya serikali zao. Pia mashirika ya kimataifa yaliweza kutumiwa kufadhili miradi mbalimbali na ambayo haikumnufaisha mwananchi wa kawaida. Wakoloni waliendelea kutumia huduma za kijeshi ili kuendeleza na kudumisha utawala wao. Nchi kama vile Amerika na Uingereza ziliweza kutumia mbinu hii kule Siera Leone. Wafaransa nao walitumia mbinu zingine kudumisha utawala au serikali

waliyoona kuwa na urafiki nao na kubomoa zile ambazo hazikudumisha uhusiano bora nao.

Kwa ujumla, ukoloni mamboleo ill nJla ya kisasa na ya ubeberu bia inayotumiwa na nchi zilizo na nguvu ya kiuchumi kuzitawala nchi maskini katika ulimwengu wa kisasa. Ukoloni mamboleo hutumia mifumo ya kibiashara na mifumo ya kiuchumi kudhibiti nchi maskini. Benjamin William Mkapa (2005) katika hotuba ya Raisi kwa Muungano wa Tanzania, anasema kuwa mambo yaliyompa faraja ni kuwa nchi tajiri hazijaitendea haki Bara la Afrika. Anasema kuwa Bara la Afrika limenyonywa kupindukia na limeonewa kwa uonevu uliokithiri tangu enzi ya utumwa, hadi ukoloni, ukoloni mamboleo, vita baridi na hata leo kwenye utandawazi.

Kapinga D.S (2004) anasema kuwa utandawazi unachukuliwa kama mwanzo mpya na jitihada za nchi za Magharibi kuwa na dunia inayofuata itikadi moja, siasa moja, uchumi na utamaduni mmoja. Soko huru linalozungumzwa kuhusu utandawazi, siyo la fedha na bidhaa tu, bali pia siasa, itikadi, utamaduni, mawazo na fikra. Anaendelea kusema kuwa utandawazi ni mfumo unaozipendelea nchi zilizoendelea. Hali hii imekuwa hivyo tangu mahusiano na maingiliano ya kiuchumi, kimataifa kati ya wakolonina koloni zao yaanze zaidi ya Kame tano zilizopita. Uhusiano kati ya nchi za Ulaya na Marekani na nchi za Dunia ya Tatu umekuwa ni wa uporaji tu. Ukoloni ndio ulioimarisha mfumo huo wa uporaji kwa

kuamua makoloni yazalishe nini na kwa soko gani na bei gani. Baada ya uhuru, hali hiyo haikubadilika, mfumo wa uchumi ulibaki ule ule.

Nchi tajiri zimeendelea kutumia nguvu za kisiasa katika kuendesha na kuendeleza sera za uchumi wa dunia. Nchi hizo hutumia njia na mbinu tofauti tofauti ili kudhibiti sera za uchumi. Zinatumia hata mabalozi wao kuingilia nchi maskini kwa visingizio vya kusimamia matumizi bora ya misaada yao. Nchi nyingi, hasa za Bara la Afrika hazijafanikiwa kujinasua na minyororo ya ukoloni mamboleo.

Uhuru wa nchi haujaleta matunda yaliyodhamiriwa na watetezi wa uhuru. Hii ill kwa sababu kuwa wakoloni waliendelea kuwekea nchi changa mikakati inayosababisha kudidimia kwa nchi hizo. Uhusiano uliopo baina ya nchi zilizotawaliwa na zile zilizowatawala hudhihirika katika uhusiano wa kijamii, kisiasa na hata wa kiuchumi. Kulingana na mabadiliko yaliyomo duniani, njia mpya ya kuendeleza udhibiti huu imegunduliwa ambayo ni utandawazi. Utandawazi huhusishwa zaidi na utandawazi wa kibiashara. Kule kuunganika kiuchumi katika uchumi moja kwa njia ya biashara, uzalishaji mali wa kigeni, urudikaji wa rasilimali, uhamiaji, kuenea kwa teknolojia ni dhihirisho kuu ya utandawazi.

Utandawazi ni mfumo ambao hatuna budi kuishi nao kwa kutumia VIZUfl fursa unazotoa na kutumia hata mabaya yake kwa manufaa yetu. Utandawazi uliweza kusukumwa na mambo yafuatayo:

(i) Msukumo wa kibepari wa faida: Tamaa ya mabepari ya kupata faida imesababisha mapinduzi makubwa katika uchumi. Soko huru la fedha na

mitaji limekua na kujipenyeza kila mahali na hasa katika nchi za Ulaya Mashariki, Asia na Marekani ya Kusini.

**(ii)** Maendeleo katika sayansi na teknolojia ya uzalishaji huduma na habari na mawasiliano ambayo yamerahisisha sana biashara ya fedha, mitaji, bidhaa na huduma.

(Hi) Kuanguka kwa dola la Shirikisho la Kisovieti la Kisosholisti la Urusi (USSR) na washirika wake (nchi za kijamaa za Ulaya ya Mashariki). Utandawasi umeifanya dunia kuwa na itikadi moj a, siasa ya kidemkrasia ya vyama vingi, mfumo wa uchumi na kuenea duniani kwa utamaduni wa Marekani na washirika wake. Nchi za Dunia ya Tatu na zilizokuwa za kikomunisti zipo katika hatua mbali mbali za utekelezaji wa marekebisho ya uchumi, ukiwemo ubinafsishaji wa mashirika ya umma.

**(iv)** Matumizi ya nguvu za kisiasa katika kuendesha uchumi wa dunia.

Kwa mujibu wa Said A. Mohamed (1999), utandawazi si dhana mpya, bali ni upeo wa dhana kongwe yenye sifa mpya ya kutumia maendeleo makubwa yaliyopatikana kiteknolojia, kunyonya kwa map ana na marefu, utajiri wa dunia na kuwaacha watu wa nchi maskini kuwa maskini zaidi. Mbali na kuwaacha maskini, utandawazi pia huchafua uchumi, tamaduni na maisha yao vibaya hadi kufikia nchi hizo kudharauliwa na kuonekana si lolote, si chochote katika fikra ya dunia ya leo.

Suala la utandawazi limekuwa tatizo sugu. Utandawazi ni suala ambalo faida na madhara yake ni mengi. Hivyo basi utandawazi umekuwa mbinu

yakuendeleza ukoloni mamboleo. Utandawazi ni mfungamano na uhusiano unaojitdihirisha katika biashara na uchumi na katika utamaduni baina ya jamii tofauti ulimwenguni. Utandawazi utofautiana na mahusiano mengine pale ambapo unaambatana na mabadiliko ya kijamii katika teknolojia. Ni kutokana na suala hila ndipo mtafiti aliamua kuchunguza jinsi masuala ya ukoloni mambo leo na utandawazi yanavyoonyeshwa katika tamthilia za *Sudana na Posa za Bikisiwa.* Said A Mohamed na Kitula King'ei (2008) katika *Posa za Bikiswa* na Alamin Mazrui na Kimani Njogu (2006) katika *Sudana* wamezungumzia suala la utandawazi, ukoloni mamboleo katika nchi za Afrika. Mtafiti amejaribu kubainisha na kue1eza vipengele mbali mbali vya ukoloni mamboleo katika utandawazi katika tamthilia hizi mbili teule.

## 1.2 . Swala la utafiti.

Utafiti huu umejikita katika tamthilia mbili: *Posa za Bikisiwa* ya Said A Mohamed na Kitula. King' ei (2008) na *Sudana* ya Alamin Mazrui na Kimani Njogu (2006). Utafiti huu umejishughulisha na swala la ukoloni mamboleo katika muktadha wa utandawazi. Katika utafiti huu mtafiti ameainisha, ameeleza na amechanganua vipengele mbalimbali vya ukoloni mamboleo na usawiri wake katika utandawazi kwa kuzingatia tamthilia za *Posa za Bikisiwa* na *Sudana.* Mtafiti ameonyesha jinsi ukoloni mamboleo unavyofasiriwa na kuendelezwa kiutandawazi katika tamthilia zilizoteuliwa. Kwa kufanya hivyo, mtafiti ameonyesha uhusiano

wa karibu uliopo kati ya ukoloni mamboleo na utandawazi kama mifumo hii ilivyo onyeshwa katika *Posa za Bikisiwa* na *Sudana.*

## 1.3. Maswali ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:-

(a) Kuna uhusiano gani kati ya ukoloni mamboleo na utandawazi?

(b) Ukoloni mamboleo na utandawazi unajitokezaje katika tamthilia mbili teule?

*(c)* Ukoloni mamboleo na utandawazi una athari gani katika tamthilia za *Posa za Bikisiwa na Sudana?*

*(d)* Mtindo gani wa kisanii umetumiwa na waandishi kuelezea utandawazi?

## 1.4. Malengo ya utafiti.

Malengo ya utafiti ni:

(a) Kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ukoloni mamboleo na utandawazi kama unavyofasiriwa na tamthilia za *Posa za Bikisiwa* na *Sudana.*

*(b)* Kuonyesha jinsi utandawazi unavyotumika kuendeleza ukoloni mamboleo kama unavyojitokeza katika tamthilia za *Posa za Bikisiwa* na *Slid ana*

*(c)* Kubainisha athari za ukoloni mamboleo na utandawazi katika *Posa za Bikisiwa* na *Sudana.*

(d) Kubainisha mtindo unaotumiwa na watunzi kuelezea utandawazi.

## 1.5. Sababu za kuchagua mada

Suala la ukoloni mamboleo na utandawazi ni suala sugu katika jamii na nchi maskini. Dunia ya Tatu huonyeshwa kama nchi ambazo hazijaendelea. Tatizo la ukoloni mamboleo huwa ni jambo linalowasakama na kuangamiza mataifa machanga katika juhudi zao za kujikomboa kisiasa, kiuchumi na hata kijamii. Kuna haja ya kuonyesha kinagaubaga uhusiano uliopo kati ya ukoloni mamboleo na utandawazi katika nchi maskini. Kilio cha Waafrika, husikika mara kwa mara katika juhudi zao za kujikomboa kimawazo na hata kiuchumi. Kuna haja pia ya kuonyesha dhima ya utandawazi katika kuendeleza ukoloni mamboleo. Pia, mataifa maskini yanaendelea kuangamia kutokana na utegemezi wao wa misaada kutoka mataifa fadhili.

Sababu nyingme ya kuchagua mada hii ni kutathmini kwa undani jinsi ukoloni mamboleo unavyohusiana na utandawazi. Baadhi ya wataalamu wameusifu utandawazi wakidai kwamba umewaleta wanajamii wa ulimwengu katika kijiji kimoja. Rata hivyo waandishi wa Kiafrika wa kileo wanaliona swala hili vingine. Wanafikiria kwamba utandawazi ni kimelea na maendeleo katika dhana ya ukoloni na ukoloni mamboleo. Pia suala 1a ukombozi wa mataifa machanga limekuwa ni jambo muhimu. Ufadhili na utegemezi wa misaada umeendelea kufukarisha nchi nyingi za Kiafrika. Pia mifumo mbaya ya uongozi ndio chanzo cha umaskini uliokithiri katika nchi nyingi za Kiafrika.

Mtafiti alikusudia kufafanua maana ya utandawazi na kueleza athari za utandawazi kwa binadamu. Sababu nyingine ya kuchagua mada ni kuonyesha jinsi utandawazi unavyojidhihirisha na kujitokeza kwenye fasihi ya Kiswahili. Fasihi ya Kiswahili inaendelea kushughulikia masuala ya kimataifa. Kwa hivyo ilipasa mtafiti aonyeshe jinsi masuala haya yalivyoshughulikiwa katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili.Vitabu hivi viwili vimechaguliwa kimaksudi. Pia ni vitabu vya hivi karibuni kwani *Sudana* (2006) na *Posa* za *Bikisiwa* (2008). Hivi ni vitabu vinavyoangazia ulimwengu wa kisasa na kushughulikia masuala ibuka katika jamii. Sababu nyingine ni kuonyesha jinsi ukoloni mamboleo hueneza sera zake hasa kwa nchi maskini.

Rata hivyo, mtafiti ameonyesha kuwa si kila athari zote za utandawazi zilizohasi, na kwa hivyo ameonyesha umuhimu wa utandawazi katika jamii ya kisasa. Matatizo makubwa ni jinsi ya kukabiliana na athari za utandawazi katika jamii. Jambo hili limewafanya viongozi wengine kufanywa vikaragosi vya mataifa fadhili. Vile vile, kuingiliwa kwa mifumo ya kisiasa na nchi tajiri umekuwa tatizo sugu. Vitabu hivi viwili vimechaguliwa kwani vimefanikiwa kwa kiwango cha juu kudhihirisha waziwazi jinsi ukoloni mamboleo umekithiri katika jamii kupitia utandawazi. Mara nyingi nchi maskini zimeshindwa kukabiliana na matatizo na athari za utandawazi. Kwa hivyo tumechagua tamthilia hizi mbili ili kuweza kutathmini athari za utandawazi kwa jamii.



KENYATTA UNIVERSITY CITY LIBRARY

Mabadiliko ya kisiasa, kiuehumi na biashara, na hata katika vyombo vya habari vimeshughulikiwa na tamthilia hizi mbili. Vile, vile, waandishi wa vitabu hivi viwili wamefanikiwa kutupa picha halisi jinsi nehi fadhili zinavyoeendelea kunyanyasa nehi maskini huku wakijifanya kuwa wao ni marafiki na ambao wangependa kuwasaidia. Pia wakoloni wameendeleza sera zao kwa nchi ehanga kupitia viongozi ambao huwa na mawazo na mitazamo ya kikoloni.

Vile vile mada hii imeehaguliwa ili kujadili kwa nini baadhi ya viongozi wanatumiwa kama vikaragosi wa wakoloni ambao bado wanaendeleza sera na mifumo ya wakoloni katika nehi zao. Mada hii imeehaguliwa ili kubainisha wazi juhudi za wakoloni kuendelea kunyanyasa, kufyonza na kudhulumu nchi maskini katika mfumo wa utandawazi. Uliberali na sera za kiuehumi na biashara vimetumika kama vyombo vya ukandamizaji na unyonyaji wa nehi za Kiafrika.

**1.6. U peo na mipaka ya utafiti**

Huu ni utafiti wa kifasihi na umeshughulikia tamthilia mbili: *Posa za Bikisiwa* na *Sudana.* Vitabu hivi viwili ni vya hivi karibuni kwani *Sudana* kiliehapishwa mwaka wa 2006 na *Posa Za Bikisiwa* ni eha mwaka 2008. Tamthilia hizi zinaangazia uhusiano kati ya utandawazi na ukoloni mamboleo Vitabu hi vi ni miongoni mwa kazi za sanaa ambazo zimeshughulikia suala la ukoloni mamboleo na utandawazi. Tamthilia hizi mbili zimeteuliwa kimaksudi. Tunaamini kuwa vitabu hivi vina hoja za kimsingi ambazo zinadhihirisha uhusiano baina ya ukoloni

mamboleo na utandawazi na zinaweza kutafitiwa. Katika utafiti huu, tumejifunga katika kutathmini ufasiri wa ukoloni mamboleo katika muktadha wa utandawazi. Mifumo ya uchumi na biashara imeangaziwa zaidi. Rata hivyo sera zingine zinazojitokeza katika utandawazi zimeangaziwa na kushughulikiwa. Utafiti huu pia umezingatia athari za utandawazi katika jamii za kisasa.

## 1.7.0 Msingi wa nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Baada ukoloni au ki-baada ukoloni.

### Nadharia ya baada ukoloni

Nadharia ya baada ukoloni ni zao la jitihada na jaribio la kutaka kuzirekebisha hali fulani kuhusu jinsi mataifa ya Kimagharibi yanavyoziangalia nchi zilizokuwa koloni zao. Mitazamo ya mataifa haya imekuwa na sifa fulani hasi au mbaya. Uhakiki wa ki-baada ukoloni ni aina ya uhakiki ambao unahusishwa na mikabala ya mitazamo ya fasihi ya wasomi na wataalamu wa jamii zilizokuwa chini ya utawala wa kikoloni (Wamitila 2003). Msingi mkubwa wa mtazamo huu ni juhudi za kuzirekebisha 'picha' zilizonazo nchi za Kimagharibi kuhusiana na nchi nyingi zinazoelezwa kama "Ulimwengu wa Tatu". Nchi nyingi za Kimagharibi zimekuwa na mitazamo hasi ya nchi hizo pamoja na raia wake. Picha zao zimejitokeza katika mandishi yao, usemi wao na picha nyingi zinazosambazwa.

Katika miaka ya 1950, Frantz Fanon ambaye ni nguzo kuu ya uasisi wa nadharia hii aliandika kitabu cha *Black Skins, White Masks*. Fanon anasema kuwa

binadamu hastahili kufungiwa kwa njia zozote zi1e bali ni hatima yake kuwa huru. Anaendelea kusema kuwa binadamu hastahili kubaguliwa kwa misingi yake ya rangi. Kulingana na Fanon, mtu mweupe hudhihirika katika rangi yake nyeupe na Mwafrika katika rangi yake nyeusi. Mwafrika anang'ang'ana na kujitambua yeye ni nani. Utamaduni wa Mwafrika huathiriwa na utamaduni wa Magharibi. Mwafrika anatumia lugha ya Kiingereza ambayo ni lugha ya kujifunza.

Katika miaka ya 1960, Fanon alichapisha kazi yake nyingine maarufu ya *The Wretched of the Earth* Hii ni kazi ambayo iliyaibua na kuyaweka wazi masuala yanayohusiana na ubaguzi wa Kimagharibi na jinsi ubaguzi huo unavyokuwa msingi mkubwa wa kuendelea kushikilia nguvu na kwa njia hiyo kuwalazimisha waliotawaliwa kutumia nguvu kijinasua. Anasema kuwa njia moja ya kuondoa ukoloni na athari zake ni matumizi ya nguvu. Kulingana na Fanon, machafuko mbalimbali yanaweza kutumiwa na Waafrika kijikomboa. Machafuko haya ni kama vile: uchokozi au ushari hasa wa maneno na vitendo, kushurutisha au kulazimisha, matumizi ya nguvu, kuumiza mwili au saikolojia na matumizi ya kijeshi

Fanon anaendelea kusema kuwa njia ya kujikomboa ni matumizi ya harakati za kutumia silaha. Harakati huitajika ili kuweka nchi huru kutokana na wakoloni na kumfanya binadamu kufahamu kutokana na kutengwa kunakotokana na ukoloni. Anatoa sababu nne za kutumia nguvu nazo ni.

(a) Kurejesha utu kwa mwenyeji

**(b)** Kama njia ya kukidhi machafuko yaliyoletwa na walowezi

(c) Kubomoa mifumo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi iliyoletwa na wakoloni.

(d) Kujenga umoja katika harakati za ukombozi.

Kwa mujibu wa Frantz Fanon (1963), lugha za kiasili na fasihi zake zilikoseshwa thamani na makao, na mtawaliwa akanyang'anywa lugha na utamaduni wake. Jambo hili lilimfanya mtawaliwa kuwa kiumbe ambacho hakina utamaduni asili. Mtawaliwa hujikuta aking'ang'ana na kujikuta baina ya kujitimbulisha na maadili ya kikoloni, na uangamizaji utokanao na mporomoko wa maadili ya kiasili. Uhakiki wa baada ya ukoloni hujaribu kufafanua na kueleza uhusiano uliopo baina ya nchi zilizotawaliwa na wakoloni na nchi zilizowatawala

Kinadharia, kitabu cha Said E *Orienta/ism* (1978), ni msingi mkuu wa uhakiki wa ki - baada ukoloni. Katika kitabu hiki, Said anachunguza jinsi nchi za Kimagharibi zinavyoisawiri jamii ya Kimashariki, picha ilizo nazo potofu zinavyoathiri mahusiano yake. Said anafafanua njia za Kimashariki zinazotumiwa kudhibiti, kuunda na kuendeleza utawala wao.

Kwa mujibu wa Kimani Njogu na Rocha Chimerah (1999), uhakiki wa baada -ukoloni ni juhudi ya kuelewa uhusiano uliopo baina ya mataifa yaliyotawaliwa na yaliyotawala. Uhakiki wa Jumuiya ya Madola wa miaka ya sitini ulikuwa umedai kwamba mataifa yanayotawaliwa hayakuwa na hiari ila kuandika kwa Kiingeereza. Kulingana na mtazamo huu, fasihi iliyosifiwa ni fasihi andishi na iliyoendelezwa

kwa lugha ya Kiingereza. Kiingereza na fasihi yake ilichukuliwa kama chombo cha ukandamizaji. Lugha na fasihi huwa ni vinyang'anyiro vya mvutano baina ya wenye nguvu za kiuchumi na wasio na nguvu. Watawaliwa walilazimishwa kujifunza lugha za kikoloni kwa sababu lugha za kiasili zilinyimwa nafasi ya kukua na ikabidi zingine zife. Unyamazishaji ni uti wa mgongo wa uhakiki wa Ki -baada ukoloni:

(a) Mna unyamazishaji wa wanawake wa mataifa ya pembezoni.

**(b)** Unyamazishaji na ububu wa watawaliwa wote popote walipo, wake kwa waume.

Unyamazishaji huu unajikita katika nyanja zote za maisha ya binadamu kama vile kisiasa, kitamaduni, kiuchumi na hata kiisimu. Baada ya kudhihirisha ukandamizaji wa kiisimu, mkondo huu wa uhakiki unasherekea kurejea kwa kauli za watawaliwa. Nchi za pembezoni zinaonyeshwa zikiibuka na kutwaa utamaduni na lugha za mataifa tawala. N chi hizi zinaukabili utamaduni wa kigeni: zinaufinyanga, zinaupinda, zinaupeperusha peperusha, zinaumba huku zikiumbua ndimi za Kimagharibi na utamaduni wao kupitia sajili za pembezoni. Hatimaye, panapatikana utamaduni inseto wenye sauti kali kutoka pembezoni.

Kutokana na mitazamo mbalimbali ya nadharia ya baada - ukoloni, mihimili ifuatayo inajitokeza:

Kwanza, lugha ya Kiingereza na fasihi yake ni vyombo vya ukandamizaji. Ulazimishaji wa lugha za Kimagharibi kwa mataifa yaliyotawaliwa ni juhudi ya kutweza mchango wa mataifa yaliyotawaliwa katika kueleza mazingira. Lugha kama

chombo cha mawasiliano ilitumiwa kuleta utandawazi. Pia kuna njia zingine za kiuchumi na kitamaduni zinazotumiwa kuwakandamiza watawaliwa ambazo zimechangia utandawazi. Mhimili huu umetumiwa kuonyesha vile lugha inavyotumiwa kuendeleza unyanyazaji na ukandamizaji wa binadamu katika nyanja zote za maisha katika nchi maskini.

Pili, unyamazishaji ni uti wa mgongo wa uhakiki wa baada ukoloni. Kuna unyamazishaji wa wanawake wa mataifa ya pembezoni, na unyamazishaji na ububu wa watawaliwa wote popote walipo, wake kwa waume. Unyamazishaji tunaozungumzia hapa ni wa kisiasa, kitamaduni na kiisimu. Mhimili huu umetumiwa kuonyesha jinsi wakoloni wanavyonyanyasa na kutawala nchi za Kiafrika kupitia mifumo ya kisiasa na kidemokrasia katika utandawazi.

Tatu, fasihi ya pembezoni huchukuliwa duni kwa sababu mbinu za kisanii hazifungamani na mbinu za kisanaa za Kimagharibi. Kuna kauli zilizoteuliwa na ambazo zinachukuliwa kuwa kweli kwa vile zimetokana na watawala. Mhimili huu umetumiwa kuonyesha jinsi fasihi simulizi imekoseshwa nafasi katika mfumo wa utandawazi.

Nne, hudhihirisha juhudi za **"ulimwengushaji"** wa usorni wa Kimagharibi. Nadharia hii imeonyesha namna udhibiti wa utamaduni wa nchi za Kimagharibi unavyovunj a kutokana na miigo na takriri za nchi tawaliwa. Maingiliano haya yamesababisha kuwepo kwa "utamaduni mseto" Mhimili huu umetumiwa kubainisha na kuonyesha

vipengele via utamaduni wa wakoloni na athari zake katika nchi za kiafrika kwa kurejelea tamthilia mbili teule.

Tano, inawanasibu watawaliwa kuasi dhidi ya watawala katika vipengele vyote vya maisha. Mhimili huu umetumiwa kuonyesha juhudi za watawaliwa za kujikomboa kutokana na mfumo wa utandawazi.

## 1.8.0. Yaliyoandikwa kuhusu mada.

Katika sehemu hii tumeshughulikia aina mbili za maandishi.

### 1.8.1 Utafiti wa awali

Hakuna utafiti wowote uliofanyiwa tamthilia hizi mbili teule. Hata hivyo kuna watafiti waliotafiti juu ya ukoloni mamboleo na pia utandawazi. Maandishi ya wahakiki ya kijumla yamesaidia katika utafiti wetu.

Said A. Khamisi (1999), anasema kuwa neno utandawazi Iilianza kuingia maskioni na kuzama akilini mwetu kuanzia miaka ya 1980. Anasema kuwa utandawazi ni neno dhahania mno na lenye maana nyingi. Neno utandawazi linaelezea mfungamano na uhusiano uliyojitokeza katika miaka ya theladhini iliyopita hasa katika biashara, uchumi na utamaduni. Mtafiti huyu alishughulikia jinsi lugha ya riwaya mpya za Kiswahili zinavyodai. Alishughulikia kipengele cha Iugha kama alama mojawapo ya mtindo, yaani lugha katika uhusiano wake na utandawazi. Lugha inayotumika katika kazi fulani ya fasihi huathiriwa na nini kinachotokea katika jamii yenyewe ambamo mwandishi huchota fikira, maudhui,



KENYATTA UNIVERSITY LIBR

falsafa, itikadi, jazanda, mitindo, maumbo na miundo - lugha. Riwaya hizi mpya ni zile za Euphrase Kezilahabi za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1990), riwaya ya Katama Mkangi ya *Walenisi* (1995), riwaya ya W.E. Mkufya ya *Ziraili na Zirani* (1999), riwaya moja ya Mohamed ya *Babu Alipofufuka* (2001) na miswada yake miwili ya *Dunia Yao* na *Mkamandume*, riwaya moja ya Wamitila ya *Bina -Adamu* (2002) na riwaya ya Chachege ya *Makuadi wa Soko Hurta* (2002). Utafiti huu umejikita katika utanzu wa riwaya na ni tofauti na utafiti wetu. Utafiti wetu pia umelenga kuonyesha jinsi ukoloni mamboleo unavyofasiriwa katika muktadha wa utandawazi. Kinyume na utafiti wake, utafiti wetu haujishughulishi na suala la lugha katika utandawazi. Rata hivyo fasiri yake ya utandawazi imekuwa msingi wa utafiti wetu.

Mhakiki John M. Mbonde (2004) katika uchambuzi na uhakiki wa riwaya ya Chachage Seithy L. Chachage ya *Makuadi wa Soko Huria* anashughulikia maudhui, muundo na mtindo. Miongoni mwa maudhui aliyoshughulikia ni dhuluma na hujuma, siasa na uchumi, uongozi, rushwa na utapeli, ukale na usasa, nafasi ya mwanamke katika jamii, mapenzi na ndoa, dini, vyombo vya habari na utandawazi na mali asili na mazingira. Katika maudhui ya vyombo vya habari na utandawazi, alionyesha jinsi vyombo vya habari vinavyoweza kuibua hisia na pia kuchokonoa ukweli wa mambo. Anasema kuwa wanahabari wanaweza kufaulu kuigufusha serikali na asasi mbalimbali kuhusu vitimbwi vya uhalifu na ukiukaji sheria. Kinyume na utafiti wetu, hakushughulikia jinsi ukoloni mamboleo unavyojitokeza

katika utandawazi. Utafiti ulioshughulikiwa katika kazi hii ni tofauti na huo kwa sababu haushughuliki kuonyesha jinsi ukoloni mamboleo unavyofasiriwa katika utandawazi. Pia utafiti wake umejikita katika riwaya lakini wetu ni katika utanzu wa tamthilia.

Gromov (2004), katika utafiti wake, alijishughulisha na kuonyesha jinsi vipengele vya usasaleo vinavyojitokeza katika riwaya mpya za Kiswahili. Miongoni mwa dhamira zinazojitokeza katika utafiti wake ni utandawazi. Kwake alidhamiria kuonyesha jinsi lugha na picha zinavyotumika kuelezea dhana ya utandawazi. Anaonyesha jinsi waandishi wanavyotumia lugha kuelezea tatizo la utandawazi. Hata hivyo, Gromov hakushughulikia tatizo la ukoloni mamboleo katika utandawazi. Anaendelea kusema kuwa ni katika miaka ya 1980 ndipo usasabaadaye ulipopata upana wa matumizi katika nyanja za kifalsafa, utamaduni na pia katika fasihi na uhakiki wa kifasihi. Lengo kuu la usasabaadaye, kinyume na uhalisia na usasa ni kuonyesha kutoweza kwa mwanadamu kuufahamu ulimwengu. Utafiti huu ni tofauti na utafiti wetu. Huu haulengi kuonyesha jinsi utandawazi unavyofasiriwa katika kazi za kifasihi. Utafiti huu ulinuiwa kuonyesha jishi ukoloni mamboleo unavyojitokeza katika utandawazi kwa kurejelea tamthilia mbili teule za *Sudana na Posa za Bikisiwa*.

Mhakiki Yared Magori Kihore, (2005), naye alishughulikia suala la utandawazi na ufundishaji wa Kiswahili. Katika utafiti wake, alionyesha jinsi ufundishaji wa Kiswahili unaweza kufanywa katika dunia ya utandawazi kwa

kuhusisha juhudi za nchi zinazozungumza Kiswahili hasa Afrika Mashariki na Kati. Alichunguza dhana ya utandawazi yenyewe na kubaini kwamba kama dhana mpya kwa sehemu kubwa ya dunia, watu wengi hawajaelewa maana yake. Anasema kuwa utandawazi ni tukio la kuunganishwa kwa karibu kwa masoko ya bidhaa na huduma na vilevile mtaji. Ufafanuzi huu unaashiria mwegemeo wa kiuchumi ambao ndio msingi wa utandawazi. Lengo lake kuu ni kuonyesha jinsi ufundishaji wa Kiswahili unavyoweza kutekelezeka chini ya mazingira mampya yaliyokita katika misingi ya utandawazi. Ingawa Kihore ameshughulikia dhana ya utandawazi, hajaonyesha kinagaubaga vile utandawazi unavyojitokeza kama njia mpya ya kuendeleza ukoloni mamboleo. Hata hivyo, umekuwa msingi wa utafiti wetu. Pia lengo la utafiti wetu ni kuonyesha jinsi ukoloni mamboleo unavyojitokeza katika misingi ya utandawazi. Utafiti wetu ulinuia kuelezea vipengele vya ukoloni mamboleo na kuonyesha uhusiano uliopo baina ya ukoloni mamboleo na utandawazi.

Simala Inyani (2001), alishughulikia suala la fasihi simulizi katika enzi ya utandawazi.Anasema kuwa athari ya utandawazi kwa asasi na taasisi ni kubwa. Mabadiliko na mageuzi makubwa yanayotokana na nguvu na mielekeo ya utandawazi yanatoa changamoto nyingi kwa binadamu kote ulimwenguni. Lengo lake kuu ni kuonyesha umuhimu wa fasihi simulizi na kuonyesha jinsi ya kuipa kipaumbele asasi hii katika maendeleo. Mtafiti huyu aliweza kuonyesha waziwazi athari za utandawazi kwa uamilifu wa fasihi simulizi katika jamii. Utafiti wake ni tofauti kabisa na wetu kwani ulijihusisha na utanzu wa fasihi simulizi. Utafiti wetu umeshughulikia utanzu

wa tamthilia. Vile vile, Simala hakujadili jinsi ukoloni mamboleo unavyojitokeza katika kipindi na sera za utandawazi. Utafiti huu basi umekusudia kufafanua, na kuonyesha vipengele vya ukoloni mamboleo katika maendeleo ya kijamii.

### 1.8.2 Maandishi ya kijumla,

Kuna waandishi wengi ambao wameshughulikia mad a ya ukoloni mamboleo na wengine utandawazi. Maoni yao yatachangia utafiti wetu. Kapinga D.S (2004) anasema kuwa utandawazi hutumika kuipa dunia sura inayofanana na mahusiano katika kijiji kupitia kwa teknolojia ya habari na mawasiliano. Uundaji wa mazingira ya utandawazi ambao sifa yake kubwa ni ushindani katika soko la dunia ambayo kutokana na mapinduzi katika teknolojia ya upashanaji habari imekuwa kama kijiji. Anaendelea kusema kuwa utandawazi ni mfumo unaozipendelea nchi zilizoendelea. Hali hii imekuwa hivyo tangu mahusiano na maingiliano ya kiuchumi ya kimataifa yaanze zaidi ya kame tano zilizopita.

Tume ya Dunia kuhusu athari za kijamii za utandawazi imebaini kwamba nchi za Dunia ya Tatu (maskini) zimeathirika sana katika maeneo yafuatayo: mfurno wa Dunia wa uzalishaji ambao umezifanya ziendelee kazalisha na kuuza nje bidhaa ghafi ambazo bei zake huendelea kushuka katika soko la dunia, utegemezi wa bidhaa za viwanda na teknolojia ya kisasa katika uzalishaji na huduma, ongezeko kubwa la idadi ya watu wasio na kazi na hasa vijana, kuwafanyisha kazi watoto wa chini ya miaka 15, hivyo kuwakosesha elimu na kuwaingiza katika mzunguko usio na

mwisho wa umaskini na dhiki na athari katika utamaduni. Athari za utandawazi katika jamii, na hasa kuiga tamaduni za magharibi ni za kutisha.

Kwa kawaida, utandawazi umechochea na kuleta: mmonyoko wa maadili katika jamii na tamaa ya utajiri wa haraka haraka ambayo imeondoa uaminifu/juhudi katika kazi na kuleta uhalifu wa kutumia silaha, utapeli, uingizaji wa bidhaa hafifu nchini.

Nyanja ya starehe na burudani. Imetawaliwa na matendo yanayoibua hisia za ngono na kuehoehea ufuska hivyo kuyafanya mapambano dhidi ya UKIMWI kuwa kama mehezo wa kuigiza. Picha zinazoonyeshwa kwenye runinga huchoehea vijana wengi kujiingiza katika mambo ya ngono. Pia kuibuka kwa vyama vya kisiasa na asasi zisizo za kiserikali ambayo huchoehea vurugu na uvunjifu wa sheria na mshikamano wa taifa.

Mwandishi huyu ameshughulikia suala la utandawazi kwa jumla. Hajaelezea jinsi utandawazi ulivyotumika kuendeleza ukoloni mamboleo. Rata hivyo, ufafanuzi wake wa utandawazi umeehangia katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu kuwa utafiti wetu umelenga kuonyesha jinsi ukoloni mamboleo umefasiriwa katika muktadha wa utandawazi.

Nehi nyingi za Afrika hazijaweza kuwa na uwezo wa kushindana na mataifa tajiri katika mifumo ya utandawazi. Nehi matajiri ndizo zinazomiliki mambo ya kimsingi kuhusu utandawazi. Jambo hili hufanya nehi maskini kutegemea misaada na kuleta dhana ya uehumi tegemezi. Huu ndio ukoloni mamboleo. Baada ya uhuru

KENYATTA UNIVERS

nchi nyingi za Kiafrika hasikufanikiwa kujikomboa kutokana na uchumi wa kibepari wa kimataifa, yaani ubeberu.

Rodney (1972), katika kitabu chake *Jinsi Ulaya ulivyoleta Maendeleo duni ya Afrika (How Europe Underdeveloped Africa)*, ameonyesha mtazamo kuwa Afrika kwa maksudi ilinyonywa na kurudishwa nyuma kimaendeleo na serikali za kikoloni za Ulaya. Mchanganyiko wa nguvu za kisiasa na unyonyaji wa 'kiuchumi wa Afrika na Ulaya ulichangia pakubwa hali mbaya ya kisiasa ya Afrika na maendeleo. Rata hivyo hajaonyesha jinsi utandawazi unavyotumika kuendeleza ukoloni mamboleo. Utafiti huu umelenga kuziba ili pengo na kudhibitisha kuwa utandawazi ni mbinu ya kisasa ya kuendeleza ukoloni mamboleo dhidi ya nchi maskini.

Utandawazi ni sehemu mojawapo ya maendeleo katika jamii na ambao umebadili mwelekeo wa jamii nyingi duniani. Sehemu ya maisha ya jamii iliyoathirika zaidi ni utamaduni. Mawazo ya watu wachache, utamaduni wao, mila na desturi zao, namna zao za kuishi kila siku, zimechukuliwa kuwa ndio mawazo ya namna ya kuishi ya watu wote ulimwenguni.

Ukoloni mamboleo ni matokeo ya ufadhili wa nchi chang a na unaotumiwa kunyanyasa nchi hizo na kuachwa bila maendeleo. Kwa mujibu wa Salisu (2004), nchi zilizotawaliwa baada ya kupata uhuru wao, bado watawala waliendelea kudhibiti uchumi wao. Anasema kuwa matokeo ya uhuru hayakuleta mabadiliko yaliyo kusudiwa. Baada ya nchi nyingi kupata uhuru, tofauti zilianza kuibuka

miongoni mwa wanajamii ambazo baadaye zilileta hata vita vya wenyewe kwa wenyewe, kama vile katika nchi za Congo, Nigeria, Malasya n.k.

Nchi tawala zilizua mbinu mpya zilizosababisha kuanguka kwa nchi maskini. Uhusiano baina ya nchi tawala na zilizotawaliwa katika nyanja za kijamii, siasa na uchumi ni mfano mzuri. Jinsi ulimwengu ulivyoendelea kupita mabadiliko mbalimbali, ukoloni mamboleo ndivyo ulivyoendelea kukidhiri.Kuliibuka mbinu mpya ya unyanyasaji kupitia utandawazi.Utandawazi umeendelea kuwa changamoto katika jamii hasa nchi maskini. Nchi nyingi za Afrika, zinaendelea kutengwa katika soko la dunia na pia umaskini unazidi kuongezeka. Udhibiti wa watu na rasilimali unaendelezwa katika misingi ya utandawazi kupitia mashirika ya kifedha ya dunia kama vile, Shirika la Fedha la Dunia (IMF) na Shirika la Biashara la Dunia (W.T.O.) ambayo huruhusu nchi chache tajiri kudhibiti uchumi wa dunia. Mwandishi huyu hajaweza kufafanua uhusiano uliopo baina ya ukoloni mamboleo na utandawazi. Hivyo basi mtafiti amejaribu kuonyesha jinsi utandawazi ulivyo mbinu mpya ya kuendeleza ukoloni mamboleo katika nchi maskini.

Ngugi T. (1993), akielezea kuhusu mabadiliko ya kijamii, anasema kuwa sura ya Kame ya ishirini ni zao la mtafaruku wa kani mbili kinzani, kwa upande moja kuna ubeberu ambao ulichangia kutwezwa kwa kundi la wanyonyaji na lisilozalishi katika uongozi dhidi, si tu kwa umma katika nchi moja bali pia dhidi ya nchi na mbari kadhaa ulimwenguni. Kwa upande mwingine, kuna mwamko wa kijamii ambao ulipigania mabadiliko ya uongozi kwa niaba na kwa mitazamo ya tabaka zalishi la jamii.

Anaendelea kuelezea kuwa ubeberu umejidumisha uongozini kwa njia tatu: kunyonya koloni kongwe na koloni-rnamboleo, kujihami dhidi ya mwamko wa umma au ubeberu mwingine hasidi na kujihaini dhidi ya uwezo wa umma kwa kutumia ukandamizaji wa kijamii, ujinsia na hata migawanyiko ya kidini. Mwandishi huyu hajaonyesha jinsi ukoloni mamboleo unavyoendelezwa katika misingi ya utandawazi. Hata hivyo, maoni yake yamechangia pakubwa katika utafiti wetu.

## 1.9.0 Mbinu za utafiti

Katika kufikia azma zetu, mtafiti alitumia mbinu za nyanjani na mbinu za maktaba.

### 1.9.1. Mbinu ya nyaniani

Utafiti huu ulitumia mbinu za nyanjani kupata data juu ya maisha ya waandishi wa tamthilia hizi mbili teule na pia kuhususiana na suala la utandawazi na ukoloni mamboleo. Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano na waandishi kwa kutumia hojaji. Pia mtafiti alikuwa na majadiliano ya ana kwa ana na wataalamu na wanafunzi wenzake ili kupata tajriba ya kutosha

### 1.9. 2 Utafiti wa Maktabani,

Utafiti huu umefanyiwa katika maktaba. Utafiti wa maktabani umehusu kusoma kwa kina vitabu, majarida, majuzuu, tasnifu na machapisho mengine

yaliyohusiana na mada yetu ya utafiti. Kusoma huku kumemwezesha mtafiti kujenga msingi bora wa kulifahamu pengo la utafiti na yaliyoandikwa kuhusu mada.

Mtafiti amelenga kusoma yale yaliyoandikwa kuhusu utandawazi na ukoloni mamboleo na vile unavyoingiliana. Utafiti wa maktabani umemwezesha mtafiti kupata mwelekeo wa nadharia na kukusanya data zilizofaa, kuchanganua na kuwasilisha matokeo.

### 1.9.3. Uteuzi wa sampuli,

Utafiti huu umetumia sampuli ya maksudi. Utafiti huu ulilenga vitabu mahsusi ambavyo vina vipengele muhimu vya kuviwezesha kuchunguzwa. Vitabu viwili vya *Sudana na Posa za Bikisiwa* vimechunguzwa. Vitabu hivi viliteuliwa kimaksudi na kuwa vimetupatia data ya kutosha katika uchunguzi wetu. Utafiti huu umelenga kundondoa vifungu au mane no au sentensi zinazodhihirisha ya kwamba ukoloni mamboleo kulingana na maelezo yanayopatikana katika utangulizi upo na unaweza kubainishwa kama utandawazi.

### 1.9.4 Ukusanyaji wa data.

Data ya utafiti huu imekusanywa kutoka kwa tamthilia mbili za *Posa za Bikisiwa na Sudana.* Mtafiti atavisoma vitabu hivi kwa kina na kuyatenga kwa kuandika mambo yote yaliyo muhimu kwa utafiti huu katika daftari. Mambo yaliyotengwa ni pamoja na maudhui ya ukoloni mambo lea na utandawazi na mtindo uliotumika katika uwasilishaji.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa data.

Data iliyopatikana baada ya kudondolewa, kutengwa na kunukuliwa imechanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na nadharia ya baada ukoloni. Katika uchanganuzi, mtafiti amebainisha vipengele vya ukoloni mamboleo kama vinavyofasiriwa katika utandawazi. Ufafanuzi zaidi juu ya vipengele hivyo umetolewa. Pia maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi yameonyeshwa.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa data.

Data zilizokusanywa zimewasilishwa kwa njia ya maelezo. Uwasilishaji wa data umezingatia malengo ya utafiti kwa misingi ya baadhi ya mihimili ya nadharia ya Baada - Ukoloni. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maandishi ya kinathari.

## 1.10. Kiishilio

Katika sura ya kwanza tumetanguliza utafiti wetu unahusu nini. Mada ya utafiti imeangaziwa. Aidha tumeelezea yale yaliyoandikwa kuhusu mada yetu ya utafiti. Maswala na malengo ya utafiti yamegusiwa na tumetoa sababu za kuchagua mada yetu ya utafiti. Hatimaye, up eo wa utafiti, nadharia iliyotumiwa katika utafiti imefafanuliwa na pia mbinu za utafiti zimeelezewa. Katika sura ya pili, tutashughulikia maisha ya waandishi wa *Sudana*, Alamini Mazrui na Kimani Njogu na waandishi wa *Posa Za Bikisiwa*, Said A. Mohamed na Kitula King' ei. Tutachunguza maendeleo ya mawazo yao katika uandishi wao kuhusu suala la utandawazi na ukoloni mamboleo.

# SURA YAPILI

## 2.0. Utangulizi

Katika sura ya kwanza tuliitambulisha mad a ya utafiti huu ambayo ni kuonyesha kuwa utandawazi ni mbinu mpya ya kuendeleza ukoloni mamboleo kama unavyofasiriwa katika tamthilia za *Sudana* (2006) ya Alamin Mazrui na Kimani Njogu na *Posa za Bikisiwa* (2008) ya S.A Mohamed na Kitula King' ei. Maswala na malengo ya utafiti pia yalishughulikiwa. Tulijadili yaliyoandikwa kuhusu mada. Sababu za kuchagua mada tunayoishughulikia zilifafanuliwa na upeo wa utafiti wetu kuelezewa. Nadharia tuliyoitumia pia ilielezewa na hatimaye mbinu za utafiti.

Katika sura hii tumeshughulikia historia ya watunzi wa tamthilia hizi mbili teule, Alamin Mazrui, Kimani Njogu, Said A. Mohamed na Kitula King'ei. Katika kufanya hivyo tumeweza kuelewa wamekuwa wakiandika kwa kutumia mitindo gani. Waandishi hawa wote walizaliwa na kukulia katika mazingira ya ukoloni. Pia wameona mengi kuhusu mabadiliko yanayofanyika katika ulimwengu wa kisasa. Hivyo basi wameungana pamoja kutunga kazi za kifasihi zinazoangazia mabadiliko haya hasa ukoloni mamboleo na utandawazi.

## 2.1. AI - Amin Mazrui.

Alamin Mazrui alizaliwa mwaka wa 1948, Kisiwani Lamu. Alizaliwa katika ukoo uliotambulika sana wa Mazrui. Babake alikuwa mfuasi wa masomo na kazi ya kidini ya Uislamu. Alamin Mazrui ni mpwa wa Ali Mazrui ambaye ni mtaalamu wa

masuala ya kisayansi na siasa. Alamin Mazrui alijitenga na masomo ya kidini ya babake kinyume na alivyotarajia babake. Alamin Mazrui alisomea shahada yake ya kwanza katika Chuo kikuu cha Rutgers kule Amerika na kufuzu na shahada yake ya Sayansi (B.SC Biology). Pia alipata shahada yake ya Uzamili (M.A), katika lugha katika chuo hicho hicho.

Katika mwaka wa 1980, alifuzu na shahada yake ya Uzamifu katika Isimu katika Chuo Kikuu Cha Stanford. Amekuwa Profesa katika idara ya African American Studies katika Chuo Kikuu Cha Ohio (Ohio State University) mwaka wa 1989 - 2004. Aidha ni mhadhiri katika Chuo Kikuu Cha Rutgers katika idara ya lugha za Kiafrika na Fasihi. Mnamo miaka ya1980, Alamin Mazrui aliwekwa kizuizini pamoja na wasomi wengine waliopinga uongozi wa serikali ya Daniel T. Moi. Baada ya kutoka kizuizini mwaka wa 1984, alikimbilia maisha yake kule Amerika. Mwaka wa 1988 alichapisha kitabu chake cha kwanza *Chembe Cha Mayo*, ambacho ni mkusanyiko wa mashairi yake yanayosheheni hali ya kisiasa nchini Kenya.

Alamin Mazrui ni mwandishi na mtafiti ambaye ameshughulikia masuala mengi kama vile: Sosiolojia ya kisiasa ya lugha katika Afrika na kwa Waafrika walio nchi za nje, Fasihi ya Kiafrika katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili Uchanganuzi wa kiutamaduni kwa haki za binadamu Barani Afrika, musuala ya Dini ya Islamu kama kitambulisho kwa Waafrika waliomo barani na walio nje ya bara. Pia

anashughulikia masuala ya Afrika baada ya Ukoloni kama vile: Siasa za Korani na mengmeyo.

Alamin Mazrui amekuwa mtetezi wa haki za binadamu na uhuru wa kijamii na ameandika ripoti kuhusu mada mbalimbali kama vile "Bandits and the Politics of Citizenship; The case of Galje'el of Tana River" (Mombasa), Muslims for human rights (1999), Media Censorship in Plural Context: A report on the Kenyan Broad Casting Corporation. London: Article 19 (International Centre against Censorship), 1998; Kaya's Revizited: A Post - Election Balance Sheet. Nairobi (Kenya): Kenya Human Rights Commission, 1998 na zinginezo. Kama mwandishi, Alamin Mazrui amejihusisha na masuala mengi yanayohusiana na siasa Barani Afrika kama vile: utamaduni, masuala ya kidini, ukoloni, ukoloni mamboleo, ukombozi, ukoloni mamboleo na utandawazi miongoni mwa mengine.

Baadhi ya vitabu alivyoandika ni kama vile: *The Tower of Babel: Language and Governance in African Experience* (1998) alichokiandika akiwa pamoja na Ali Mazrui, Mhariri akiwa na Willy Mutunga, *Debating the African Condition:* Volume 1: *Race, Gender and Culture Conflict and Volume* 2: *Governance and Leadership (2004), Sudana* (2006) alichoandika akiwa na Kimani Njogu, na *Swahili Beyond the Boundaries: Literature, Language and Identity* (2007), Alamin Mazrui pia ameandika makala mengi kama vile: *Globalization* and the *Social Linguistics of the Internal: Between English and Kiswahili* (2008), Beyond *Appropriation: Language, Knowledge and Discourse in the Africa.* Between *English and Swahili Literature.*

*Research in African Literatures* (1996). Haya ni baadhi ya maandishi yake. Hali halisi ya maisha yake ndiyo imechangia pakubwa katika kushughulikia suala la ukoloni mamboleo katika utandawazi.

Al - Amin Mazrui ameishi na kuona mengi wanayofanyiwa mataifa ya Afrika na mataifa ya Kimagharibi. Pia amejishughulisha na masuala mengi kuhusu utawala na uongozi. Kwa kuwa mtetezi wa wanyonge katika jamii, amejikita kwa kuangazia maovu ya kijamii katika mifumo mbalimbali ya utawala. Hii ndio inayompa motisha wa kushughulikia suala la ukoloni mamboleo katika utandawazi. Kwa mujibu wake, lengo la utandawazi ni kuendeleza dhuluma katika mataifa maskini.

**2.2.** Kimani Njogu

Kimani Njogu alizaliwa mwaka wa 1953 katika wilaya ya Nakuru kaunti ya Nakuru. Alisomea Shule ya msingi ya Kipkelion Mjini ambako alifanya mtihani wake wa darasa la saba (C.P.E) mwaka wa 1967. Katika mwaka wa 1968, alijiunga na Shule ya Upili ya Taita Towett hadi mwaka wa 1971. Katika miaka ya 1972 -75 alijiunga na Chuo Cha Kenyatta ambako alisomea masomo yake ya diploma (SJ) na kuwa mwalimu wa Kiswahili. Aliweza pia kusomea mtihani wake wa kidato cha sita kama mtahiniwa wa kibinafsi katika mwaka wa 1980 - 81. Baadaye alijiunga na Chuo Kikuu Cha Nairobi alikofuzu na shahada yake ya kwanza ya ualimu (REd Arts) katika mwaka 1985. Alisomea somo la fasihi ya Kiingereza, Kiswahili na

ualimu. Katika mwaka wa 1987, alihitimu na shada yake ya Uzamili ya Isimu katika Chuo Kikuu Cha Nairobi (M.A. Linguistics). Mwaka wa 1990, pia alipata shahada nyingine ya uzamili ya Falsafa ya Isimu ya Chuo Kikuu Cha Yale. Kimani Njogu ni mhadhiri na mwandishi wa vitabu vya fasihi. Alianza kazi yake ya uandishi mnamo miaka ya 1970 alipokuwa katika shule ya Sekondari. Alianza kuandika michezo ya kuigiza iliyowasilishwa katika kipindi cha mchezo wa wiki (Jumapili) katika idhaa ya K.B. C. Baadaye katika miaka ya 1986 - 89, 92 - 95, aliweza kuandika mchezo wa kuigiza kwa redio uitwapo "Ushikwapo Shikamana" na "Kuelewana na Kuzungumza" .

Kimani Njogu ni mwandishi aliyeshughulikia masuala mbalimbali katika jamii yakiwemo masuala ya lugha, fasihi, kijamii na hata uraia. Baadhi ya vitabu alivyoandika ni kama vile *Falsafa ya Shaaban Robert* katika riwaya zake (1986), *Mwongozo wa Mukwava wa Uhehe* (1986), *Riwaya za Visiwani Zanzibar* na *mwamko wa kisiasa* (1987), *Mwongozo wa Kilio Cha Haki* (1988), *'Grassroots Standardisation of Swahili'* Democratically speaking (1992), *'Decolonizing the Child:* Paintbrush Vol. 20 nambari 39 na 40, Spring and Autumin (1993). *'Reversal as Reply in Kiswahili Poetry:* Two example' *The Egerton Journal Vol: 1 Number 2, (1996), Uhakiki wa Riwaya za visiwani Zanzibar* (1997), *Mwongozo wa Amezidi* (1997), Mwongozo wa *Siku Njema* (1998), *Tanzu za Lugha* (Kitabu Cha Mwalimu) *(1999), ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu* (1999), *Mwongozo wa Kilio Cha Haki* (2001), *Embe Tamu* (2004), *Tanzu za lugha Kitabu* Cha 1, 2, 3 na 4 (2004-

2005) na *Zilizala* (2006). Aidha Kimani Njogu ameshirikiana na waandishi wengine katika kuandika vitabu vingine. Akiwa na Aswani na Mwihaki, *Sarufi ya Kiswahili: Uchanganuzi na matumizi* (2006), akiwa na Aswani na Mwihaki, *Isimu Jamii kwa wanafunzi* (2006), akiwa na Alamin Mazrui, *Sudana* (2006), akiwa na R. M. Wafula, *Nadharia ya Fasihi* (2007). Pia ameandika pamoja na wengine *Kamusi ya Karne ya ishirini na moja* (2011) na *Kamusi Kibindoni* (2011). Ameandika makala mengi kuhusu masuala ya kijamii kama vile *Leadership, Youth and Culture (2007), Governance and Development: Towards Cultural Leadership in Kenya (2007), Globalized Identity: Diaspora Kenyans and Local Conflict* (2011), *Putting out the Flames. The Kenya National Dialogue Process* (2011) miongoni mwa mengine.

Kimani Njogu ni mkurugenzi wa Twaweza Communications. Hili ni shirika linaloshughulikia masuala ya utawala na uongozi Barani Afrika. Shirika hili limejihusisha na njia zingine za kuchangia suala la uongozi hasa kwa lugha za Kiafrika. Ni shirika ambalo linaegemea upande wa sanaa, utamaduni na matumizi ya vyombo vya habari kwa kushughulikia masuala mbalimbali kuhusu jamii kwa kutumia wasomi na washikadau wengine katika masuala ya uongozi na utawala

Ni msomi wa masuala ya lugha, fasihi, vyombo vya habari na masuala ya utawala hasa kwa mabadiliko ya kijamii. Kutokana na tajriba yake, ameweza kuonyesha mambo yanayowaathiri wanajamii. Kupitia katika uandishi wake, ameshughulikia masuala ibuka katika jamii. Aidha Kimani Njogu ameshikilia nyadhifa nyingi katika maisha yake. Kutoka mwaka wa 1980 - 81, alikuwa mmoja

wa wanakamati wa Rift Valley Drama Association, 1980 - 81, katibu mtendaji wa Kericho District Drama Association, 1983 - 85, Mwenyekiti wa Professor Kibera Poetry Association, Chuo Kikuu Cha Kenyatta, 1984 - 85, Mwenyekiti wa Kiswahili Association, Chuo Kikuu Cha Kenyatta, 1989 - 91, mwanakamati wa "Yale-Stanford Kiswahili Poetry Video Project", kutoka mwaka wa 1989 hadi leo, mwanakamati wa Kenya Oral Literature Association, 1992 - hadi leo, mwanakamati wa Kenya Writers Association. Pia ni mmoja wa wanachama wa Chama Cha Kiswahili Cha Afrika Mashariki (CHAKAMA), ni mwenyekiti wa Chama Cha Kiswahili Cha Taifa (CHAKIT A) - Kenya (Kamati ya Kiswahili ya taifa) na Kamishna wa Kiswahili Cross Border Commission.

Kimani Njogu ametunukiwa tuzo mbalimbali kama vile: 1985 - mwanafunzi bora katika Kiswahili katika idara ya lugha ya Kiswahili na fasihi katika Chuo Kikuu Cha Kenyatta. Ni mshindi wa mwaka wa 2001 katika Global Award for Excellence Best Radio Program in Population Reporting katika mchezo wake wa kuigiza wa 'Ushikwapo Shikamana,' idhaa ya KBC Nairobi; pia ni mshindi wa tuzo ya NOMA mwaka 2000 kupitia kwa kitabu chake: *Ufundishaji 1va Fasihi. Nadharia na mbinu.* Kimani Njogu anakubali kuwa Alamin Mazrui ndiye aliyeanzisha uandishi wa tamthilia ya *Sudana.* Anasema kuwa aliweza kujiunga naye baadaye katika kukamilisha uandishi wa tamthilia ya *Sudana.* Kilichowachochea kuandika tamthilia hii ni mvutano uliomo baina ya mataifa ya Bara la Afrika na yale ya Magharibi. Kumekuwa na mivutano kadhaa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii baina ya mataifa



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

haya. Kimani Njogu anakiri kuwa utandawazi ni mbinu mpya na ya kisasa ya kuendeleza ukoloni mamboleo. Utandawazi ni mbinu ya kisasa inayoendelezwa katika teknolojia na inayodhihirika katika mifumo ya kiuchumi. Katika mahojiano ya ana kwa ana anasema kuwa mataifa ya Bara la Afrika hayana mchango wowote katika mfumo huu wa utandawazi. Hata hivyo anakubali kuwa mbinu hii mpya ikitumika vizuri inaweza kuleta manufaa kwa Waafrika.

## 2.3. Said A. Mohamed.

Said A. Mohamed alizaliwa Unguja (Zanzibar) katika mwaka wa 1947. Alisomea shule kadhaa za msingi na shule ya sekondari Visiwani Zanzibar. Baadaye mwaka wa 1974 alijiunga na Chuo Kikuu Cha Dar – es – Salaam kusomea shahada ya B.A (Elimu). Mwaka wa 1981, alihitimu katika chuo hicho na shahada ya uzamili (M.A) ya Isimu. Alifundisha katika idara ya Kiswahili chuo hicho kwa muda mrefu. Baadaye katika mwaka wa 1982 – 1985, alijiunga na Chuo Kikuu cha Leipzig, Ujerumani kwa shahada ya uzamifu. Baada ya masomo yake ya uzamifu, alirudi kwao na kufanya kazi katika Taasisi ya Kiswahili na lugha za Kigeni, Unguja kama mkurugenzi. Ni mhadhiri aliyefundisha visiwani Zanzibar, vyuo vikuu vya Nairobi na Moi nchini Kenya na chuo kikuu cha Osaka nchini Japani. Amekuwa mhadhiri katika chuo kikuu cha Bayreuth nchini Ujerumani alipokuwa akifundisha fasihi ya Kiafrika hadi mwaka 2013 alipostaafu na kurundi nyumbani Tanzania.

Said A. Mohamed alianza kazi yake ya uandishi mnamo miaka ya 1960 alipokuwa katika shule ya msingi. Alitunga mashairi yaliyosomwa siku za wazee na mengine kutangazwa katika idhaa iliyokuwa ikiitwa "Sauti ya Unguja" wakati ule (Mohamed 2001: 1993). Katika miaka hiyo ya 1960, idhaa ya Kiswahili ya BBC ilianzisha mashindano ya uandishi wa hadithi fupi za Kiswahili. Aliweza kushiriki katika mashindano hayo. Mojawapo ya hadithi alizoandika ni '*Msiba Wa Pamoja*' katika *Hekaya za Kuburudisha*. Mnamo miaka ya 1970, S.A. Mohamed alianza kuandika vitabu vya misemo. Miongoni mwa vitabu hivi ni kama vile *Vito Vya Hekima, Methali na Misemo ya Mshangao na Milio na Tashbihi*. Pia alianza kuandika riwaya. Riwaya yake ya kwanza ni *Asali Chungu* (1978). Ameandika riwaya zingine kama vile *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Kiza Katika Nuru* (1988), *Tata za Asumini* (1990) na *Babu Alipofufuka* (2001). Said A. Mohamed pia ni mwandishi wa mashairi na tamthilia. Diwani za mashairi alizotunga ni *Sikate Tamaa* (1980), *Kina cha Maisha* (1984) na *Jicho La Ndani* (2001). Miongoni mwa tamthilia alizotunga ni *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaishi* (1990), *Amezidi* (1995), *Kitumbua kimeingia Mchanga* (2001), *Dunia Yao*, (2006) na kile ambacho ameandika pamoja na Kitula King'ei, *Posa za Bikisiwa* (2008). Pia ameandika vitabu vingine kama vile: *Nyuzo za Mwanamke* (2008), *Mhanga Nafsi Yangu* (2011), *Janga la Werevu* (2011), *Mkama Dume* (2012) na *Kimya Kimya Kimya* (2012).

Said A. Mohamed, amejihusisha na uandishi mwingi kwa kuangazia masuala yanayoikabili jamii hasa za Waafrika. Kazi zake zote zinaweza

kugawanywa katika vipindi mbali mbali vya uandishi wake. Kuna vitabu alivyoandika kushambulia maovu ya kijamii. Katika maandishi haya, anachora jamii iliyo nzuri. Katika jamii hii pia kunatokea watu ambao huharibu utaratibu ama kwa kukiuka maadili ya kidini na kukatiza hali nzuri iliyotarajiwa na wanajamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Utengano* (1980), Bwana Maksudi anasawiriwa kama mnafiki na mfisadi. Ana tabia ya kushiriki kimapenzi nje ya ndoa na Kazija ilhali yeye ni Shehe. Hata kama Maksudi alipigania uhuru, baada ya kupata uongozi aliweza kuasi na kuanza kuwanyanyasa wananchi waliomchagua. Ni watu kama hawa ambao Said A. Mohamed anadhimiria kuasa.

Pia mwandishi ameandika kazi nyingi zinazoonyesha migogoro na mivutano ya kiuchumi iliyomo katika jamii. Mifano ya kazi hizi ni kama vile *Dunia Mti Kavu* (1980), *Utengano* (1980) na *Kiza Katika Nuru* (1988). Mwandishi katika vitabu hivi anaonyesha kuwa matatizo ya jamii yanatokana na mitafaruku ya kiuchumi, kitabaka na unyonyaji. Suluhu ya matatizo haya ni mapinduzi yatakayoleta usawa kati ya wanajamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Utengano* (1980), wananchi wanaamua kuwatimua mamlakani watu kama Maksudi, watu wasiojali maslahi ya umma na maskini katika jamii. Said A. Mohamed pia ameshughulikia suala la ukoloni mamboleo na utandawazi katika kazi zake ikiwemo tamthilia ya *Posa za Bikisiwa*. Ameandika kitabu hiki katika kipindi cha uhakiki na mkemeo wa utandawazi. Katika uhakiki huu, siasa na mwenendo wa jamii, wanataja kuwa umefika wakati wa Mwafrika ajilaumu mwenyewe juu ya balaa lote linalomkabili.

Wakulaumiwa zaidi ni viongozi na utaratibu wa uongozi unaotumika katika Bara la Afrika. Mohamed katika *Babu Alipofuka* (2001:10) anasema

"Siku hizi Kinying'inya Changu anaweza kuketi meza moja na watu ambao miaka michache iliyopita ilikuwa mwiko kukaa nao. Mazimwi, aliwaita. Akatangaza vita nao kwa kusaidiwa na nyuki--------". Anakemea viongozi wa Afrika ambao wanakubali kukaa pamoja na kula pamoja na mataifa tajiri ambayo yamekuwa chanzo cha dhuluma na ukandamizaji wa nchi maskini.

Hivyo basi, Said A. Mohamed ameshughulikia kwa undani suala la ukoloni mamboleo na utandawazi katika vitabu vyake vingi. Anawakemea viongozi wa Bara la Afrika kwa kukubali uhsiano usio na manufaa kwa wananchi kupitia mfumo wa utandawazi. Kwake, utandawazi ni mbinu mpya ya kuendeleza dhuluma na unyanyasaji kwa mataifa maskini unaofanywa na nchi matajiri. Anaonyesha uhusiano wa kisasa uliopo baina ya mataifa ya Kimagharibi na ya Kiafrika kupitia utandawazi haukuchunguzwa. Hii ni kuwa wanaonufaika zaidi katika mfumo wa utandawazi ni mataifa ya Kimagharibi kuliko ya Kiafrika. Said A. Mohamed anawalaumu viongozi wanaojingiza katika uhusiano wa aina hii bila kuchunguza athari zake.

## 2.4. Kitula G. King'ei.

Kitula King'ei alizaliwa mwaka wa 1952 katika kata dogo ya Tulia, kata ya Mutonguni, Kaunti ya Kitui. Alipata elimu yake ya msingi miongoni mwa shule za msingi za Mutonguni. Alisomea katika shule ya upili ya Mutonguni hadi mwaka wa 1973 alipofanya mtihani wake wa Cambridge School Certificate (C.S.C). Baadaye alijiunga na shule ya upili ya Alliance, Kikuyu ambako alisomea hadi kidato cha sita. Alijiunga na Chuo Kikuu Cha Nairobi na kusomea shahada ya B.A (Elimu) na kuhitimu katika mwaka wa 1979. Alisomea somo la Isimu, Kiswahili na Fasihi kisha kusomea Kiswahili katika kiwango cha uzamili katika chuo hicho hicho cha Nairobi hadi mwaka wa 1983. Amewahi kufundisha katika shule mbalimbali, zikiwemo zile za msingi kama vile Shule ya Msingi ya Kyangalu (1974) ambako alifundisha somo la Kiswahili, Kiingereza, Hesabati na Sayansi ya jamii. Pia alifundisha shule za upili za Muthale (1976), Mumbuni hadi 1980 na Mutonguni hadi 1983, kule alikofundisha somo la Kiswahili, Kingereza na somo la dini.

Mwaka wa 1983, alijiunga na idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kama mhadhiri msaidizi. Alisajiliwa kama mwanafunzi wa Uzamifu mwaka wa 1989 katika Chuo Kikuu cha Howard, Washington DC, U.S.A. Alifuzu mwaka wa 1992. Ni mhadhiri ambaye amefundisha kwa muda mrefu katika Chuo Kikuu Cha Kenyatta katika idara ya Kiswahili na lugha za Kiafrika. Ni mtaalam katika masuala ya fasihi na isimu jamii. Kitula King'ei ni mwandishi mashuhuri wa vitabu vya Kiswahili hasa katika fasihi na Isimu. Ameandika zaidi ya vitabu 15 vya Kiswahili na fasihi kama

vile *Mwongozo wa Malimwengu Ulimwenguni* (1984), *Mwongozo wa Malenga wa Mrima* (1985), *Mwongozo wa Mashetani* (1988), *Kamusi ya Semi za Kiswahili* (1988), *Kamusi ya Methali za Kiswahili* (1989), *Hadithi za Furaha* (1988 – 1989), *Taaluma ya ushairi* (2001), *Misingi ya Fasihi Simulizi* (2005) na *Posa za Bikisiwa* (2008) alichoandika na S.A. Mohamed. Pia ameandika makala mengi katika majarida mbalimbali kama vile: 'Matumizi ya lugha katika maandishi ya Ebrahim Hussein' *Mulika* (1987), '*Inculcating a sense of Responsibility in the Youth*' Kenya Journal of Education Vol. 2, 1989,. '*Swahili Taarab as a Medium of political Expression in Kenya*' in Writers Forum Vol. 2, 1994, *Matatizo ya 'Matumizi ya Lugha katika vyombo vya Habari, mifano kutoka Kenya*' A.A.P Swahili Forum No 64, 2000), '*Kiswahili Technical Terminology: Problems of Development and Usage in Kenya*' Kiswahili Vol. 63, (2000) na '*Nafasi ya Nyimbo za Taarab za Kiswahili katika jamii ya kisasa*' Mulika No. 25 (2002) miongoni mwa mengine.

Kitula King'ei ni mwandishi ambaye anajulikana na ametambulikana sana. Ametunukiwa zawadi nyingi kwa mchango wake katika uandishi kwa kushughulikia masuala mengi kuhusu lugha ya Kiswahili katika jamii na pia juu ya masuala yanayoathiri jamii kwa ujumla. Ametunukiwa tuzo nyingi za hapa nchini Kenya na za Kimataifa. Mifano ni kama vile: 2 National Kiswahili Creative Writing Awards, 1971 na 1983 (iliyopangwa na B.A.T na Ministry of Culture and Social Services), Kenyatta University Deans Research Award (1986), International Development

Research Centre (IDRC) Nairobi, 1986, Kenyatta University's Vice – Chancellor's Publications Award 2000) na The Greater Global Understanding Award 1992

Kitula King'ei pia amewasilisha masuala mbalimbali katika mawasilisho tofauti kama vile: "The Historical and Thematic Development of the Swahili Novel, Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Idara ya Lugha na Isimu, Semina, 1981, "*Themes in Swahili Taarab Songs*", katika semina iliyoandaliwa na idara ya Muziki, Chuo Kikuu Cha Kenyatta, 1986, "*Matatizo ya matumizi ya lugha katika vyombo vya Habari*" katika kongomano la kimataifa la Kiswahili, Mombasa, Oktoba 3 – 6 mwaka wa 2000; "*Globalization of Kiswahili*: The role of Germans from 1848 to 2002, kule DAAD Workshop on Cross – Cultural Studies, Chuo Kikuu Cha Nairobi, Machi 17 – 18, 2005 miongoni mwa mengine.

### 2.5. Waandishi na ukoloni mamboleo kama utandawazi

Waandishi hawa wote wanne walizaliwa katika kipindi cha ukoloni. Walizaliwa wakati mataifa yao yalikuwa chini ya wakoloni. Alamin Mazrui alizaliwa mwaka wa 1948, Kimani Njogu mwaka wa 1953, Said A. Mohamed mwaka wa1947 na Kitula King'ei mwaka wa 1952. Walikulia katika mazingira ya ukoloni. Pia walipoenda shuleni walisoma baadhi ya maandishi ya kikoloni na ukoloni mamboleo. Maandishi haya yalichangia pakubwa katika mitazamo yao dhidi ya ukoloni na ukoloni mamboleo. Waandishi hawa pia wameshuhudia mateso na dhuluma walizofanyiwa Waafrika na wakoloni na pia viongozi waliochukua

uongozi baada ya nchi ya Kenya kupata uhuru. Wengine wao kama vile Alamini Mazrui wameteswa na kufungwa jela na viongozi. Wote pia wamekuwa miongoni mwa juhudi zinazokinzana na ukoloni na ukoloni mamboleo. Ni kutokana na hali hizi ambapo wameshirikiana kuandika vitabu vinavyosheheni ukoloni na ukoloni mamboleo. Wameshuhudia jinsi ulimwengu umebadilika na kuwa ulimwengu unaoongozwa na kutawaliwa na mfumo wa utandawazi. Wamesafiri kwingi na kuona mengi. Wameshuhudia mateso na dhihaka wanazofanyiwa mataifa ya "Dunia ya Tatu"na mataifa yaliyoendelea. Si ajabu basi waandishi hawa wameshirikiana kwa kutunga tamthilia zao. Tamthilia hizi mbili zimedhihirisha kinaga ubaga ukoloni mamboleo katika utandawazi.

**2.6. Kiishilio.**

Katika sura hii, tumeangazia historia ya watunzi wa tamthilia ya *Sudana,* Alamini Mazrui na Kimani Njogu na tamthilia ya *Posa Za Bikisiwa*, Said A. Mohamed na Kitula King'ei. Aidha sura hii imeangazia waandishi na ukoloni mamboleo kama utandawazi. Kwa kufanya hivyo tumeweza kuonyesha jinsi wameshirikiana kuthibitisha mfumo wa ukoloni mamboleo katika utandawazi. Katika sura ya tatu, tutatoa muhtasari wa tamthilia ya *Sudana* ili kuleta ufahamu wa mada yetu, tutaonyesha maudhui ya ukoloni mamboleo katika utandawazi. Aidha sura hii ya tatu itashughulikia suala la mtindo kama mkakati wa kuendeleza utandawazi na ukoloni mamboleo.

# SURA YA TATU:

## MAUDHUI YA UKOLONI MAMBOLEO KATIKA UTANDAWAZI.

### 3.0. Utangulizi.

Katika sura ya pili tumechunguza historia ya waandishi wa tamthilia hizi mbili teule, Alamin Mazrui, Kimani Njogu, Said A. Mohamed na Kitula King'ei. Madhumuni ya kufanya hivyo ni kubainisha mambo yaliyowaelekeza kushughulikia suala la ukoloni mamboleo na utandawazi. Tumeweza kuonyesha kuwa hali ya maisha waliyoishi na mazingira yao yamechangia pakubwa katika uandishi wao wa tamthilia hizi mbili na kuweza kushughulikia ukoloni mamboleo na utandawazi. Katika sura hii tunadhamiria kutoa muhtasari wa tamthilia ya *Sudana* ili kuleta ufahamu wa mada yetu, maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi. Pia tutashughulikia mtindo uliotumika kama mkakati wa kuendeleza utandawazi na ukoloni mamboleo

### 3.1. Muhtasari wa Tamthilia.

Kitabu hiki kinahusu makundi mawili makuu: Wamerope ambao ni Wazungu kutoka Uingereza na Marekani na Wazanji ambao ni Waafrika. Nahodha wa kundi la Wamerope ni Wamerigo (Wamarekani) na naibu wao ni Mzungu .Hawa wanaonekana kuwa na nguvu zaidi ya Waafrika.

Katika tamthilia hii kundi la Waafrika linaongozwa na Sudzungu na ambalo ni kundi la watu wasiojiweza kiuchumi na kiujuzi. Waafrika wanaonekana

wametapakaa kote ulimwenguni kama vile anavyosema Sudana: "Nawalingania nyinyi wanangu, wana -Afrika mliotawanyika kila pembe ulimwenguni..." (uk 1). Wamefanya hivyo ili kujitafutia ruzuku zao. Wanapokutana kule wanaanza kujadiliana juu ya shida zinazozikumba nchi zao. Sudana anasawiriwa kama mwanamke shujaa aliyezinduka na jasiri. Yeye ndiye anayechukuliwa kuwa ndiye mama wa Wazanji Anajitokeza kutetea haki za Waafrika na kupinga utawala wa kikoloni unaowanyanyasa Waafrika kupitia mbinu mpya ya utandawazi.

Matatizo na shida ya chombo chao baharini yanapeleka Sudana pamoja na jamaa yake (Sudzungu, Shume na Sizwe) kujikuta dhidi ya washirika wawili (Amerigo na Mzungu), ambao ni watu wenye matendo, tabia na hatua zao zinazotawaliwa na imani, mielekeo na taasubi kali. Anatatizika baina ya kulinda hadhi yake kwa upande mmoja na kuiuza hadhi hiyo kwa upande mwingine ili kuwanusuru wanawe wasiangamizwe katika madhila na mizigo wanayobebeshwa na Amerigo na washirika wake. Sudana anasema: "mwili wangu ni wa wanangu tu.! Nawe shauku yako kaizimiye kwa mamayo" (uk. 43).

Mhusika Sudana anaingia jukwaani akiwa amevalia kanzu iliyochorwa ramani ya Afrika. Anatoa kilio dhidi ya unyanyasaji na unyonywaji wa bara la Afrika na Wamerigo na Wazungu . Wamerigo na Wazungu wameungana pamoja kupitia mfumo wa utandawazi kulinda maslahi yao huku wakiwanyanyasa mataifa maskini. Mataifa mengi ya Afrika bado yamepata uhuru wa bendera tu! Uhuru Waafrika waliopata haukuwa uhuru wa kiuchumi, kisiasa na hata kijamii. Bado



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

mkoloni, anaendeleza dhuluma zake na mienendo yake hata katika serikali ya Mwafrika. Anatumia mbinu mbalimbali kama vile utandawazi kujidumisha mamlakani. Mkoloni anatumia utandawazi kwa manufaa yake binafsi. Waafrika wanapohitaji msaada wanawekewa masharti ili kupata misaada. Utegemezi huu wa misaada na Bara la Afrika umewafanya kubakia maskini na kushindwa kushindana na mataifa tajiri kupitia utandawazi.

Umaskini unaendelea kuwasakama, hadi kuomba usaidizi kutoka kwa Wamerope. Utegemezi wa misaada na jamii maskini huwa ni tatizo sugu kwa nchi. Jamii zilizo na uwezo wa kiuchumi hutawala na kudhibiti nchi maskini. Mara nyingi mataifa maskini hulazimika kuuza hadhi zao kusudi wapate misaada. Amerigo anasema:

> Msijali, hapa mtapata msaada muutakao mpaka mashua yenu iwe imetengenezeka. Lakini muda huu wa msaada wetu, tutawatarajia kuitumikia AMEROPE kwa kila njia (uk 13).

Sudana anasema ni lazima Mwafrika ajikomboe na afanye juhudi zote za kujiokoa na ana matumaini makubwa, maadam wakati uko upande wao kama tuonavyo mwishoni mwa tamthilia. Sudana anasema: "… katika maisha yetu milele mapambano yaendelee!" Sauti nyingine: "Mapambano yaendelee" (uk 53 hadi 54). Lazima Mwafrika apiganie haki yake na ajinasue kutokana na minyororo ya Wazungu. Ukombozi wa Mwafrika dhidi ya utandawazi utategemea juhudi zake na msimamo wake. Mwafrika hana budi kupambana na utandawazi ili kijikomboa kutokana na athari zake.

### 3.2. Maudhui ya ukoloni mamboleo katika utandawazi.

Bara la Afrika limegawanyika katika matabaka mbalimbali, tabaka la maskini na tabaka la matajiri. Mwanzo wa mgawanyiko huu wa kitabaka una mizizi yake katika historia ya mapambano dhidi ya utawala wa kikoloni. Wakoloni walianzisha mfumo wa kibepari ambao uliruhusu watu binafsi au kundi la watu kumiliki njia za uzalishaji mali na kulazimisha idadi kubwa ya watu iuze nguvu na jasho lao. Badala ya watu kufurahia kazi kama njia ya maisha inakuwa chanzo cha maumivu na mateso.

Kutokana na mfumo huu wa kibepari, inadhihirika wazi kuwa uhuru ulipopatikana ukoloni mamboleo ulianzishwa. Hivyo basi, Waafrika hawakupata uhuru halisi kama anavyosema Sudana:

> Ukombozini,
> 'toka utumwani
> tangu kaskazini hadi kusini
> kote Amerikani.
> Lakini ukombozi ................
> Ukawa ukombozi
> Katika pingu za ugozi ........... (uk. 3).

Waafrika walipopewa uhuru mkoloni aliendelea kuwafuata na kuwatawala kwa kutumia mbinu zingine. Wakoloni walidhibiti mbinu zote za uzalishaji mali na kuwadhulumu Waafrika kiuchumi. Hivyo basi Waafrika wanaisi kuwa uhuru wao haukuwa uhuru kamili bali ulibadilika na kuwa pingu za ugozi kupitia mfumo wa utandawazi.

Utandawazi umekuwa kifungo kingine cha mataifa maskini. Athari za utandawazi dhidi ya mataifa maskini zimekuwa kama minyororo inayowafunga. Hivyo basi kuna haja ya Waafrika kujinasua kutokana na minyororo hii. Miaka mingi baada ya kupata uhuru; siasa, sera na baadhi ya mipango iliyowekwa na serikali za Bara la Afrika katika nyakati tofauti za utawala ziliendelea kuyafunga mataifa haya katika minyororo ya ukoloni wa utandawazi unaohalilisha ukoloni mamboleo. Sudana anasema: 'Lakini ukombozi ukawa ukombozi wa pingu za ugozi. Na kwa mdundo wa asikitiko, wa "bluzi" mkaendelea na kuijenga dunia hii" (uk.3). Mfumo wa utandawazi unalinganishwa na pingu. Utandawazi umechukuliwa kama minyororo ya kuwafunga Waafrika. Utandawazi unakuwa pingu kwani Waafrika hawawezi kushindana nao. Pia hawawezi kujiamlia mambo yao bila mwingilio wa watawala wao. Hivyo ndivyo utandawazi umewafanya Waafrika kwa kutumiwa kama mbinu ya kuwafungamanisha na watawala wao.

Alamin Mazrui na Kimani Njogu wanasema kuwa ukombozi ambao Waafrika walipigania ulibadilika na kuwa pingu ya ugozi. Huu ni utandawazi. Wanaonyesha na kudhihirisha jinsi utandawazi unavyoendelea kuwanyanyasa na kuwanyonya Waafrika. Wazanji wanasema:

> Maharamia waliniiba zamani
> Wakaniuza humu melini
> Mwa ubepari uzunguni
> Waliposhanitoa kwetu Azania. (uk. 8).

Hapa Wazanji ambao ni Waafrika wanawaita Wazungu "Maharamia" yaani watu wanaotumia nguvu na silaha kuwaangamiza wengine waliowanyonge.

Wakoloni wa zama hizi hutumia Waafrika katika ujenzi wa mashua zao.Wanawatumia Waafrika kama wafanyikazi wao kwa malipo duni kwa manufaa ya wakoloni. Mzanji I anasema:

> Nilifikiria zile nguvu na jasho jingi tulilotumia kuijenga mashua hii, nikifikiria damu na roho nyingi zilizotoka kuilinda Mashua hii .......... nikifikiria haya yote, maini yangu hunikatika kwa hasira nyingi nilizovumbika. Huwaza nikiwazua mpaka lini tutaendelea kuijenga na kuilinda mashua hii isiyokuisha kujiunda huku ikituumbua na isiyotupa nafasi ya kufurahia tukiundacho? (uk. 7).

Waafrika walidhani kuwa baada ya kupata uhuru watafurahia matunda ya uhuru. Wakoloni walitafuta njia mpya ya kuendelea kunyanyasa na kunyonya nchi maskini kwa kuleta mfumo mpya wa utandawazi. Huu ni uhusiano ambao haufaidi nchi maskini. Amerigo anasema: "Haya, wamefika karibu; watupieni kamba kamba! Kamba! Kamba!" (uk. 12). Huu ni utandawazi wa kuwafunganisha pamoja Wazungu na Waafrika. Amerigo anaendelea kusema kwa ujanja wake:

> Karibuni! Karibuni katika mashua yetu AMEROPE. AMEROPE imeshawahi kuokoa watu wengi kama nyinyi. Karibuni tena! (uk. 12).

Wamerope wanawakaribisha Waafrika katika mashua yao. Mashua ni chombo kinachotumiwa kusafiria na pia kubebea mizigo. Mashua hapa inaashiria mfumo wa utandawazi unaotumiwa kubebea matakwa ya wakoloni na pia vibovu vyao kwa mataifa maskini. Utandawazi hutumiwa na Wazungu kuingiza bidhaa kutoka nchi zao katika mataifa ya Bara la Afrika kupitia mfumo wa biashara na uchumi. Mataifa maskini hutegemea misaada kutoka kwa nchi matajiri ambazo ndizo zilizodhibiti

mfumo mpya wa utandawazi. Msaada wanaopokea hutolewa masharti mbalimbali kama anavyosema Amerigo:

> Msijali, hapa mtapata msaada muutakao mpaka mashua yenu iwe imetengenezeka. Lakini muda huu wa msaada wetu tutawatarajia kuitumikia Amerope kwa kila njia. Mtajiunga na hawa wazanji wenzenu, ambao tuliwaokoa zamani, kwa kuihudumia mashua hii. Na mashua yenu ikiwa tayari mtaweza kwenda zenu. (uk.13).

Katika mfumo wa utandawazi, Wazungu waliendelea kutumia rasilimali za waafrika katika kujenga na kuendeleza nchi zao huku wakibomoa nchi maskini. Bara la Afrika limerembeshwa kwa rasilimali mbalimbali kama vile madini, watu wenye ujuzi, mito na maziwa ambayo haijatumika ipasavyo. Hivi vitu vyote vingetumiwa kuendeleza mataifa ya Bara la Afrika lakini yamekosa viongozi wenye maono.

Amerigo anasema: 'Muzungu, angalia mashua ile ilivyoumbika au unasemaji? Kitu ilichokosa ni nahodha tu kama mimi .................. (uk. 14).

Anaendelea kusema:

> A – a! That's it! Hebu ngoja kidogo (*Mzungu anasima).*
> Kuna hii mashua ya ZINJI tuliyoifungasha. Ni uzito wa bure tu. Afadhali tutumie baadhi ya vifaa vyake kuitengeneza hii mashua yetu. Mbao na vifaa vingine tulivyonavyo tuviweke akiba. (uk 20).

Wazungu wanabomoa utamaduni na amali wa Mwafrika kupitia mbinu mpya ya utandawazi. Mwafrika alibomolewa kiakili na kitamaduni na kufaywa mtu asiye na chake. Utandawazi umetumika kubomoa Bara la Afrika kimaadili, kiutamaduni, kisiasa ha hata kijamii. Kuna kundi la viongozi wa Kiafrika ambao wanakuwa mstari wa mbele katika kubomoa mashua yao kama anavyosema Sudzungu

Waandishi hawa wa tamthilia hii pia wanaonyesha kuwa Mwafrika anapaswa kujilaumu yeye mwenyewe juu ya maovu na balaa linamkuta. Hii ni kwa sababu ya uongozi mbaya unaokubali chochote kutoka kwa Wazungu. Wao huwakaribisha mabeberu kuchukua rasilimali za nchi zao na kutumia jasho la watu wao. Alamini Mazrui na Kimani Njogu katika *Sudana* wakitumia maneno ya Sudzungu wanaonyesha ujinga wa viongozi wa Kiafrika. Sudzungu anasema:

> Aaah! Mwache huyu Afande! Mashua yetu! Mashua yetu! Mashua yetu tutaifanya nini bila ya ukarimu na msaada wa AMEROPE?
> AMEROPE ikiangamia si nasi tumeangamia?
> Na ZINJI nayo si imeangamia? (uk. 20).

Ujinga wa viongozi wa Bara la Afrika hauko tu katika kukubali kuibiwa rasilimali, bali pia katika kukubali masharti yote wanayowekewa. Mengi ya masharti hayo ni mabaya. Sudzungu anamsihi mamake Sudana akubali kunajisiwa na Amerope ili kupata marupurupu. Anasema: Haya pole mama. Sasa nasema .............

> Yaani kwa nini hukubali tu! Unajua Mwamerope ni Mwamerope! Atakupatia marupurupu mengi na sisi tutaweza kunonea nunduni .............. (uk 22).

Viongozi wa Bara la Afrika wanafaa kulaumiwa. Hawa ndio waliowakaribisha mabeberu kwa kukubali uhusiano na wao bila kujali matokeo ya uhusiano huo. Baadhi ya viongozi walikubali uhusiano huu bila kuupiga msasa na kutumbukiza nchi zao katika lindi la matatizo. Ukweli ni kuwa wakoloni ndio hufaidika katika mfumo huu wa utawala kupitia mbinu ya utandawazi. Alamin Mazrui na Kimani



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Njogu wanawakemea viongozi wanaowakaribisha mabeberu kwa kupokea marupurupu ili kuchukua rasilimali za nchi zao na kwa kutumia jasho la wananchi kwa malipo duni.

### 3.3. Mtindo kama mkakati wa kuendeleza ukoloni mamboleo na utandawazi

Mtindo ni ufundi wa kupanga na kupangua. Ni ufundi wa kujieleza. Kila mtunzi au mwandishi huwa na njia yake ya kujieleza na inayomtofautisha na mwandishi mwingine. Vipengele vya mtindo ni pamoja na jazanda, taashira, tashbihi, tafsida, taswira, taharuki, mbinu rejeshi na viangaza mbele miongoni mwa vingine (Kimani Njogu na Chimerah R, 1999). Ufafanuzi huu unaeleza mtindo kama fani.

Mbatiah (2001) anasema kuwa mtindo ni jinsi mtunzi wa kazi ya kisanaa anavyotumia lugha kujieleza, kama vile uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, miundo ya sentensi, aya na beti. Kwa ujumla anasema mtindo hujumlisha vipengele vyote vya lugha. Tathmini ya maelezo haya inaonyesha kwamba hatofautishi fani na mtindo. Wamitila (2003: 145) anasema kuwa mtindo ni jinsi mwandishi fulani anavyojieleza katika kazi yake. Uchunguzi wa mtindo unahusisha uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, mbinu za kibalagha, miundo ya sentensi, sura na upana wa aya zake na uakifishi. Kila mwandishi ana mtindo wake wa kipekee.

King'ei na Kemoli (2001) wanasema kuwa mtindo unaweza kurejelea fani, matumizi ya lugha ya kishairi, mpangilio wa maneno, matumizi ya methali, kiswahili cha kikale, matumizi ya msamiati uliotoholewa, matumizi ya maneno ya kilahaja na

kuchanganya ndimi. Kwa ujumla, mtindo ni njia ya kipekee ambayo mwandishi mmoja anajitofautisha na mwingine kwa jinsi anavyotumia lugha kujieleza. Katika utafiti wetu, tumechunguza mtindo kama muundo na fani zilizotumika katika utunzi wa tamthilia ya *Sudana*. Alamini Mazrui na Kimani Njogu wametumia mbinu zifuatazo ili kuwasilisha ujumbe wao.

### 3.3.1. Mpangilio wa Tamthilia ya *Sudana*

Tamthilia hii imepangwa kwa kutumia matendo. Matendo hapa yanatumika kuonyesha tabia na mienendo ya wakoloni kupitia mfumo wa utandawazi. Tamthilia imepangwa katika tendo la kwanza ambalo lina onyesho la 1 na 2. Tendo la Pili lina onyesho 1 na 2 na mwisho kuna Tendo la Tatu ambalo lina onyesho la 1 na 2. Kwa ujumla tamthilia ina matendo matatu na maonyesho sita. Haya ni matendo yanayoashiria matukio mbalimbali ya kihistoria. Tendo la kwanza linaashiria majalio ya wakoloni. Tendo hili linaonyesha maovu waliyofanyiwa Waafrika kama wanavyosema Wazanji:

> Maharamia waliniiba zamani
> Wakaniuza humu melini
> Mwa bepari Uzunguni
> Waliposhanitoa kwetu
> Azania (uk 8).

Hili linaonyesha jinsi Waafrika walivyochukuliwa kuwa watumwa katika nchi za Amerika.

Tendo la Pili linaashiria wakati wa ukoloni mamboleo na utandawazi. Amerigo anamsihi Sudana wafanye mapenzi lakini Sudana anakataa kata kata. Amerigo anajisifu mbele ya Sudana kwa kumwita kipenzi chake na kuwa anajulikana kama nahodha mwenye huruma. Mapenzi ni kishawishi kinachowafanya watu kuwa na uhusiano katika jamii. Mapenzi huwa kama ishara ya maingiliano katika jamii. Ni mbinu inayotumiwa na watu kuingia katika ndoa. Wakoloni walitumia vishawishi vingi kuweza kuingiliana na Waafrika. Mara nyingi walitumia misaada kama njia ya maingiliano na viongozi wa Kiafrika. Pia kuna wale ambao walitumia silaha kuwakinga mataifa dhidi ya kuingiliwa na mataifa mengine. Vitu hivi vilitumika kama ishara ya mapenzi na wakoloni dhidi ya Waafrika .Wakoloni pia walitumia mfumo wa dini ili kushirikiana na Waafrika. Walijengewa kanisa, walipewa masomo kama vishawishi vya kuingia katika uhusiano. Hata hivyo uhusiano huu ulijawa na dhuluma nyingi maana yalikuwa mapenzi ya pande moja. Hii ni mbinu wanaotumia mataifa tajiri kuwahadaa nchi maskini kuingia katika mfumo wa utandawazi. Amerigo anasema:

> La! La! La! kipenzi changu.
> Kote duniani mimi najulikana kama nahodha mwenye huruma kabisa.
> Najali maslahi ya watu wote bila kubagua ---- (uk 35).

Hata hivyo Sudana anapinga wazo lake kwa kumwita katili, zimwi mla watu. Sudana anasema:

> Katili wee! Zimwi Mla Watu! Tangu maisha yetu ya kumbane na yako umetudhulumu na kututendea unyama. Haini wee! Utakoma lini? (uk 35).

Sudana anawaita Wamerigo mahaini kwa kuzua mbinu za kuendeleza dhuluma dhidi ya Bara la Afrika kwa kutumia mbinu mpya ya utandawazi.

Tendo la Tatu linaashiria juhudi za Waafrika kujinasua kutokana na unajisi waliopata kwa athari za utandawazi. Shume anasema hivi:

> Kwa hivyo kwanza lazima tumtoharishe mamaetu, tumtakase na najisi iliyompata. Bila ya hivyo, idadi ya ndugu walionajisika itaongezeka kati yetu, ndugu ambao, kwa athari ya najisi hiyo, huendelea kutusaliti kwa njia -------- (uk 45).

Shume anaonyesha kuwa utandawazi ulitumika kuwanajisi Waafrika. Hiki ni kitendo cha kuonyesha athari hasi za utandawazi kwa Waafrika. Mila, desturi na tamaduni za Kiafrika zilichafuliwa na tamaduni za kigeni kupitia utandawazi. Hii ndio maana Shume anasema kuwa kuna haja ya kutakasa mama yao kutokana na unajisi uliompata. Mama yao hapa ametumika kijazanda kuashiria mataifa ya Kiafrika.

Pia mazingira ya Bara la Afrika yanachafuliwa kwa kurudikwa bidhaa mbovu mbovu kutoka nchi za Kimagharibi. Waafrika huuziwa magari kuu kuu na ambayo yanachafua hewa kwa kutoa moshi mwingi. Pia Waafrika huuziwa vinywaji mbalimbali kama vile pombe ambazo hapo mbeleni hazikupatikana katika mataifa ya Kiafrika kama vile pombe na bia kali. Hivi vyote ni vitu vitu vya kutia unajisi Waafrika. Waafrika wanaashiria kupambana na athari za utandawazi. Uhusiano wa mataifa ya "Dunia ya Tatu" na mataifa ya Magharibi unawanajisi kwa kuwaharibia mila na desturi zao. Utamaduni wao na uchumi wao unaharibiwa na mbinu hii mpya ya utandawazi.

### 3.3.2. Usimulizi.

Mbali na kutumia mpangilio mahsusi, Alamin Mazrui na Kimani Njogu wametumia mbinu ya usimulizi katika kuwasilisha maudhui na dhamira zao. Kuna masimulizi ya Sudana yanayojitokeza katika utangulizi (uk.1 – 6). Haya ni masimulizi yanayosimulia historia ya Afrika, wakati wa ukoloni na baada ya uhuru kupatikana. Pia Amerigo anamsimulia Muzungu hadithi inayoonyesha asili ya ngoma ya Wazanji. Amerigo anasema

> "Hapana! Hapana! Hapana!
> Hayo si mambo ya juzi na jana tu, ni mambo ya maumbile. (Kimya kidogo).Ndivyo, yalianza muda tu baada ya kuumbwa. Si unakumbuka tulivyokuwa tukisomeshwa, katika madarasa ya dini? Mungu, baada ya kuumba binadamu, alichukua ngoma yake kuu, akawa anaipiga kuwaita watu wa makabila mbali mbali. Bila ya shaka kabila lililoitwa mwanzo ni lile la Wamerope: Watu kama mimi na wewe. Bwana Mungu akawauliza,"Mnataka nini wanangu? ................. (uk 17 hadi 19).

Masimulizi hapa yanaashiria mitazamo yaliyonayo mataifa ya Kimagharibi dhidi ya Waafrika. Inaonyesha chanzo cha utengano wa kiakili walionayo Wazungu na Waafrika. Inasemekana kuwa Wazungu walipewa akili lakini Waafrika walipewa ujinga na ngoma. Ni kutokana na ujinga wa Waafrika ndio wanakubali vibovu vyote kutokana na nchi za kigeni. Wanatawaliwa kimawazo kupitia utandawazi na kukubali rasilimali zao kuchukuliwa na wakoloni. Utandawazi ni dhana ya ushindani. Kama anavyosema Amerigo, Wazungu waliweza kuwashinda Waafrika kwa kunyakua kilicho chema na kuwaachia ngoma. Hii inaashiria kuwa Waafrika hawawezi kunufaika na mfumo wa utandawazi. Waafrika hawana ujuzi mwingi na

Wazungu ndio wanaodhibiti mfumo huu wa utandawazi. Huu ni ukoloni mamboleo katika utandawazi.

Tangu zamani biashara imekuwa ikiendeleza dhuluma. Ndani ya biashara kumefichika uozo na udhalimu unaoongozwa na ubinafsi. Tamaa ya pesa na nguvu za kiuchumi husababisha kuporomoshwa kwa mataifa maskini na mataifa tajiri. Ni vigumu mataifa maskini kuweza kushindana na mataifa ya Kimagharibi ambayo ndiyo hudhibiti nyanja zote za uzalishaji mali na pia mifumo ya kiuchumi kupitia taasisi zao kama vile Benki Ya Dunia, Shirika La Fedha la Kimataifa na hata Shirika la Biashara. Hivi ni vyombo vinavyotumiwa kuendeleza dhuluma dhidi ya mataifa maskini kwa kuendeleza uliberali mpya. Mataifa ya Kimagharibi hutumia mbinu kama hizi kwa kuwawekea Waafrika masharti ya kibiashara ambayo huwaondoa katika kushiriki ipasavyo katika mfumo huu mpya wa utandawazi. Msimulizi ni mbinu ya kikale iliyotumika na Waafrika kueleza na kuendeleza fasihi yao. Wakoloni wanatumia mbinu hii ya usimulisi kama njia kuu ya kujitambulisha na Waafrika. Huu ni ujaja waWakoloni kuendelea kudhibiti nyenzo kuu za utanaduni wa Mwafrika.

### 3.3.3. Matumizi ya Nyimbo na Ushairi.

Kuna matumizi ya nyimbo katika tamthilia ya *Sudana*. Kuna nyimbo zilizoimbwa na Wazanji ili kuonyesha hisia zao dhidi ya watawala wao. Kwa mfano kuna wimbo huu: Wazanji (*wakiimba):*

Maharamia waliniiba zamani
Wakaniuza humu melini
Mwa bepari uzunguni
Waliposhanitoa kwetu
Azania ...............
Lakini mkono wa Mungu
Ukapenya kifua changu
Kuujaza moyo wangu
Na nguvu za miamba na majabali ........................ (uk 8 hadi 9).

Kuna ushairi unaokaririwa na Shume.

"Silie mama, silie
Kilio unacholia
Ni kilio cha unyonge ............ ( uk 39).

Utandawazi hapa umepewa jina la maharamia. Utandawazi ni nguvu ambayo hutumiwa na nchi za Kimagharibi kuibia nchi maskini. Utandawazi huwaingiza Waafrika katika ubepari ambao ni aina ya uchumi wenye sifa za ubidhaaishaji wa rasilimali, nguvu – kazi na maarifa na ambao ni mfumo wa unyanyasaji. Hii ndio maana wazanji wanasema kuwa waliuzwa kule melini mwa bepari wa uzunguni. Utandawazi umekuwa mfumo wa kuwaingiza Waafrika katika ubepari na ubeberu. Katika mfumo huu wa utandawazi Waafrika wanaisi kuwa wameibiwa kila kitu kama vile rasilimali zao, utamaduni wao na hata vyakula vyao asilia. Nyimbo zimetumika kuelezea mitazamo na hisia za Waafrika dhidi ya wakoloni wanaowanyanyasa kupitia mfumo wa utandawazi.

Pia katika ukurasa wa 48 hadi 49, kuna ushairi unaokaririwa na msichana na mwanamke ni kama ngonjera. Mbinu ya nyimbo na ushairi ni mtindo ambao hupatikana katika tamthilia nyingi kama anavyosema Wamitila (2002). Mbinu ya nyimbo imetumiwa sawa na A. Mazrui na Kimani Njogu ili kuendeleza kazi yao.

Matumizi ya nyimbo katika tamthilia hii yanaonyesha hisia za Waafrika dhidi ya Wazungu. Waafrika wanawaona Wazungu kama maharamia. Hawa ni watu wanaowadhulumu Waafrika na kuchukua vitu vyao kupitia nguvu ya utandawazi. Mwanamke anapokariri shairi anasema kuwa hana budi kujitakasa kutokana na unajisi wa wakoloni.

Mfumo wa utandawazi umepewa sifa za unajisi. Hii ina maana ya kuchafua au kuharibu kitu kilichokuwa kizuri. Unajisi wa kikoloni unaashiria kuchafuliwa kwa utamaduni wa Mwafrika kupitia tamaduni za kigeni. Utandawazi umefungua milango ya biashara, masoko huria ya bidhaa na kuufanya utamaduni wa kigeni kukutana na utamaduni wa Kiafrika. Mwingiliano huu wa utamaduni umezua utamaduni mseto na pia kuwafanya Waafrika hasa vijana kuiga tamaduni zinazokinzana na tamaduni za Kiafrika. Kupitia vyombo vya habari na mawasiliano, Waafrika wamepokezwa tamaduni na itikadi zilizo kinyume na amali zao. Huu ndio unajisi wa kikoloni unaopokezwa Waafrika kupitia mfumo wa utandawazi. Waafrika basi hawana budi kujitakasa kutokana na unajisi huu.

Nyimbo na mashairi basi zimetumiwa kuonyesha juhudi za Waafrika za kupambana na mfumo mpya wa utandawazi. Utandawazi umetumika kuwaibia Waafrika imani zao, itikadi na utamaduni wao. Waandishi hawa wametumia mbinu hii ili kuendeleza maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi.

### 3.3.4. Kuchanganya ndimi

Watunzi wa tamthilia ya *Sudana* wametumia mtindo wa kuchanganya ndimi. Kwa kutumia wahusika Amerigo na Mzungu wametumia lugha ya Kiingereza ili kudhihirisha taasubi yao dhidi ya Waafrika. Lugha ya Kiingereza ndiyo iliyotumiwa na watawala kuendeleza utawala wao dhidi ya Waafrika. Lugha ya Kiingereza ndiyo iliyosambaa na kutumiwa na mataifa mengi ya Kigeni. Hii ni lugha inayotumika katika utandawazi. Lugha ya Kiingereza hutumiwa kiutandawazi kuendeleza matakwa na malengo ya kikoloni na ukoloni mamboleo katika utandawazi.

Matumizi lugha ya Kiingereza yanaashiria hadhi yake kuliko lugha za Kiafrika. Hii ndiyo sababu kuwa lugha ya Kiingereza huchukuliwa na kutumiwa katika mfumo wa utandawazi hasa katika tarakilishi. Aidha kuchanganya ndimi kunatumika kama ishara ya kuingiliana na ndio maana kuna wageni waliojaribu kutumia Kiswahili kama lugha ya kuwasiliana na Waafrika kama vile Wajerumani nchini Tanzania. Hawa ni washirika wawili wa utandawazi na wametumiwa kuonyesha mitazamo na mielekeo hasi ya wakoloni dhidi ya watu weusi. Kwa mfano, Amerigo anasema: " .................... hatua hufahamu kamwe

> Nasema nini! Wake up, Man! " (uk 15).

Amerigo anamwambia Mzungu azinduke na kuona angependa waungane pamoja ili waweze kuwadhibiti Waafrika. Mzungu akiwaamrisha Wazanji kwa ukali anasema:

> "Silence! Nyamazeni!
> .................. Hamuwezi kuzuia hizo tarumbeta zenu ......... You foolish baboons! (uk 16).

Hii ni lugha ya matusi. Mzungu anaonyesha jinsi anavyowadharau watu weusi kwa kuwadunisha na kuwaita wanjinga kama tumbili. Mzungu anaendelea kusema: "….. They are just like children" (uk 16). Hii inamaanisha kuwa Waafrika kama watoto ni watu ambao hawajaendelea na hawana akili au ujuzi bora kama Wazungu. Amerigo anaendelea kutumia lugha ya kiingereza kama vile

> "Oh No!........ Know thy people. …………………
> "……….. To them Music is life my dear man! (uk 17).

Hapa Amerigo anadhihirisha kwamba wao ni watu wanaodharahau Waafrika. Anasema kuwa Waafrika hawana lingine isipokuwa ngoma tu. Kuna maneno mengine yaliyotumika kama vile: "IQ", "You know", "imbeciles" (u.k. 18). Lugha ya Kiingereza inatumiwa na Amerigo na Mzungu ili kuonyesha kuwa wao ni tofauti na Wazanji. Lugha ya Kingereza imetumika kama chombo cha ukandamizaji. Ikumbukwe kwamba ni kupitia lugha ambako amali na utamaduni wa jamii hudhihirika. Lugha ya Kiingereza ndiyo inayotumika katika mfumo wa utandawazi. Kwa kutumia lugha ya Kiingereza, Alamin Mazrui na Kimani Njogu wameonyesha wazi vile lugha hii hutumiwa na mataifa ya kigeni kunyamazisha mataifa ya "Dunia ya Tatu". Ulazimishaji wa lugha ya Kiingereza kama njia ya mawasiliano ni ukandamizaji na unyanyazaji kwa Mwafrika unaoendelezwa kupitia kwa utandawazi. Pia kwa kutumia lugha isiyoeleweka kwa Waafrika ni kama mbinu ya kuwanyamasisha. Huu ni ukoloni mamboleo katika utandawazi. Lugha za Kiafrika hukoseshwa nafasi katika mfumo wa utandawazi. Lugha za Kiafrika huchukuliwa

kama lugha duni na ambazo pia hazina utaratibu wa kisarufi unaokubalika. Lakini pia hali ya kuchanganya ndimi inaashiria athari za kiutandawazi.

### 3.3.5. Tamathali za usemi

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004), tamathali ya usemi ni usemi wa kufananisha dhana moja na nyingine tafauti au zinazofanana. Mbatiah (2001: 77) anaelezea tamathali ya usemi kama ukiushi wa kimaksudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana na mpangilio wa maneno ili kuleta maana mpya au msisitizo. Naye Senkoro (1982: 13), anasema kuwa tamathali za usemi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandishi ama kusema. Hizi wakati mwingine hutumiwa kama njia ya kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha. Tamathali za usemi zilizotumiwa katika tamthilia ya *Sudana* zinaonyesha jishi Waafrika wameangamizwa na mfumo wa utandawazi. Matumisi ya tashbihi, jazanda, nahau na zinginezo ni mbinu za ujanja wa wakoloni ambao wanapenda kudhibiti Bara la Afrika. Kufananisha Bara la Afrika na mwanamke anayevutia wengi ni ishara ya ujanja wa Wazungu kutamani rasilimali za Afrika kwa ajili ya manufaa yao wenyewe. Tamathali za usemi zifuatazo zimetumiwa katika tamthilia ya *Sudana:*

**Tashbihi**

Tashbihi ifuatayo imejitokeza katika tamthilia ya *Sudana:*

........... "zikijitatua kama nyoka nyusoni mwenu" (uk 17).

Ina maana kuwa mipango ya siri waliyonayo Waafrika kupambana na maadui wa nchi zao inafananishwa na nyoka aliyetayari kuuma. Maneno haya yalitolewa na Sudana katika kitangulizi akiwanenea Waafrika waliotawanyika kila pembe ulimwenguni. Tashbihi hii inaashiria kuwa Waafrika wanajipanga kupigana na nguvu za utandawazi ambazo ndicho kiini na chanzo cha matatizo mengi katika mataifa yao._Inatumika kuonyesha hisia walizo nazo Waafrika wanaoteswa na wakoloni. Sudana analinganisha siri na mipango waliyonayo wana wa Afrika za kujinasua na nyoka aliyetayari kuuma._ "..........ilivyosimima wima kama matiti ya bikira" (uk.11). Matiti ya bikira hapa yanaashiria migodi na madini yaliyomo Barani Afrika ambayo haijachimbuliwa. Pia yanaashiria misitu ambayo haijatumiwa ipasavyo, mafuta ambayo hayajagunduliwa na nchi yenye rutuba nyingi ambayo haijatumika. Amerigo anaashiria kuwa Bara la Afrika lina rasilimali nyingi ambazo hazijatumiwa na ambazo wanaweza kuzitumia. Rasilimali hizi ndizo zinazowavutia Wazungu kupenda kufanya biashara na mataifa ya Kiafrika kwa manufaa yao wenyewe. Uhusiano wa kibiashara umekuwa wa kuendeleza dhuluma na ukandimizaji._ Hapa Amerigo anaelezea uzuri wa Bara la Afrika. Analinganisha milima yake na matiti ya bikira ambaye hajanyonyesha mtoto yeyote. Milima hii inavutia watu wengi. Mfano mwingine wa tashbihi ni kama:

……… "They are just like children" (Hawa ni kama watoto) (uk 16). Neno watoto limetumika kuashiria hali ya kutoweza kujikinga na mifumo ya kiulimwengu. Mtoto hutumiwa kuashiria ndugu wa daraja ya pili, yaani, ni zao la kitu kingine. Watu ambao ni watoto hawana budi kutawaliwa na kuelekezwa. Kiutandawazi, mataifa ya Kiafrika huchukuliwa kama watoto na ndio wanaotawaliwa na Wazungu ambao ndio wenye uwezo wa kudhibiti mfumo wa utandawazi. Hapa Mzungu anawalinganisha Wazanji ambao ni watu wengi na watoto. Mtoto ni mtu ambaye haelewi chochote na hana ujuzi wowote. Kwao Mwafrika ni mtu ambaye hana akili kamili na hawatumii akili.

**Takriri.**

Takriri ni tamathali ya usemi ya kusisitiza. Hii ni hali ya kurudia herufi fulani, neno au maneno katika usemi. Wamitila (2003:215) anasema kuwa kuna takriri ya irabu au vokali, takriri ya neno au maneno na takriri ya konsonanti. Tamthilia hii ya *Sudana* imetumia mbinu ya urudiaji ili kusisitiza ujumbe. Kwa mfano:

Lakini ukombozi ……………..
Ukawa ukombozi ……………..
Katika pingu ya ugozi ……….. (uk 3).

Neno ukombozi limerudiwarudiwa kusisitiza kuwa Waafrika wana hamu kubwa ya uhuru wao kutokana na minyororo ya wakoloni. Wanasisitiza kuwa ukombozi kwao umebadilika na kuwa pingu ya ugozi katika mfumo mpya wa utawala wa

utandawazi. Hapa Sudana anaonyesha kuwa ukombozi uliopiganiwa na Waafrika ulibadilika na kuwa si ukombozi kamwe bali ni kifungo kingine.

> Huko Amerika
> Huko Afrika
> Huko Uingereza, Ufaransa na Ujerumani
> Huko Ubeligiji, Ugiriji na hata Utaliani
> Mlisimama wima kukabili hatari ............... (uk 4).

Neno huko limerudiwarudiwa kusisitiza kuwa popote Waafrika walipo, Amerika, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Ubeligiji, Uginji na Utaliani walikuwa tayari kupigana na nguvu za ubeberu na ubepari katika mfumo wa utandawazi. Msisitizo huu pia unaashiria kuwa Waafrika wametapakaa kila mahali katika mfumo huu wa utandawazi. Kifungu hiki kinaonyesha jinsi Waafrika walipigania uhuru wao bila kujali mahali walipokuwa. Waliungana kwa pamoja na kupinga ubeberu.

> Haya! Haya! Haya!
> Fanyeni haraka!
> Tanga! Tieni Tanga!
> Nanga! Tieni nanga!
> Kamba! Rusheni Kamba!
> Haya! Haya! Haya! (uk 11).

Maneno: haya; tieni tanga, tieni nanga yamerudiwarudiwa. Haya ni maneno yaliyonenwa na Amerigo kwa Mzungu. Anamwonyesha mashua ya Wazanji iliyokuwa imevunjikavunjika. Maneno hayo yanaashiria haraka waliyokuwa nayo kuwapa msaada Wazanji. Hii inaonyesha utegemezi wa msaada na mataifa ya Kiafrika. Waafrika hawawezi kushiriki ipasavyo katika mfumo wa utandawazi pasipokuwa na misaada. Hali hii ya kiuchumi ya utegemezi wa misaada hufanya nchi za Kiafrika kubakia maskini kwa kuwa hawana uwezo wa kiuchumi na pia misaada hutolewa kwa masharti.

Amerigo anasisitiza kuwa kuna haja ya kuharakisha ili kuwasaidia wazanji kwa kuwatupia kamba ili wafunganishwe na wao.

> Hawawezi kazi bila ya ngoma
> Hawawezi kula bila ya ngoma
> Hawawezi kufa bila ya ngoma
> Hata kwenda bila ya ngoma (uk 17).

Katika kifungu hiki, Amerigo anaonyesha jinsi Waafrika ambao wanafikiriwa kuwa ngoma kwao ndio kazi muhimu na hawajui chochote bila ngoma. Haya ni madharau wayofanyiwa Waafrika katika mfumo wa utandawazi. Huu ni ukoloni mamboleo katika utandawazi.

> Nahodha ni kama mimi: The Captain!
> .................... ...........................
> Nahodha ni kama mimi: The Captain!
> ........................... ....................
> Nahodha ni kama mimi: The Captain! (uk 25).

Amerigo anaonyesha maringo yake na kusema kuwa hakuna kiongozi mwingine kama yeye. Hii ni mbinu inayotumiwa na waadishi kuonyesha na kusisistiza ukoloni mamboleo katika utandawazi.

**Nahau**

Nahau ni vifungu vya maneno vilivyo na maana iliyofichika. Maana hii haitokani na maneno yanayopatikana katika nahau. Inabidi msomaji wa kazi hiyo kutafakari maana anayokusudia msanii katika nahau iliyotumika. Nahau ni misemo ambayo huwa na maana iliyofichika.

Wamitila (2003: 163), nahau huwa na maana ya ndani kuliko baadhi ya misemo inayopatikana katika lugha fulani. Tumebainisha nahau zifuatazo katika *Sudana* miongoni mwa nyingine: 'Huko Ubeligiji, Ugirigi na hata Utaliani mlisimama wima kukabili hatari kufa na kupona kumtetea ndugu yenu' ( uk 4). Hii inamaanisha kuwa Waafrika walijitoa kupigania uhuru/ ukombozi wao.

'Huwaza nikiwazua, mpaka lini tutaendelea kuijenga nakuilinda mashua isiyokuisha kujiunda huku ikituumbua, na isiyotupa nafasi ya kufurahia tukiundacho?'(uk 7). Hii inaonyesha vile Waafrika walikuwa na mipango isiyokamilika hasa kwa vile walikuwa wanapanga kupigania ukombozi wao. 'Wenzetu wengi wengine wamefariki dunia mashua yetu ilipokumbana na dhoruba' (uk 14). Yaani kumetokea vifo vingi kutokana na dhoruba na shida wanazokumbana nazo Waafrika. Hii ni kwa kuwa Waafrika hawana ujuzi wakukabiliana na majanga.

'Atakupatia marupurupu mengi na sisi wanao tutaweza kunonea nunduni' (uk 22). Hii inaonyesha kuwa Wamerigo wangewapa marupurupu ambayo wakiyapata wataweza kujizibisha na kunenepa vilivyo. Hii inaonyesha tamaa waliyokuwa nayo viongozi wa wazanji. Sudana anamwambia Shume: 'Kilio unacholia si kilio cha kishume au umekata tamaa Shume?' (uk 29). Hii inamaanisha kuwa ni kama Shume alikuwa amepoteza moyo wa kupigania ukombozi wao. Pia inaashiria kuwa Shume amepoteza matumaini ya kupambana na nguvu za utandawazi.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**Matumizi ya jazanda**

Kwa mujibu wa Kimani Njogu na Rocha Chimerah, (1999: 32), jazanda ni mafumbo ambamo ndanimwe maana ya kitu imefichana. Ni sawa na Isitiari. Ni uhamishaji wa sifa za A kwenda kwa B. Katika kujadili kuhusu jazanda, tunazingatia mfanano na uhusiano mkubwa na utamaduni na muktadha wa matumizi. Katika tamthilia ya *Sudana,* jazanda zifuatazo zimetumika: Kwanza, kuna jazanda ya mashua ya inayoongozwa na nahodha mbalimbali. Kuna mashua ya Wamerope inayowakilisha Bara la Amerika na Uropa. Nahodha wao ni Amerope akisaidiwa na Mzungu. Nahodha hapa inaashiria viongozi waliochaguliwa kuongoza mataifa haya ya Ulaya. Pia kuna mashua ya Waafrika ambayo nahodha wao ni Sudzungu. Mashua hii inaashiria Bara la Afrika ambalo limekumbwa na tatizo la uongozi. Viongozi wa Bara la Afrika wanaposhindwa kuongoza mataifa yao hukimbilia mataifa ya nje kwa misaada. Kama anavyosema Amerigo "Mzungu, angalia mashua ile ilivyoumbika au unasemaje? Kitu ilichokosa ni nahodha tu". (uk 14). Hii inadhihirisha uzuri wa Bara la Afrika.

Pia kuna jazanda ya dhoruba inayoashiria shida na maafa ya Bara la Afrika. Maafa haya yanaweza kuwa ni kama vile magonjwa yasiyo na tiba, Malaria miongoni mwa mengine. Shida hizi zimesababisha vifo vya wengi kama anavyosema Sudzungu "……… Wenzetu wengine wamefariki dunia mashua yetu ilipokumbana na dhoruba" (uk. 14). Aidha kuna jazanda ya mwanamke. Mwanamke hapa pia ametumiwa kijazanda kuleta maana ya taifa au Bara la Afrika. Bara la Afrika

limebarikiwa na rasilimali nyingi ambazo zinawavutia Wazungu kama vile madini, wafanyakazi walio na ujuzi mwingi miongoni mwa nyingine. Amerigo anapendezwa na Sudana na kutaka kumnajisi. Huyu mwanamke ana uwezo wa kulea watoto wake kama anavyosema Sudana

> ........... Ni marupurupu gani hayo unayoweza kuyapata kwa Wamerope ambayo umeyakosa kwangu?
> Nimekuruzuku mpaka umekuwa shababi kwa haya maziwa yangu ............
> Kutokana na mwili wangu huu mwili wako umejengeka
> ................................................
> Nimekuwa mkate na mvinyo wa mwili na roho yako. ................. (uk 23).

Bara la Afrika lina uwezo wa kujitunza na kujisimamia bila misaada na marupurupu ya Wazungu. Sudana anapinga kunajisiwa na Amerope kuonyesha juhudi za Waafrika kujikomboa na kujitenga na nguvu za ukoloni zinazowafuata kupitia mbinu mpya ya utandawazi. Mitindo mingine iliyotumiwa katika tamthilia ya Sudana ni matumizi ya ngoma, matumizi ya vicheko na matumizi ya Sauti.

### 3.4. Kiishilio.

Katika sura hii ya tatu, tumetoa muhtasari wa tamthilia ya *Sudana.* Aidha tumechunguza maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi na mtindo uliotumika kama mkakati wa kuendeleza utandawazi na ukoloni mamboleo. Katika sura ya nne tutatoa muhtasari wa tamthilia ya *Posa za Bikisiwa*. Pia tutachunguza maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi. Tutashughulikia mtindo uliotumika kama mkakati wa kuendeleza ukoloni mamboleo na utandawazi.

# SURA YA NNE

## 4.0. Utangulizi

Katika sura ya tatu tumetoa muhtasari wa tamthilia ya *Sudana.* Aidha tumechunguza maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi na mtindo uliotumika kama mkakati wa kuendeleza ukoloni mamboleo na utandawazi. Katika sura hii tunadhamiria kutoa muhtasari wa tamthilia ya *Posa za Bikisiwa.* Tutashughulikia maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi. Aidha tutashughulikia suala la mtindo kama mkakati wa kuendeleza ukoloni mamboleo na utandawazi.

## 4.1 Vipindi vya kihistoria katika tamthilia.

Tamhilia hii imegawanywa katika vipindi tofauti tofauti badala ya maonyesho kama ilivyo katika tamthilia nyingine. Vipindi hivi vimetumika kuashiria vipindi tofauti vya kihistoria. Bara la Afrika limepitia katika vipindi tofauti vya kihistoria hadi sasa. Mandhari ya kitabu hiki ni ya Ki-Afrika Mashariki. Vipindi vinavyoashiriwa ni kama vifuatavyo: kipindi cha utumwa cha karne ya 14, kipindi cha ukoloni mkongwe cha karne ya 19, kipindi cha ukoloni Mamboleo cha karne ya 20 na kipindi cha utandawazi cha karne ya 21.

### 4.1.1 Kipindi cha utumwa (karne ya 14).

Hiki ni kipindi ambacho hakijatajwa kwa uwazi. Katika kipindi hiki, nchi za Kimagharibi ziliwachukua watu kutoka Bara la Afrika na kuwafanya watumwa

katika nchi zao. Waafrika waliochukuliwa kama watumwa waliweza kubaguliwa kwa misingi ya rangi. Mwanamke anasema: "Toka zamani walikuja watu kama mnavyokuja nyinyi sasa...." (uk. 3). Mwanamke anaashiria mbinu walizotumia Wazungu kuwahadaa Waafrika. Walitumia ndimi na utemi kuingia katika mahusiano na Waafrika. Matokeo ya uhusiano huo ni utumwa wa Waafrika. Waafrika walichukuliwa na kusafirishia hadi nchi zao na kufanyishwa kazi kubwa. Walichukuliwa na kufanyishwa kazi katika mashamba ya Wazungu kule Amerika. Katika uhusiano huu, Waafrika walidunishwa, walidharauliwa na kubaguliwa kwa misingi ya rangi.

Pia, Bikisiwa katika ukurasa 16 hadi 17 anatuambia kuwa tayari amemaliza kusoma kitabu cha *East Africa Through a Thousand Years* cha Gideon Were. Hiki ni kitabu kinachozungumzia utumwa na jinsi ulivyoendelezwa. Hiki kitabu kinaelezea jinsi Waafrika walivyochukuliwa na kuuzwa kama watumwa.

### 4.1.2 Kipindi cha ukoloni mkongwe (karne ya 19)

Katika kipindi hiki, nchi za ulaya ziligawa Bara la Afrika na kuwa nchi mbalimbali kama himaya zao. Kipindi hiki kimeonyeshwa kupitia waposaji mbalimbali waliokuja kumposa Bikisiwa. Mposaji wa kwanza ni Hassan Bin Ali na watu wake ukurasa 29 hadi 33. Hawa wanaomba hifadhi kwani wao ni wakimbizi. Hassan anamwambia Bikisiwa kuwa yeye ni mkimbizi anayetoroka mapigano ya wenyewe kwa wenyewe. Amekimbilia Afrika ndio apate mahali pa kuhifadhiwa.

Tunaambiwa kuwa Bikisiwa alihofia huenda wakawa ni majasusi. Hassan Bin Ali anawakilisha Waarabu waliotaka kufanya biashara Afrika Mashariki. Hatimaye, Hassan alitaka kumposa Bikisiwa. Anamwambia Bikisiwa kuwa yeye ameleta watu ambao ni wazuri tena wenye ujuzi mwingi na watasaidia na kuiendeleza mbele nchi yao kama watukubali kumpokea (uk 30). Katika hali ya kumshawishi alimpa zawadi ya kitabu kiitwacho "Fasili ya Watu Washenzi" Wazenji kwa maana ya Washenzi. Hawa ni watu wanaochukuliwa kuwa wapumbavu. Kitabu hiki kinaashiria taasubi hasi waliyonayo Wazungu dhidi ya Waafrika. Waafrika huchukuliwa kuwa ni washenzi.

Hiki ni kitabu kinachoelezea juu ya watu wa Bara la Afrika. Tunaambiwa kuwa Afrika Mashariki ilikuwa sehemu iliyokuwa na ukwasi, urembo na sifa zake hazina mfano. Hassan anasema "Kama utakavyosoma kwenye kitabu hicho nilichokutunikia, enzi yangu imetalii eneo lote hili la Pwani. Ukwasi , urembo na sifa zako hazina mfano. Upekee miongoni mwa wanawake wote, ndio maana nikaamua kukimbilia huku" (uk 31). Hapa tunaona kuwa uzuri wa Afrika Mashariki ndio uliowatoa Waarabu kuja huku na kuanzisha biashara zao sehemu ya pwani. Hassan anamwambia Bikisiwa:

> ..........Urembo na mapambo yako. Fuo zake za mwili. Konde za ujanajike wako ............... kwa hayo yote, na zaidi ya hayo ningetaka tuunganike kwenye ndoa ......... (uk 32).

Hassan alimpa Bikisiwa zawadi nyingi kama vile magauni ya hariri, herini za dhahabu, vidani vya dhahabu na manukato ili kumshawishi Bikisiwa akubali ndoa

yao. Bikisiwa alimkataa kata kata lakini Hassan hakukata tamaa kwani alitumainia kuwa siku moja Bikisiwa atakuja kukubali. Anasema:

> Pamoja na hayo, asiyependa mwanzo huenda akapenda mwisho. Nitabaki hapa penu. Najua siku moja utabadili mawazo ................... (uk 33).

Tunapata mfano mwingine wa wasafiri wavumbuzi wa Kolumba wanaotia nanga ufuoni wa Afrika (uk. 34). Hawa nao ni Wareno. Mfalme na watu wake walihofia kuwa ni watawala wa mabavu.

Anasema mfalme: ..........hawa ni watawala wa mabavu.Tena walazimishaji mambo. Baada ya kwisha tuteka watatunyang'anya kila kitu na kisha watatutaka lazima tuingie katika dini yao (uk 34).

Amirijeshi alitoa ushauri wa kupambana na wao. Amirijeshi akiwa ni kielezo cha wale wasaidizi wa mfalme. Mfalme anakataa wazo lake na kumpendekezea kuwa wapate msaada kutoka kwa SS badala ya kupigana na kutumia nguvu. Wana waza kuwa SS atakapotaka malipo kupitia kumuoa Bikisiwa, Bikisiwa asikatae. Bikisiwa naye hataki kuolewa na kutolewa kama mhanga. Mfalme naye anamwambia Bikiswa, "Hutaoelewa naye. Tutazikubali posa tu, halafu tutafanya mpango wa kuicheleweshà arusi kwa muda wa miezi sita. Tutamwandikia SS aje atuhami. Kwani sisi si watu wa dini moja" (uk 35). Wote wanakubaliana kufanya njama ya kucheleweshà arusi na kumficha Bikisiwa halisi na kumpa SS Bikisiwa mwingine. Hii ni thibitisho kuwa Waafrika walipinga hila na njama za wageni kutaka kutawala bara lao. Mgeni hana uwezo wa kujua ukweli Bikisiwa ni nani. Anaingia S S huku amevalia mavazi rasmi ya kifalme na ameambatana na watumishi

wake ambao wamebeba mabunda kwa mabunda ya zawadi (uk. 37). Baadhi ya watumishi wake wanafika wakimsifu. S S ni Seyyid Saidi wa himaya ya Waarabu. Anapokuja anajitambulisha kama mwenye huruma kwani sasa watesaji wameondoka. S S alipoingia, aliomba mambo matatu yatekelezwe na Bikisiwa.

i. Akubaliwe kuishi Afrika Mashariki

ii. Akubaliwe kuilinda nchi yao.

iii. Awe na usuhuba na Bikisiwa,

Bikisiwa anakubali ombi la kwanza. Kuhusu ombi la pili anasema kuwa ni bora wao walinde nchi yao lakini S S na watu wake wawe washauri. Anakubali pia ombi la tatu na kumtahadharisha huenda asiwe Bikisiwa halisi. Kihistoria, mkoloni mkongwe alikuja wakaishi nasi lakini kuna wale ambao hawakuwakubali kabisa. Miongoni mwa jamii zilizopinga ukoloni ni kama vile Wamaasai, Wagalla na Wanandi. Mataifa ya Kimagharibi waliweza kung'ang'ania Bara la Afrika na kuligawa kama himaya zao. Kuingia kwa waposaji mbalimbali ni ishara ya kung'ang'ania bara la Afrika. Hawa wote wanang'ang'ania rasilimali na uzuri wa Bara la Afrika. Rasilimali hizi zilihitajika kwa viwanda vyao na kuuzwa papa hapa Barani Afrika kwa bei ya juu. Kila mmoja alitamani Bara la Afrika kwani pia walikuwa wanatafuta soko ya bidhaa vyao.

Mfano mwingine wa ukoloni mkongwe ni majalio ya Bwana Biss (Biss mark). Anaingia Bwana Biss akisafiria VW. Vw (Volkswagen) ya Beetle'. (uk. 43). Anafuatana na mtumishi wake anayebeba mbegi mkubwa. Huyu naye anaashiria

Wajerumani. Walikuwa watu wenye kiburi na waliozoea ushindani. Biss anasema: "Mimi Biss mwakilishi wa kabila takatifu" (uk 43). Biss naye anataka kumposa Bikisiwa kutokana na sifa alizozisikia kama vile: bahari iliyoshwari, bandari nzuri, rasilimali za kipekee na rotuba ya kuotesha kila aina ya mimea. Anasema Biss.

> Asali au nini mimi nakubali kwamba uzuri wako haulinganishiki. Bandari izungukayo mwili wako ni shwari na ya kina. Bandari zako zote zimesitirika. Rasilimali za pekee mungu alizokajaii ndani ya nafsi yako. Madini ni nini kuliko ardhi ya rotuba ya kutosha, kila mimea ndani ya mwili wako?.......... (uk 44).

Anamshawishi Bikisiwa kwa kusema kuwa wao ni kabila takatifu, watu walioendelea kisayansi, kiufundi na kiteknolojia. Pia wameendelea katika elimu, kilimo, tiba na mawasiliano. Biss pia anamwambia Bikisiwa kuwa Wajerumani ni watu waliozoea ushindani. Anasema:

> Sisi tumejihindi kuunda udugu na nyinyi tokea zamani. Tumejifunza hata lugha yenu ya Kiswahili. Tutafahamiana kwa urahisi. Nasisi tumefanikiwa na mambo mengi ya sayansi, ufundi na teknolojia. Tumeendelea katika elimu, kilimo, sifa, tiba na mambo ya mawasiliano...................(uk 45).

Kihistoria ni ukweli Wajerumani walijifunza lugha ya Kiswahili. Bikisiwa anatambua nia ya Bwana Biss ni kama ya watangulizi wake. Ni walaji, wajinga, wanyang'anyi wala hawana nia ya kuwalinda. Baadaye Bikisiwa anamwambia tayari ameposwa na S S na aende ashindane naye na atautoa uamuzi wake kutokana na matokeo ya ushindani wao. Naye Biss akasema

Asante Bikisiwa. Si nimekwambia kwamba ushindani ndiyo siri yetu? Tutaona ..............ati S S, S S ni kitu gain? Mbele yetu hatumbi kitu. Yeye ni mtu au kitu? (uk 45). Bwana Biss yuko tayari kupambana na washindani wenzake ili

kukumposa Bikisiwa. Anasema kuwa yeye S S hawezi kushindana na Wajerumani kwani wao wameendelea kiteknolojia na wana silaha za vita.

Katika tamthilia hii, mposaji mwingine ni Bwana Chachi (William Churchill). Naye ni Mwingereza aliyevaa mavazi rasmi ya tabaka la juu. Yeye na msaidizi wake wanashuka kwenye gari lao rasmi la 'Land-Rover' lenye maandishi ya OHMS. Maandishi haya yanaashiria uwezo wa Mwingereza wakuweza kujikinga dhidi ya wazindani wake. Hawa wote wanang'ang'ania kuthibiti Bara la Afrika. Naye pia amekuja kutafuta posa na Bikisiwa. Anajigamba kuwa tayari wana himaya za ndoa na West Indies na visiwa vya Carribean, Cape Town kusini hadi Kairo. Naye anamshawishi Bikisiwa kuwa watastawisha kilimo, kupanua biashara na kuunda jeshi kuu la kulinda maslahi na mipaka yao. Pia, anamwambia ufalme utaongozwa na Malkia kama wao kwani bunge lao litapitisha sheria na kumpa mamlaka ya kuongoza himaya yao yote nzima.

Bwana Chachi anampa yamini na kumuondolea hofu yote. Anasema: usiwe na hofu yoyote. Nakulia yamini. Yote niliyokuahidi yatakuja kujiri (uk 50).

Bikisiwa anapewa zawadi kama pete ya dhahabu, mkufu wa dhahabu na ushanga wa dhahabu. Bikisiwa anamwambia kuwa zawadi amepokea, lakini si dhibitisho ya mapenzi yao.

### 4.1.3 Kipindi cha Ukoloni Mamboleo

Bikisiwa ni mtoto wa kihistoria. Tunambiwa kuwa Bikisiwa anaweza kuwa mtu (Mwanamke), hewa, ardhi, kichaka, jumuiya ya dhahiri au mawazo. Katika

kipindi hiki, Mwafrika amechukua hatamu za uongozi lakini anaendeleza sera za kikoloni. Hii inamaana kuwa uhuru waliopata Waafrika ni wa bendera tu.

Mwanamke anasema: ..............hii ni tamthilia ya hasira na hasara. Jiulize kwa nini miaka, mikaka na karne zote hizi wametuandama sisi? Hawataki kutuacha. Hawataki hata tupoe hata kidogo (uk 1).

Hii inadhihirisha kuwa hata kama wakoloni waliondoka wangali wanawafuata Waafrika. Viongozi wa Kiafrika waliochukua utawala waliendeleza mifumo kama vile ya utawala ya wakoloni kama vile kuwa na chifu, mkuu wa wilaya na mkuu wa mkoa. Pia, mifumo ya elimu tuliyoridhi ndiyo tuliyoendeleza. Vile vile, Waafrika hawakuwa na uhuru wa kiuchumi, na kwa hivyo iliwabidi viongozi wengine kuwa vikaragosi vya Wazungu. Utegemezi wa misaada pia unaendelezwa. Mwanamke anasema:

> Mtazameni, mtazameni vile. Sasa anatumia vivuli na sauti, badala ya mwili, ngozi, nyama na mifupa. Mtazameni bado anadai usuhuba kwa nguvu (uk 4).

Katika kifungu hiki, mwanamke anaashiria kuwa mkoloni yuko lakini kwa sura nyingine tofauti. Mkoloni anatumia vivuli na sauti katika kuendeleza utawala wake. Huu ni utandawazi unaoendelezwa kupitia vyombo vya habari na mawasiliano. Mkoloni amejificha katika utandawazi na anasikika katika nyanja zote za maisha ya Waafrika.

Mwanamke anasema: "Nini nyinyi mnaotafuta usuhuba wangu bila kujali hisia zangu?" (uk 2). Mwanamke anasisitiza kuwa hata kama kuna uwezekano wa

ushirikiano, lazima ushirikiano huo uongozwe na maslahi ya pande zote mbili. Msingi wa uhusiano bora huwa ni utu. Anaonyesha kuwa uhusiano huu wa kiutandawazi unanufaisha pande moja. Wazungu hujali maslahi yao wenyewe kuliko ya Waafrika. Utandawazi unaongozwa na ubinafsi na kwa hivyo umekuwa mfumo wa kuendeleza ukoloni mamboleo. Mkoloni amejificha ndani ya utandawazi.

Waafrika wametambua kuwa mkoloni yupo ingawa kwa njia tofauti. Hawakatai ushirikiano hila wanatamani majadiliano na kuheshimiana. (uk 2). Mwanamke anazidi kusema:

> Nyinyi ni wale mnaotaka kuudhibiti mwili wangu! Mwili unaweza kuchukua kwa nguvu lakini hamuwezi kuichukua roho yangu kwa nguvu (uk 2).

Ukoloni mamboleo pia unapatikana pale mfalme na jamii yake wanaendelea kusoma vitabu vilivyoandikwa kwa Kiingereza kama vile *Black Skins White Masks cha* Franz Fanon, *Siri ya kiongozi kuweza kudumu Uongozini* cha Mlalohoi Bin Msakatonge na *Marriages of Convenience* kilichoandikwa na Bwana Sasa Bongo Kali. Hivi vyote ni vitabu vinavyoonyesha dhana ya ukoloni mamboleo. Sogaramaneno anawapokea akina Hassan, Biss na Chachi. (uk 52, 53). Sogoramaneno anawakilisha viongozi wa Kiafrika ambao wanatumiwa kuendeleza sera za wakoloni na kuziangusha nchi za Afrika.

#### 4.1.4. Kipindi cha Utandawazi (Karne ya 21)

Mtambaji katika tamthilia hii anasimamia mbinu za kale za utambaji zilizotimika zamani kabla ya kipindi hiki cha utandawazi. Pia tunamuona mtumbaji akiwa mkimbizi kama anavyotuambia mtambaji:

> Kwa sababu mimi ni mkimbizi aliyepagazwa uhalifu. Ni mtambaji na mkimbizi na mhalifu wa kusingiziwa (uk 7).

Mtambaji anawakilisha tabaka la Waafrika la siku zilizopita. Usimulizi ulikuwa njia ya kuelimisha jamii, njia ambayo nafasi yake imechukuliwa na vyombo vya habari kama vile magazeti, vitabu, redio na runinga. Mtambaji anafukuzwa na teknolojia mpya na hawezi kuzikimbia hizo nguvu. Kipindi cha utandawazi huwa ni dhana ya kushirikisha nchi mbalimbali kibiashara, kiini hasa ni ushindani. Katika kipindi hiki, nchi zilizoendelea ndizo zinazofaidika. Tamthilia hii ya *Posa za Bikisiwa* si maigizo bali ni ufunuo wa kihistoria ambapo mja anafunguliwa kurasa za kihistoria yake kuafikiana na mifumo maalimu ya kuzalisha mali.

Dunia ya utandawazi imelinganishwa na mtoto wa kisasa. Bikisiwa ana safari nyingi kwa kipindi cha muda mfupi. Wakati mwingine yuko Washington, mara Dubai. Dunia nzima imo mkononi mwake. Kokote aendako hukufanya kuwa kwao. Hizi ni nguvu za utandawazi na hatuwezi kuziepuka. Kihistoria, viongozi wa Kiafrika wanapojiingiza katika ushirikiano huu wa kimataifa au wa nchi za Kimagharibi lazima wajue athari itawaandama wananchi wote. Utandawazi upo lakini huonekana katika athari zake. Utandawazi ni dhana inayoendeshwa kwa uhaulishi wa fedha na hundi kwenye mabenki au kwa njia ya kompyuta na pia

katika vyombo vya usafiri na mawasiliano ambamo ndimo unamojificha. Utandawazi ni nguvu kamili ya wale walioko upande wa tajiri dhidi ya wale walioko upande wa maskini na wanaozidi kudidimizwa. Mtambaji anasema:

> Nasema hivi. Posa au arusi ya Binti mfalme haiwi ya kiovyovyo tu.................. lakini lazima awe makini katika ubaguzi wake. Maana ndoa yake si yake peke yake. Ni ndoa ya sisi sote (uk 64).

Madhamuni ya utandawazi ni ya kukausha nchi changa kwa kutumia maneno matamu ya demokrasia, uwazi na uliberali mpya wa Benki ya Dunia na IMF, pia kuhodhi njia za shirika la fedha la kimataifa na ya matangazo ya runinga za kimataifa (uk 72). Huu ni wizi na unyanganyi wa kila kitu cha Mwafrika. Ni nguvu za nchi tajiri kudidimiza nchi maskini, Bikisiwa anasema:

> ...........Tunanyang'anywa kila kitu chetu mpaka vyakula vyetu, mpaka vitoweo vyetu kama vile samaki na nyama. Twanyang'anywa pasi na sisi kuwa na nguvu za kuzuia unyang'anyi huo. Isitoshe, tunaharibiwa mazingira yetu, mito, maziwa, vidimbwi, fukwe, upwa, pwani na bahari. Pia amali zetu tunazothamini zinafujwa kupita kiasi. Unaparaganywa utamanduni wetu na sisi bado tumo tunatazama tu (uk 73).

Watunzi wa tamthilia hii wanapendekeza mambo yafuatayo ili kukabiliana na utandawazi na athari zake: Mfumo wa elimu kufanyiwa mabadiliko, kukuza vipawa vyetu vya akili ili tuweze kuvithamini vitu vya watu wengine, kufuata amali za utamaduni zenye uzito kwetu, tuamke na tupiganie haki zetu na tupiganie kwa umoja wetu wa ndani na wa nje pamoja na nchi jirani.

**4.2 Maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi**

Tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* ni tamthilia ya kihistoria inayosheheni matukio mbali mbali ya kihistoria. Waandishi wa tamthilia hii, kwa kutumia jazanda ya posa wamejaribu kudhihirisha aina mbalimbali za mahusiano baina ya mataifa tawala na yaliyotawaliwa. Baada ya kupata uhuru, Waafrika waliendelea kunyanyaswa na kudhulumiwa na mataifa tajiri. Hata baada ya kuondoka, athari za wakoloni zilibakia katika nchi zilizotawaliwa. Katika kifunguzi, mwanamke anasema: .... Hii si dunia ya kulala. Si dunia ya mahubiri na maombolezo. Hii ni dunia ya unyang'anyi (uk 1).

Wakoloni waliendelea kuwanyanyasa Waafrika hasa kupitia mifumo yao ya dini. Hii ndiyo sababu mwanamke anasema kuwa hii si dunia ya mahubiri bali ni dunia ya unyang'anyi. Hapa dini ilitumiwa na wakoloni kulinda na kuendeleza maslahi yao. Mwafrika alinyang'anywa imani na itikadi zake. Waafrika wanaendelea kudharau kilicho chao asili na kukumbatia yaliyo ya wakoloni.

Anaendelea kusema:

> .......Hii ni tamthilia ya hasara na hasira. Jiulize kwa nini miaka, mikaka na karne zote hizi wametuandama sisi? Hawataki kutuacha. Hawataki hata tupoe hata kidogo (uk 1).

Jambo hili linadhihirisha kuwa Waafrika walipokea uhuru wa bendera lakini wakoloni waliendelea kuwafuata. Waafrika hawakupata uhuru wao kisiasa, kiuchumi na hata kijamii. Wakoloni waliendelea kudhibiti kila nyanja ya maisha ya Waafrika. Mwanamke anasema kuwa viongozi wa Waafrika walijifanya vipofu na viziwi.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Anauliza. .... Kwa nini unaachia maovu yatendeke mbele ya macho yako? Kwa nini umetia komango za masikio usisikie kelele za jirani yako? (uk. 2).

Viongozi waliochukua uongozi baada ya wakoloni hawakujali maslahi ya wananchi. Walinyamaza kimya huku wakoloni wakiendelea kuwadhulumu wananchi. Hawa wakoloni walitumia mbinu mpya za kuendeleza utawala wao. Mwanamke anauliza.

> ... Nani nyinyi mnaotafuta usuhuba wangu bila ya kujali hisia zangu? Nani nyinyi mnaojificha nyuma ya ndoa mpya? ... mnatoka kujichoma katika ndoa isiyojadiliwa? (uk. 2).

Said A Mohamed na Kitula King'ei wanaonyesha kuwa wakoloni walitafuta mbinu mpya za kuendeleza utawala wao dhidi ya Waafrika. Walitumia mbinu mpya za kisiasa, hasa demokrasia na mbinu mpya za kiuchumi hasa katika biashara. Uhusiano wa aina hii haukubaliki maana ni uhusiano ambao haujachunguzwa na kukubaliwa na wengi. Kama Waafrika wataweza kunufaika na maingiliano mapya ya kimataifa, itawabidi wayajadili kwanza ili kuona manufaa yao. Mwanamke anawashtumu viongozi wa Bara la Afrika kwa kukubali posa na nchi tawala bila kuwahusisha wananchi. Anasema kuwa uhusiano mpya unaweza kukubaliwa ikiwa ni uhusiano wenye nia njema na wenye kuheshimiana. Waposaji waliweza kutumia mbinu nyingi ili kuweza kuingia katika mahusiano na viongozi wa kiafrika.

Said A. Mohamed na Kitula King'ei wanaonyesha vile Waafrika waliweza kuingia katika utumwa wa wakoloni. Wakoloni walitumia mbinu za ujanja

kuwahadaa viongozi wa Waafrika. Kuna wale kama akina Sogoramaneno ambao wanajitokeza kama kabila lenye nguvu na kuwaahidi kuwa watawalinda.

Bikisiwa anamwambia babake:

> Samahani baba, lakini kosa ni lako wewe kwa kutotaka kushahuriana na raia kuhusu posa zangu- jambo ambalo kama hili kubwa kuliko jingine lolote katika familia yetu na katika ufalme wako kukutaka kumshauri mtu yeyote? (uk.. 18).

Jambo hili linadhihirisha kuwa, viongozi wengi wa Kiafrika waliingia katika mahusiano na nchi za kigeni bila kushauriana na wananchi. Uhusiano wa aina hii ulikuwa tu ni wa kujali maslahi ya pande moja. Ndipo Bikisiwa anasema kuwa posa au uchumba lazima usimame ndani ya nafsi za wanaochumbiana. Anaendelea kusema kuwa wote walitamani sana kumwoa kwa maslahi yao.

Katika enzi za kikoloni, Waafrika walichukuliwa kama viumbe duni, visiojiweza, watu dhaifu na wajinga. Mielekeo ya wakoloni dhidi ya Waafrika ilikuwa hasi kama anavyo dhihirisha Bikisiwa:

> Mwenzangu kamwe hanijali wala hanibali. Anasema kuwa ........ si vibaya kuposana iwapo posa ni yenye nia njema. Si vibaya kuoa, iwapo ndoa ni ya kuheshimiana (uk. 2).

Ukoloni mamboleo uliendeleza maslahi ya wakoloni bila kujali maslahi ya nchi maskini. Wakoloni walitamani kila kilicho kizuri cha Waafrika. Rasilimali zote za Waafrika zilitumiwa na wakoloni ili kuendeleza nchi zao kiuchumi. Mwanamke anawaonya kuwa, hata kama wanaweza kudhibiti mwili wake, hawataweza kudhibiti roho yake kwa nguvu. Waandishi wanaonyesha jinsi ndoa ilivyotumiwa na wakoloni

kuendeleza maslahi yake. Malkia anakisoma kitabu kinachoitwa *Nitaolewa Nikipenda* cha Ngugi wa Thiong'o. Anasema hivi:

> Ama kweli kumbe dini na ndoa huweza kutumiwa na malaghai kubatilisha mambo na kuwaadhibisha watu wasio na hatia? (uk. 17).

Hii inaonyesha mbinu walizozitumia wakoloni kuendeleza maslahi yao. Dini ilitumiwa na wakoloni ili kunyakua mashamba yenye rotuba ya nchi walizotawala huku watawaliwa wakichukua sehemu ambazo hasikuwa na rotuba nyingi. Pia dini ilitumiwa na wakoloni kuwaliwaza Waafrika ili wasifunguliwe macho yao na kuona unyanyasaji na dhuluma walizofanyiwa na wakoloni.

Uhusiano uliokuwa kati ya Waafrika na wakoloni unafananishwa na posa. Bikisiwa anasema: "Kwake mini ni kiatu kibovu. Kila shauri lazima akate yeye. Chumo lote kwa nguvu atwae yeye" (uk 22). Mkoloni hakumpa Mwafrika nafasi ya kujiamulia kilicho kizuri kwake. Bikisiwa anatetea haki yake kwa kusema kuwa pia yeye ana haki kama binadamu wengine. Anataka kujikomboa kutokana na posa ya udhalimu na kudai uhuru wake na usawa. Kwa kutuonyesha asili ya utandawazi, tunamwona mtambaji akimwahadithia mpita njia hadithi. Anamweleza kuwa yeye ni mkimbizi aliyepagazwa uhalifu lakini yeye ni mkimbizi na mhalifu wa kusingiziwa. Anasema:

> ...nimo mbioni ninaandamwa na kufukuzwa na jitu ovu linalohofu kazi yangu inayofichua upotofu katika jamii. Jitu linalojifanya kuwa ni muhimu zaidi kuliko mtu yeyote kuliko hata jamii. (uk. 9).

Utandawazi unaelezewa kama kitu kilicho na nguvu ya kutawala kila kitu. Kama anavyosema mtambaji, utandawazi hudhibitiwa na watu wenye nguvu na ambao huongozwa na tamaa na msalahi yayo wenyewe. Anasema:

> ... lakini najua nina kimbia nini. Nawakimbia watu wenye nguvu wanaonifukuza wanikamate ili kuendeleza maslahi yao maovu....watu wetu wote wanavutiwa na vyombo vya habari, hasa vile vya kutoka nje... (uk. 11).

Said A. Mohamed na Kitula King'ei wanaashiria kuwa tangu majaliwa ya utandawazi, fasihi simulizi iliyokuwa msingi wa utamaduni wa jamii za Kiafrika imekoseshwa nafasi na kugunduliwa kwa teknolojia mpya ya habari na mawasiliano. Hii ndio sababu mtambaji anasema kuwa hana watu ambao wangependa kumsikiliza. Watu wengi wanavutiwa na vyombo vya habari vya nje na ambavyo vinaendeleza utamaduni wa kigeni. Kwa kutumia mhusika mtambaji, waandishi hawa wanawaonya Waafrika dhidi ya kukimbilia utamaduni wa kigeni. Mtambaji anasema:

> Ndiyo, lakini na hivyo vyombo vya habari navyo vina matatizo yake. Havijali historia na mazingira ya nchi yetu kama tunavyojali sisi. Na kama tujuavyo, watu hutawaliwa kirahisi wakisahau historia yao... (uk 10).

Kwa ujumla, utandawazi unachangia pakubwa kuendeleza dhuluma na unyanyasaji kwa Mwafrika. Hivi vyombo vya habari tunalazimishwa navyo. Huwa havina ari na uchungu katika kuchagua na kupanga habari zilizo na maslahi ya Waafrika. Hivi vyombo hutumiwa na wakoloni kudidimiza sauti dhaifu za Waafrika na kuzipa nafasi kubwa sauti za wakubwa wa nje na ndani ya nchi za Waafrika. Teknolojia

mpya ya habari na mawasiliano imetumiwa na wakoloni kuendeleza utamaduni wao katika Bara la Afrika, jambo ambalo limezua momonyoko wa maadili ya Kiafrika.

Mwafrika hufanywa kuchukia kilicho chake na kupenda kile cha kigeni. Huu ni ukoloni mamboleo unaoendelezwa katika mfumo mpya wa utandawazi. Hata hivyo, hivi vyombo vya habari vina manufaa yake hasa katika karne hii, kama anavyosema mtaambaji:

> najua kwamba katika karne hii tulivonavyo kuna sehemu ambayo mimi siwezi kuitelkeleza ukilinganisha na vyombo vya habari….ile sehemu ya kutafuta na kupekua matokeo au ile sehemu ya utapatakazaji wa habari zenyewe…(uk 10).

Anaendelea kuonyesha kuwa utandawazi una manufaa mengi kama vile kuweza kufikia taifa nzima na hata umataifa, usambazaji na uenezaji wa habari kote ulimwengani kwa urahisi na pia kwa haraka wa wepesi wa kusambaza taarifa na kubana wakati. Kwa kufafanua maana ya utandawazi, wanasema:

> utandawazi ni dude au nyangarika linalopita kila pahala kuhakisha maslahi yake yanatimizwa kwa kutimia hila au nguvu. Likikosa maslahi yake huwaandama maadui au hata marafiki zake kuwakamata au kuwaua. (uk 24 hadi 25).

Utandawazi ni dhana ambayo imepewa jina la nyang'anya au manyung'unya. Utandawazi huwanyang'anya watu kilicho chao na kuwaacha kama watu wasio na asili. Utandawazi ni dhana ambayo imetapakaa katika kila nyanja ya maisha ya binadamu na ndiyo maana mtambaji anasema kuwa huwezi kujiepusha na utandawazi. Mtambaji Anasema:

> Ukweli ni kwamba halikimbiliki. Liko hewani. Liko juu ya ardhi. Liko chini ya ardhi .....liko ndani ya maji katika mito, maziwa, pwani na bahari. Limo katika mfumo wa elimu, limo katika mikutanoni na kongomano zote....limo hata akilini mwetu.... (uk 25).

Waandishi hawa wanaashiria kuwa utandawazi ni kitu ambacho kimeingiliana na maisha ya binadamu. Utandawazi umedhihirika kote ulimwenguni. Katika mfumo huu, watu huchukuliwa na kupelekwa hata kule hawataki kama anavyosema Bikisiwa:

> ......Tokea kuingia utawala wa Sogaramaneno unakamatana na utandawazi, watu siku hizi hukamatwa tu akiwa YEYE anataka. Hukamatwa wakasafirishwa na kupelekwa kwake na kuuzwa kama samaki au kuuzwa kwa malipo ya hisani ya mafunzo ya kijeshi na rundo za slaha mbovu (uk. 65).

Mkoloni amejificha katika utandawazi ili kuendeleza maslahi yake na kwa manufaa yake mwenyewe. Utandawazi ni mbinu mpya ya ukoloni mamboleo Bikisiwa anasema: "Utandawazi ni mtu au kikundi cha watu wanaojificha nyuma ya kivuli cha U-YEYE au picha ya YEYE."(uk 66). Wakoloni walizua mbinu mpya ya kuendelea kutawala koloni zao kupitia mfumo wa utandawazi kama anavyopsema Bikisiwa:

> .........ni mtu au dude tu lisilo na imani wala hisia. Chakula chake ni pesa na utajiri wa jamii mbalimbali." (uk 66).

Ukoloni unaweza kuonekana kupitia ishara zake kama vile ubalozi, elimu na utamaduni. Pia utandawazi hudhihirika katika athari zake. Ubeberu na ukoloni una sehemu gandifu inayoonekana na kushikika. Ndani ya ubeberu na ukoloni mamboleo kuna kikundi cha watu katika mataifa fulani waanaojitambulisha na ubeberu na

wanaoendeleza ukoloni mamboleo kwa misaada na mikopo. Makundi hayo pia huja katika nchi zilizokuwa himaya zao na kuchukua rasilimali za Waafrika kwa lengo la kujinufaisha wao wenyewe. Makundi haya huongozwa na mielekeo ya kikoloni ambayo ilidhamiria kumdunisha, kumnyanyasa na kumkandamiza mtawaliwa.

Utandawazi kama wanavyosema Said A Mohamed na Kitula King'ei (2008), ni dhana inayoendeshwa kwa uhaulishi wa fedha na hundi kwenye mabenki au kwa njia ya kompyuta na pia katika vyombo vya usafiri na mawasiliano ambamo ndimo unamojificha. Utandawazi ni jina ambalo ni geni kwa mataifa changa linalosimamia madhumuni ya kukausha nchi zinazoendelea. Utandawazi hutumia maneno matamu ya demokrasia, uwazi na uliberali mpya wa Benki la Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ili kuendeleza dhuluma na na tuhuma zao kwa nchi changa. Mataifa haya huwekewa vikwazo vikubwa ili kuweza kupata misaada na mikopo na ambayo baaadaye huyafukarisha. Nchi maskini huwekewa vikwazo ili kupata misaada na mikopo na baadaye hufanikisha mataifa ya Ulaya. Ukosefu wa uhuru wa kiuchumi hufanya nchi changa kuabudu mataifa ya Ulaya. Utandawazi basi ni mbinu mpya ya wakoloni kuendeleza sera zao na kudumisha utawala wao katika mataifa masikini.

Lengo kuu la utandawazi ni ushindani. Mataifa ya Kiafrika hayawezi kushindana na mataifa tajiri kwani hao ndio waliomiliki mbinu zote za uzalishaji mali. Said A Mohamed na Kitula King'ei wanasema kuwa biashara ambayo imekuwa msingi wa ushirikiano wa kitaifa hutumika kuendeleza dhuluma. Anasema Bikisiwa:

> ushirikano ni mzuri, lakini ushirikiano wa namna gani? Ushirikiano umekuwepo duniani tokea enzi za zamani. Biashara imedumu karne nyingi sana miongoni mwa watu duniani kote. Lakini katika karne zote hizo biasharea imekuwa ikiwekewa misingi ya dhuluma, na mpaka sasa bado inasimamia dhuluma (uk 73).

Kwa hivyo utandawazi ni wizi. Kupitia utandawazi, mataifa machanga hunyang'anywa kila kitu. Wananyang'anywa utamaduni wao na vyakula vyao vizuri kwa kutokuwa na nguvu ya kupambana na utandawazi. Mataifa machanga huishia kukubali masharti ya kinyonyaji. Anaendelea kusema Bikisiwa: Tunanyang'anywa pasi na sisi kuwa na nguvu za kuzuia unyang'anyi huo. (uk .73).

Waafrika wanaishia kukubaliana na utandawazi kwani hawana ujuzi wa teknolojia mpya wa kuweza kupambabana na utandawazi. Utandawazi umechukuliwa kuwa ndio dawa ya umaskini kama unavyosema mpitanjia:

> lakini nimesikia kwaamba hakuna nchi inayoweza kuepuka utandawazi… Yaani watu husema utandawazi ni kama dawa chungu ya maradhi ya umaskini… (uk 72 hadi 73).

Maoni kama haya hutumika kama mtego wa kuwanasa watu wasio na nguvu ya kiuchumi. Utandawazi umechangia pakubwa katika kuharibu mazingira kama vile mito, maziwa, upwa na bahari. Kupitia kwa utandawazi, mali za Waafrika wanazozithamini hufujwa. Anasema Bikiwa:

> Pia amali zetu tunazozithamini zinafujwa kupita kiasi. Unaparaganywa utamaduni wetu na sisi bado tunatazama tu! (uk 73).

Baada ya kuzinduka, Mwafrika anaanza kupambana na utandawazi ingawa anajua kuwa utandawazi ni nguvu ambayo ina misingi yake katika mataifa tajiri. Anajaribu kwa vyovyote vile kupambana na hizo nguvu. Bikisiwa anasema

> Sitaposwa na YEYE maanaYEYE mimi pia simtaki. Nangojea posa za hapa petu, bila ya shaka zikiwa posa za maslahi ya pande zote (uk 67).

Hii ni dhihirisho kuwa Mwafrika anataka kujiondoa katika uhusiano usio na manufaa kwake. Pia, kwa kutumia wahusika Cecilia na Jane, waandishi hawa wanaonyesha vita dhidi ya utandawazi.

> Cecilia: (Huku akikwangura ukuta) Twasema ondoka
> Jane: Ondoka haraka.
> Cecilia: Ondoka nakwambia.
> Jane: Tutakukwangurakwangura sisi. Tutakuchanachana kama karatasi. (uk 69).

Wahusika hawa wanaelekeza hasira zao kwenye kuta kwa kupambana na uwezo wa utandawazi. Bikisiwa anasema kuwa, kwanza itawabidi wakusanye nguvu zao zote ili waweze kuungana na kupigana na utandawazi. Watunzi wa tamthlia hii pia wamefaulu kuwasilisha athari za utandawazi hasa kwa vijana. Bikongwe anawakilisha ukale wa sehemu yake katika jamii na ni ukumbusho wa yale yanayopotea na yale yanayozuka na kuathiri nchi za Kiafrika na kupitia kwake tunaelezwa athari za utandawazi kwa vijana wa siku hizi kama vile: Mavazi yasiyositiri. Vijana wa siku hizi wanakwenda uchi jambo mbalo ni kinyume na utamaduni wa Mwafrika. Matumizi ya lugha isiyoeleweka. Hao vijana husema lugha isiyoeleweka. Kizungu si kizungu, kichina si kichina, kiswsahili si kiswahili (uk 74). Pia vijana wa siku hizi huimba nyimbo zisizoeleweka, pia fikira zao hasieleweki. Malengo yao, hamu zao hayaeleweki. Tunaambiwa kuwa kila siku utaona kwamba hawapo hapa wakichanganywa na vyombo vya habari, wao ni watumwa wa utandawazi (uk 75).

## 4.3. Mtindo kama mkakati wa kuendeleza ukoloni mamboleo na utandawazi.

Mtindo ni njia ya kipekee ambayo mwandishi mmoja anajitofautisha na mwingine kwa jinsi anavyotumia lugha kuelezea maudhui yake. Katika utafiti huu tumechunguza mtindo kama mkakati wa kuendeleza maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi. Said A. Mohamed na Kitula King'ei wametumia mbinu zifuatazo ili kuwasilisha ujumbe wao.

### 4.3.1. Mpangilio wa tamthilia

Tamthilia yenyewe imegawanywa katika vipindi mbalimbali. Vipindi hivi vinaashiria vipindi tofauti vya kihistoria ambavyo vimenasibiwa na Bara la Afrika hasa Afrika Mashariki. Vipindi hivi vya kihistoria kama vifuatavyo: Kipindi cha utumwa ni cha karne ya 14. Katika kipindi hiki, Waafrika walichukuliwa na kuuzwa katika mataifa ya Amerika. Walitumiwa kufanya kazi ngumu kwa mashamba ya Wazungu na kwa malipo duni. Kipindi cha ukoloni mkongwe cha karne ya 19, ambapo Wazungu waling'ang'ania mataifa ya Bara la Afrika. Waligawanya mataifa haya na kuwa himaya zao. Waafrika walitawaliwa na kufanyishwa kazi ngumu na kwa malipo duni. Walinyimwa uhuru lakini baadaye Waafrika waliungana na kupinga ukoloni. Kisha kuna kipindi cha ukoloni mamboleo. Baada ya Waafrika kupata uhuru, uhuru wao ulikuwa wa bendera tu. Hawakuwa na uhuru wa kisiasa, kiuchumi na hata wa kiutamaduni. Athari za ukoloni ziliendelezwa kwa mifumo ya uongozi na viongozi wa Afrika wenyewe. Hatimaye kipindi cha utandawazi. Hiki ni

kipindi kinachofanana na Ukoloni Mamboleo ingawa kimechukua sura moja. Hii ni dhana ya kushirikisha nchi mbalimbali kibiashara katika Soko huria. Kiini hasa ni ushindani. Nchi zilizoendelea ndizo zinazofaidika. Hii ni njia moja ya kuwanyonya na kuwanyanyasa Waafrika kiuchumi. Mtambaji anasema:

> ------- Dunia yote inalisubu, lakini halisikii wala halijali. Likiwa limeshughulika namna hiyo husambaza makuwadi wake walitumikie. Na makuwadi wake siku hizi ni hata wale waliomo katika nchi kubwa wanaomngojea yeye akitupa mifupa wang'ong'one .......... (uk 25).

Anadhihirisha kuwa wadhibiti wa utandawazi ni mataifa matajiri. Hawa hutumia makuwadi ili kuendeleza maslahi yao. Huu ni ukoloni mamboleo katika utandawazi.

### 4.3.2. Usimulizi.

Usimulizi ni mbinu iliyotumika kwa wingi katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa*. Kwa kumtumia mhusika mtambaji, Said A. Mohamed na Kitula King'ei wameweza kuonyesha majilio ya utandawazi na ukoloni mamboleo. Katika hadithi, mtambaji anasimulia hadithi ya mwanamke wa zamani na wa sasa. Kwa kutumia mbinu ya usimulizi, waandishi hawa wamefanikiwa kutupa taswira halisi ya ukoloni mamboleo na utandawazi. Mtambaji anahadithia hadithi ya *Posa za Bikisiwa*. Tamthilia hii ni kama hadithi inayosimulia majilio ya utandawazi. Inadhihirisha jinsi mataifa tajiri yanavyotafuta usuhuba na mataifa maskini huku yakiwanyonya na kuwanyanyasa. Ukoloni na ukoloni mamboleo ulifumwa kwa utaratibu maalumu.

### 4.3.3. Matumizi ya jazanda.

Jazanda ni mafumbo ambamo ndani yake maana ya kitu kimefichika. Katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* kuna jazanda zifuatazo. Kwanza kuna jazanda ya mwanamke. Mwanamke hapa ametumiwa kuashiria mazingira, historia na utamaduni wa Mwafrika. Mwanamke hapa pia ameashiria rasilimali za Bara la Afrika. Anaweza kuwa ni madini, maziwa, bahari au watu wa Bara la Afrika. Hivi ndivyo vilivyovutia Wazungu na wageni kutoka mataifa ya nje kutamani Bara la Afrika.

Pili, kuna jazanda la Posa. Posa hapa linatumwa kama uhusiano. Kihistoria viongozi wa Kiafrika wanapojiingiza katika ushirikiano huu wa kimataifa kwa mfumo wa utandawazi lazima wajue una athari zake kwa raia. Lazima uhusiano wa aina hii ujadiliwe na kila mmoja. Anasema mtambaji:

> Nasema hivi; Posa au arusi ya binti mfalme haiwi ya kiovyoovyo tu. Kweli binti mfalme ana uhuru wa kuchagua mchumba na mume kama mvulana au binti yeyote. Lakini lazima awe makini katika uchaguzi wake Maana ndoa yake si yake pekee yake. Ni ndoa ya sisi sote. (uk 64).

Viongozi wanatolewa tahadhari hasa katika kipindi cha utandawazi kabla hawajakubali ushirikiano (Posa). Wanaonywa wajitazame, wajichuje, wajiangalie na kujipima. Wana uhuru wa kuzijadili posa hizo ili zimfae mwananchi. Bikisiwa anasema:

> Baba. Naomba ufanye kulihali
> Unipunguzie idhilali
> Hapa hebu nipe dalili
> Posa zipigwe darubini kali



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Iwe posa njia mbili
Tuposane kwa adili
Jumuiko la wawili
Lenye tija, heshima na mustakabali ------- (uk 23).

Bikisiwa anatoa ushauri kwa viongozi wa Bara la Afrika. Anasema kuwa uhusiano wa kiutandawazi lazima uwe na manufaa kwa pande mbili. La sivyo upigwe marufuku. Utandawazi unatumiwa kuwanufaisha wale wenye nguvu maana wao ndio wanaodhibiti nyenzo za utandawazi. Hivyo basi, kuna haja ya kujadili uhusiano huu hadharani na kuupima na kupiga msasa ili uweze kuwa wa manufaa kwa wananchi wote.

Katika mfumo wa utandawazi, Waafrika hawakuhusishwa kamwe kuhusu masuala muhimu ya mfumo huo. Malkia anaeleza kwa kusema:

> Sisi wanawake hatutelezi tu, tunaanguka hasa! Na wanaotusukuma ni nyinyi wanaume, maana ndio mnaokamata hatamu na kuvuta. (uk.22).

Hapa anamaanisha kuwa wanaume (wenye nguvu za kiuchumi) ndio wanasababisha kuanguka na kuteleza kwa wanawake (mataifa maskini) ambao hawana uwezo wa kujiamulia au kujisimamisha wenyewe. Hii inaonyesha athari ya utandawazi katika Bara la Afrika. Nchi nyingi za Afrika zimeanguka kiuchumi kutokana na utandawazi ilhali nchi za Ulaya na Amerika zina uwezo wa kiuchumi. Bikisiwa pia anawashauri viongozi kwa kutumia methali "Mwamba ngoma kawa, ngozi huivuta kwake" (uk 22). Hapa anamaanisha kuwa mataifa tajiri wanatumia mfumo wa utandawazi kujinufaisha wao wenyewe. Hivyo inawapasa viongozi wa mataifa changa kuwa waangalifu na makini katika uhusiano wao na mataifa tajiri.

#### 4.3.4. Matumizi ya taswira.

Taswira ni picha ya mambo au vitu inayomjia mtu akilini mwake baada ya maelezo kutolewa. Said A. Mohamed na Kitula King'ei wametumia mbinu hii ili kuelezea na kufafanua dhana ya utandawazi. Kupitia kwa mtambaji utandawazi umefananishwa na zimwi, jini, pepo, kibwengo, muumiani, dude, nyangarika na nyang'anya manyung'unya. Kupitia kwa majina haya, utandawazi umechorwa kama kitu kiovu na kibaya, ambacho kinaweza kuangamiza Mtambaji anasema:

> Ni dude linaloitwa utandawazi. Ni dude au nyang'arika linalopita kila mahala kuhakikisha maslahi yake yanatimizwa kwa kutumia hila au nguvu. Likikosa maslahi yake, huwaandama maadui au hata marafiki zake kuwakamata au kuwaua. ....... (uk 24 – 25).

Kulingana na mtambaji, utandawazi ni mbinu mpya ya unyang'anyi. Utandawazi umo kila mahali. Uko juu ya ardhi, chini ya ardhi, uko ndani ya maji katika mito, maziwa, pwani na bahari. Uko pia katika mfumo wa elimu, ndani ya vyombo vya habari na kila sehemu ya maisha ya watu.

Utandawazi pia umelinganishwa na ubabedume. Tunaambiwa kuwa bado umwamba wa kiume umetawala na bado humo akilini mwake. Mtambaji katika *Posa za Bikisiwa* anasema kuwa wanawake wanabakwa na aliyewabaka sheria haimkamati kwani wanawake wenyewe wanataka kubakwa. Wanaume wanawabaka wanawake lakini anayewabaka sheria haimfungi. Wanawake ndio wanaokubali kubakwa. Hii inaashiria kuwa wakoloni walitumia nguvu kuchukua rasilimali za Waafirika na pia kuna baadhi ya viongozi wa Kiafrika walioshirikiana na wakoloni. Kuna baadhi ya



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

nchi za Kiafrika wanaokubali mfumo wa utandawazi bila kuupinga kwa vyovyote vile. Wanakubali vibovu vinavyotokana na utandawazi.

Hii inamaanisha kuwa katika mfumo wa utandawazi mataifa ya Bara la Afrika yanatumiwa kwa nguvu na mataifa tajiri. Hii ni kwa sababu sheria na kanuni za utandawazi zimewekwa kulinda maslahi ya wenye nguvu. Mataifa ya "Dunia ya Tatu" hayana uwezo wa kujikinga dhidi ya utandawazi. Huu ni ukoloni mamboleo katika utandawazi. Katika mfumo wa ubabedume, wanawake wanarushwa juu angani na wanaume na kuanguka chini wakiwa wameumia vibaya. Hii inaashiria kuwa mataifa machanga yamedhoofishwa na mfumo wa utandawazi.

**4.4. Kiishilio.**

Katika sura ya nne, tumetoa muhtasari wa tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* ili kufahamu wazo lake kuu. Tumeshughulikia maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi. Aidha, tumeshughulikia mtindo kama mkakati wa kuendeleza ukoloni mamboleo na utandawazi. Katika sura inayofuata tutatoa hitimisho la tasnifu hii. Vile vile, tutaonyesha matokeo ya utafiti mchango, changamoto tulizozikabili katika utafiti na hatimaye tutatoa mapendekezo kwa watafiti wengine.

# SURA YA TANO.

# HITIMISHO

## 5.0. Utangulizi

Katika sura hii muhtasari wa utafiti umetolewa. Aidha lengo kuu la utafiti limeelezwa pamoja na upeo wa utafiti na yaliyomo katika kila sura. Vile vile, matokeo ya utafiti yamejadiliwa kwa undani kwa kuonyesha jinsi utafiti ulivyofanikiwa katika kuyafikia malengo yake. Pia matatizo tuliyoyakabili yameelezwa, mchango wa utafiti umejadiliwa na hatimaye mapendekezo ya tafiti za baadaye yametolewa.

## 5.1. Muhtasari.

Utafiti huu uliongozwa na malengo manne. Kwanza tulilenga kutambua na kuchanganua sura mbalimbali za ukoloni mamboleo na utandawazi kama zinavyofasiriwa katika tamthilia za *Posa za Bikisiwa* na *Sudana*. Pia utafiti wetu ulilenga kuonyesha jinsi utandawazi unavyotumika kuendeleza ukoloni mamboleo kama unavyojitokeza katika tamthilia za *Posa za Bikisiwa* na *Sudana.* Aidha tulilenga kubainisha athari za ukoloni mamboleo na utandawazi katika *Posa za Bikisiwa* na *Sudana.* Hatimaye utafiti ulitenga kuonyesha mtindo unaotumika kufafanulia utandawazi.

Utafiti wetu umeonyesha wazi kwamba utandawazi ni mbinu mpya ya kuendeleza mfumo wa ukoloni mamboleo. Uchunguzi wetu umethibitisha kuwa

ukoloni mamboleo umekita mizizi katika utandawazi. Utandawazi umetumika kuendeleza dhuluma katika mataifa maskini. Utafiti wetu pia umebainisha kuwa utandawazi ambao unaendezwa katika uchumi na biashara ni mbinu mpya ya ukandamizaji, unyonyaji na unyanyasaji inayoendelezwa na mataifa ya Kimagharibi dhidi ya mataifa ya "Dunia Ya Tatu".

Ili kufikia malengo yetu, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Baada - ukoloni. Wanaotumia nadharia hii hukemea mataifa maskini ambayo yanatumiwa na mataifa matajiri kuendeleza tamaa zao za kudhibiti uchumi na biashara. Tumetumia mihimili inayojitokeza katika tamthilia hizi mbili. Tumeonyesha jinsi mihimili hii inavyoweza kutumiwa kuchambua tamthilia zetu mbili na kudhihirisha kuwa tamthilia hizi zimeandikwa kwa misingi ya nadharia ya ukoloni mamboleo. Tamthilia hizi mbili zimeweza kuchambuliwa ili kupata data ya kutosha kulingana na malengo yetu ya utafiti. Tasnifu yetu imegawanywa katika sura tano.

Sura ya kwanza ambayo ni utangulizi imeshughulikia masuala ya kimsingi. Haya ni mambo kama vile usuli, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, misingi ya nadharia ya Baada - ukoloni iliyoongoza utafiti wetu na udurusu wa maandishi juu ya mada. Sura hii pia imeangazia mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

Katika sura ya pili, tumeshughulikia maisha ya waandishi wa tamthilia za *Sudana*, Alamin Mazrui na Kimani Njogu na waandishi ya *Posa za Bikisiwa,* Said

A. Mohamed na Kitula King'ei. Pia tumeonyesha waandishi na ukoloni mamboleo kama utandawazi. Kwa kufanya hivyo, tumeonyesha vile wameweza kushirikiana kushughulikia suala la ukoloni mamboleo na utandawazi.

Sura ya tatu imeshughulikia maudhui ya ukoloni mamboleo katika utandawazi kwa kurejelea tamthilia ya *Sudana.* Muhtasari wa tamthilia umeshughulikiwa pia. Aidha katika sura hii suala la mtindo kama mkakati wa kuendeleza ukoloni mamboleo na utandawazi umeshughulikiwa. Tumeangazia matumizi ya usimulizi, matumizi ya nyimbo na usemi. Tumedhihirisha kuwa waandishi wa tamthilia ya *Sudana* wameweza kutumia mbinu hizi hili kusuka suala la ukoloni mamboleo na utandawazi.

Katika sura ya nne tumeshughulikia maudhui ya ukoloni mamboleo na utandawazi katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa*. Pia tumeonyesha jinsi mtindo umetumika kama mkakati wa kuendeleza ukoloni mamboleo. Mbinu zilizotumika ni kama vile usimulizi, jazanda na taswira ili kuthibitisha ukoloni mamboleo katika utandawazi. Tumeonyesha wazi jinsi waandishi hawa wawili wameweza kushughulikia suala la ukoloni mamboleo na utandawazi.

## 5.2. Matokeo ya utafiti.

Utafiti huu ulilenga kuyatimiza malengo manne. Lengo la kwanza lilikuwa ni kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ukoloni mamboleo na utandawazi kama unavyofasiriwa na tamthilia za *Posa za Bikisiwa* na *Sudana.* Kutokana na usomaji

wetu, wa tamthilia za *Posa za Bikisiwa* na *Sudana,* tumegundua kuwa zinaangazia suala la ukoloni mamboleo na utandawazi. Kulingana na waandishi wa tamthilia ya *Sudana* Alamin *Mazrui* na Kimani Njogu, suala la ukoloni mamboleo limejitokeza wazi. Alamin Mazrui na Kimani Njogu wanazungumzia suala la utegemezi wa misaada na nchi maskini. Mataifa maskini hutegemea misaada kutoka nchi matajiri. Nchi matajiri ndizo hudhibiti mfumo mpya wa utandawazi hasa wa biashara na uchumi. Msaada wanaopewa hutolewa masharti mbalimbali. Utandawazi hutumiwa na nchi za Kimagharibi kuendeleza dhuluma dhidi ya nchi maskini. Dhana ya utandawazi ni zao la Kimagharibi la kusisitiza kuwa kijiji cha ulimwengu. Mfumo huu mpya ni njama za nchi za Kimagharibi kuendeleza ukoloni mamboleo katika mataifa maskini. Wazungu huzua masharti kadhaa ambayo huzifanya nchi maskini kuondolewa kuhusika na kushiriki ipasavyo. Hii ni kwa sababu kuwa Waafrika huchukuliwa kama "Pembeni mwa kijiji" kwa vile hawana ujuzi na maarifa ya kudhibiti mfumo mpya wa utandawazi.

Said A.Mohamed na Kitula King'ei wakizungumzia suala la ukoloni mamboleo na utandawazi wanasema kuwa madhumuni ya utandawazi ni kukausha nchi changa kwa kutumia maneno matamu ya demokrasia, uwazi na uliberali mpya wa Benki ya Dunia, Shirika la Kifedha la Kimataifa (IMF) na pia kuhodhi njia za shirika la kifedha la kimataifa na ya matangazo ya runinga. Huu ni wizi na unyang'anyi wa kila kitu cha Mwafrika. Utandawazi basi huchukuliwa kama nguvu mpya za nchi tajiri kudidimiza nchi maskini. Hii ni sura mpya ya ukoloni mamboleo

inayoendelezwa katika utandawazi. Kutokana na utafiti wetu tumebainisha kwamba utandawazi umetumika kuendeleza unyonyaji, ukandamizaji na dhuluma dhidi ya mataifa maskini na mataifa ya Kimagharibi.

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kuonyesha jinsi utandawazi unavyotumika kuendelaza ukoloni mamboleo kama unavyojitokeza katika tamthilia za *Posa za Bikisiwa* na *Sudana*. Kama wanavyosema Alamin Mazrui na Kimani Njogu katika tamthilia ya *Sudana*, utandawazi ulichukua sura ya ukoloni mamboleo. Wanasema kuwa ukombozi waliopigania Waafrika ulibadilika na kuwa pingu ya ugozi. Utandawazi unaendeleza mbinu za unyanyasaji na unyonyaji. Hii ndio sababu ya Wazanji kuwaita Wazungu maharamia. Katika kipindi cha utandawazi, Waafrika wanachukuliwa na kupewa kazi ngumu kwa kujenga mashua ya Wamerope. Wananyonywa nguvu zao kwa malipo duni. Huu ni ukoloni mamboleo katika mfumo wa utandawazi. Pia Wazungu hutumia rasilimali za Waafrika katika kujenga mataifa yao. Wanabomoa mashua ya Wazanji ilikujenga mashua yao. Katika mfumo huu wa utandawazi wanaonufaika ni wale wenye uwezo wa kudhibiti nyenzo zote za uzalishaji. Viongozi pia wa nchi maskini hukubali uhusiano na mataifa matajiri kwa manufaa yao binafsi. Hii ndio sababu ya Sudzungu kumsihi mamake akubali kunajisiwa na Mwamerope. Huu ni ukoloni mamboleo unaoendelezwa katika utandawazi. Viongozi kama hawa hujiingiza katika mahusiano na mataifa ya Kimagharibi bila kujali athari zake.

Said A. Mohamed na Kitula King'ei wakielezea suala la ukoloni mamboleo na utandawazi, wanaonyesha mbinu zinazotumiwa na mataifa ya Kimagharibi kukandamiza mataifa ya "Dunia Ya Tatu". Wanakuja kama marafiki lakini kwa lengo la kutaka kukubaliwa. Mataifa ya Kimagharibi yalitaka uposaji lakini uposaji usiokuwa na mapenzi ya pande zote mbili. Hii ndio sababu ya Bikisiwa kupinga uhusiano usio na hisia za pande mbili. Wazungu wanatumia unyang'anyi na uporaji kudhibiti mataifa maskini. Utandawazi pia umemiliki njia za kuelimisha jamii kupitia teknolojia ya habari na mawasiliano. Kwa hivyo Waafrika hupokezwa vibovu kupitia vipindi vya runinga na ambavyo hawana uwezo wa kudhibiti. Huu pia ni ukoloni mamboleo unaoendelezwa kupitia kwa utandawazi.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha athari za ukoloni mamboleo na utandawazi katika *Posa za Bikisiwa* na *Sudana.* Katika usomi wetu tumegundua kuwa athari za utandawazi ni nyingi katika jamii za Kiafrika. Si kila athari ya utandawazi iliyo hasi. Hii ni kwa sababu kuwa katika kipindi cha utandawazi gharama na muda wa usafirishaji wa bidhaa umerahisishwa. Pia watu wanaweza kufanya kazi popote ulimwenguni kama inavyodhihirika katika tamthilia ya *Sudana.* Katika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa,* tunaambiwa kuwa Bikisiwa ana safari nyingi kwa kipindi cha muda mfupi. Kokote aendako hukufanya kuwa kwao. Hata hivyo, tumegundua utandawazi umeathiri pakubwa mataifa maskini katika nyanja zote za maisha. Kibiashara, lengo kuu la utandawazi ni ushindani. Madhumuni ya utandawazi ni kukausha nchi changa kwa kutumia maneno matamu

ya demkrasia uwazi wa uliberali mpya wa Benki Ya Dunia na Shirika La Fedha ulimwenguni. Waafrika hawana nguvu ya kiuchumi ili kuweza kushindana ilivyo katika mfumo wa utandawazi. Mwishowe wananyang'anywa kila kitu na kubakia kuwa maskini. Aidha utandawazi umeathiri mataifa changa pakubwa katika utamaduni wao. Wamenyang'anywa vyakula vyao, vitoweo vyao kama vile samaki na nyama pasipokuwa na uwezo wa kujikinga. Wameiga tamaduni za kigeni hasa kimavazi. Watoto wa siku hizi hutembea nusu uchi kinyume na ilivyo na utamaduni na desturi za Mwafrika. Lugha na nyimbo pia zinazotumiwa ni za kigeni.

Lengo la nne la utafiti huu lilikuwa ni kuonyesha mtindo uliotumika kufafanulia utandawazi. Tumegundua kuwa mtindo ni jinsi mtunzi wa kazi ya kisanaa anavyotumia lugha kuelezea na kuwasilisha maudhui. Kipengele muhimu ni mbinu za lugha anazotumia msanii. Lugha inayotumiwa na waandishi wa tamthilia hizi mbili teule inaenda sambamba na utandawazi na ukoloni mamboleo. Waandishi hawa wametumia jazanda, nyimbo na ushairi, misemo na nahau ili kusisitiza dhana ya utandawazi na ukoloni mamboleo. Lugha iliyotumika katika tamthilia hizi imesheheni uhusiano uliopo baina ya Mataifa Ya Kimagharibi na Ya Kiafrika katika kipindi hiki cha utandawazi. Ili kupambana na athari za utandawazi, Said A. Mohamed na Kitula King'ei wanapendekeza kuwa lazima mfumo wa elimu ufanyiwe mabadiliko, Waafrika wakuze vipawa vyao na kuthamini vitu vyao, Waafrika wafuate amali za utamaduni wao na wazinduke na wapiganie haki zao. Katika usomi wetu wa tamthilia za *Sudana na Posa za Bikisiwa* tumegundua kuwa

lugha ya Kiingereza ndiyo inayotumika katika mfumo wa utandawazi. Lugha za Kiafrika hazina nafasi katika utandawazi. Waafrika wamelazimishwa kutumia lughaza Kimagharibi hasa katika biashara na uchumi. Pia fasihi ya Kimagharibi imepokezwa Waafrika kupitia kwa vyombo vya habari na mawasiliano. Kwa jumla nikuwa lugha hutumiwa na wakoloni kama chombo cha ukandamizaji. Matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kuwasiliana na Waafrika ni ukandamizaji kwani wengi hawana ujuzi wa kutumia lugha hizo.

Kinadharia, tuliweza kutumia nadharia ya Baada - ukoloni. Mhimili wa kwanza wa nadharia hii ni kuwa lugha ya Kiingereza na fasihi yake ni vyombo vya ukandamizaji. Katika usomi wetu wa tamthilia za *Sudana* na *Posa za Bikisiwa* tumegundua kuwa lugha ya Kiingereza ndiyo inayotumika katika mfumo wa utandawazi. Lugha za Kiafrika hasina nafasi katika utandawazi. Waafrika wamelazimishwa kutumia lugha za Kimagharibi hasa katika biashara na uchumi. Pia fasihi ya Kimagharibi imepokezwa Waafrika kupitia kwa vyombo vya habari na mawasiliano. Kwa jumla ni kuwa lugha hutumiwa na wakoloni kama chombo cha ukandamizaji. Matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kuwasiliana na Waafrika ni ukandamizaji kwani wengi hawana ujuzi wa kutumia lugha hizo.

Mhimili wa pili ni kuwa unyamazishaji ni uti wa mgongo wa uhakiki wa baada ya ukoloni.Wazungu wametumia utandawazi kama mbinu mpya ya kuwanyamazisha Waafrika. Katika mfumo huu, Waafrika hawana nafasi ya kujiamulia watakacho. Wanapokezwa na kulazimishwa kukubali hata utamaduni wa

Kimagharibi bila swali lolote. Pia mifumo wanayopokezwa ya kisiasa ni ya Kimagharibi. Waafrika hulazimishwa masharti ya kibiashara katika mfumo wa utandawazi.

Mhimili wa tatu ni kuwa fasihi ya pembezoni huchukuliwa duni kwa sababu mbinu za kisanii hazifungamani na mbinu za kisanaa za Kimagharibu. Katika usomi wetu wa tamthilia hizi mbili tumegundua kuwa fasihi ya Kiafrika haina nafasi katika mfumo wa utandawazi. Hii ndiyo sababu kuwa hata Waafrika walioandika vitabu vyao vya fasihi vimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Said A. Mohamed na Kitula King'ei wameonyesha kwa tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* kuwa fasihi simulizi haina nafasi katika mfumo mpya wa utandawazi. Hii ndiyo sababu mtambaji anasema kuwa yeye ni mkimbizi na mhalifu wa kuzingiziwa.

Mhimili wa nne nao hudhihirisha juhudi za "ulimwengushaji" wa usomi wa Kimagharibi. Nadharia hii imeonyesha namna udhibiti wa utamaduni wa nchi za Kimagharibi unavyovunja kutokana na miigo na takiriri za nchi tawaliwa. Maingiliano haya yamesababisha kuwepo kwa 'utamaduni mseto'. Tumegundua kuwa Waafrika waliweza kupokezwa utamaduni wa kigeni na kuchukia utamaduni wao. Hii ndiyo sababu vijana wa kisasa wanavaa mavazi yaliyositiri, wanatumia lugha isiyoeleweka na kuimba nyimbo sizizoeleweka.

Mhimili wa tano tuliotumia ni kuwa nadharia ya Baada - ukoloni inawanasibu watawaliwa kuasi dhidi ya watawala katika vipengele vyote vya maisha. Kutokana na usomi wetu wa tamthilia za *Posa za Bikisiwa* na *Sudana*



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

tumewaona Waafrika wakipingana na nguvu za ukoloni mamboleo katika utandawazi. Katika tamthilia ya *Sudana*, waandishi wanaonyesha kuwa tayari Waafrika wangetaka kujikomboa. Sudana anasema kuwa lazima mapambano yaendelee huku wengine wakikubaliana naye. Alamin Mazrui na Kimani Njogu wanasisitiza kuwa lazima Mwafrika azinduke na kujikomboa kutokana na athari za utandawazi. Pia waandishi wa *Posa za Bikisiwa*, Said A. Mohamed na Kitula King'ei wanaonyesha juhudi za Waafrika za kupigana na athari za utandawazi. Wanapendekeza pia mabadiliko ya mfumo wa elimu kama njia mwafaka ya kupambana na utandawazi na athari zake.

## 5.3. Mchango.

Matokeo ya utafiti huu yatakuwa ya manufaa sana kwa viongozi wa mataifa maskini hasa wanaoingia katika uhusiano na mataifa ya Kimagharibi bila kujali athari za uhusiano wao. Pia utafiti huu hutawafaidi wasomi wa fasihi ya Kiswahili kwa kuwa umewapa mwangaza juu ya utandawazi na ukoloni mamboleo. Mchango mkuu wa kazi hii ni kuwa imeonyesha kuwa utandawazi ni mbinu mpya ya kuendeleza ukoloni mamboleo. Uhakiki huu hutawafaidi wasomi na watafiti kuhusu masuala yanayo husiana na utandawazi na athari zake katika jamii ya kisasa.

## 5.4. Matatizo.

Utafiti huu ulikabiliwa na matatizo kadhaa.Kwanza ni ukosefu na uhaba wa vitabu vya Kiswahili vya kutumiwa katika usomi wa awali. Baadhi ya vitabu vilivyokuwepo vingi ni vya Kiingereza. Ilimbidi mtafiti kutumia vitabu vya Kiingereza na kulazimika kutafsiri. Mara nyingi mtafiti alikumbana na changamoto za kutafsiri vitabu hivi ili kuweza kupata isitillahi sambamba. Ilibidi mtafiti kubuni maneno mengine na tafsiri kama hizi mara nyingi huathiri utafiti. Aidha mtafiti alilazimika kutumia mtandao ili kupata maelezo zaidi juu ya nadharia ya Baada - ukoloni. Mara nyingi haikuwa kazi rahisi hasa kupata nafasi kwa sababu ya ushindani uliokuwepo kwa tarakilishi chache zilizopatikana kijijini. Ilimbidi mtafiti kusafiri mbali aghalau kufidia tatizo ili.

Tatizo lingine lilikuwa la wakati. Wakati mara nyingi ulikosekana kwa kuwa mtafiti alikuwa angali kazini. Tatizo hili liliathiri muda wa kuwasilisha na kusheleweshа kazi kwa mtahini. Hata hivyo, mtafiti alilazimika kutia juhudi zote ili kufanikisha utafiti huu. Mtafiti pia alikumbana na tatizo la kuwapata waandishi wote ili kuwahoji. Kitula King'ei alikuwa likizoni na alikuwa Afrika ya Kuzini. Said A. Mohamed na Alamin Mazrui nao huishi ng'amboni na kwa hivyo ilikuwa vigumu kuwapata. Hata hivyo mtafiti aliweza kutumia mtandao ili kupata tawasifu zao.

## 5.5. Mapendekezo.

Utafiti huu umeshughulikia suala la ukoloni mamboleo na utandawazi. Kazi hii imezingatia tamthilia mbili tu za Kiswahili *Sudana* na *Posa za Bikisiwa*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya baada ukoloni. Tunapendekeza utafiti wa baadaye ufanywe kuhusu utandawazi kwa kuzingatia nadharia ya udenguzi. Hapa mtafiti anaweza kuchunguza kama tamthilia hizi mbili zinaweza kuhakikiwa kwa kutumia nadharia ya udenguzi. Tamthilia hizi mbili zimetumia mtindo tofauti wa kuwashilisha maudhui yake. Aidha utafiti wa baadaye unaweza kutumia nadharia ya uhalisia kuzungumzia suala la uajibikaji wa viongozi katika kuendeleza masuala ya nchi. Utafiti wa baadaye pia unaweza kuchunguza matumizi ya kijazanda katika tamthilia hizi mbili teule kama mtindo wa kuwasilisha maudhui.

**MAREJELEO.**


Abrams, M.H (1993) *A Glossary of Literary Terms. 6th Edition.* New York: Harcourt & Brace

Achebe, C. (1973): *Shujaa Okoukwo*. (Mfasiri: Clement Ndulute). Nairobi: Heinemann Education Books.

Ankie, M. M. Hoogvett (2001): *Globalisation and the Post Colonialism Word: The new political economy of Development*. Johns Hopkins University Press.

Ashcroft Bill, et al (1995): *The Post-Colonial Studies reader.* Routledge. London.

Bauman, Z.. (1998): *Globalization: The human Consequences.* New York. Columbia University Press.

Che Guevara (1965): *Marxist Revolutionary: A speech at the Afro–Asian* Conference in Algeria to the Second Economic Semina of Afro – Asian Soliderity in Algers, Algeria on 24 February, 1965. (From Wikipedia)

Featherstone, M. (ed) :( 1990) *Global Culture: Nationalism, Globalization and Modernity*. London. Sage Press.

Gromov, M.D. (2004): *Post-modernistic Element in Recent Kiswahili Novels.* Katika 'The Nairobi Journal of Literature. The Journal of Department of Literature, University of Nairobi' 2 uk 28-36

Jameson, Fredric. (1984) "*Postmodernism, or the Cultural Logic of Late Capitalism,*" New Left Review 146: 53 -93. Ithaca, Cornel University Press.

Jauch, Herbert. (ed) (2001): *Playing the Globalization Game: The implication of Economic Liberalisation for Namibia*, Labour Resource and Research Institute windhoeck.

Kapinga, D.S. (2004): *Chama Cha mapinduzi na serikali zake wafanye nini ili Kufaidika na mfumo wa utandawazi. Makala Kwa ajili ya semina ya Wenyeviti na makatibu wa CCM wa Mikoa na Wilaya.*

--------------- (2003): *Globalisation: Its Evolution and Changed Perspective, Processed*, DSI, SUA.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar-es-Salaam. University Press

………………*(1990). Mzingile.* Dar-es-saam. University Press

Khamis, Said A.M (1999): *Defamiliarisation and Experimentation in the Kiswahili Novel: A Case Study of Kezilahabi's Novel: Nagona. Hotuba isiyochapishwa ya kupokea uprofesa Chuo kikuu cha Bayreuth.*

Kimani, Njogu et al. (2006): *Fasihi Simulizi ya Kiswahili* Nairobi. Twaweza Communications.

Kimani Njogu na Rocha Chimerah. (1999): *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu.* Jomo Kenyata Foundation.

King'ei K. na Kemoli A. (2001): *Taaluma za Ushairi*. Nairobi Acacia Stantex

Publishers.

Korg, J. (1959): *An introduction to Poetry. New York.* HoH Reinehartx Wilson.

Kwame Nkurumah: (1965) Neo – Colonialism, The Last Stage of Imperialism. London: Thomas Nelson & Sons Ltd.

Mbatiah, Mwenda. (2001): Kamusi ya fasihi. Nairobi. Fotoform Ltd.

Mkapa, B.W. (2005): *Hotuba ya Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kwa Wananchi.*

Mkangi, Katama. (1995). *Walenisi.* Nairobo, East African Education Publishers

Mkufya, W.E. (1999): *Ziraili na Zirani*. Dar-es-salaam Hekima Publishers.

Mohamed, Said A. (2001). *Babu Alipofufuka.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation

Murray, A. (2000): *Public Sector Restructuring in Namibia-* Commercialization, *Privatisation and Outsourcing: Implication for Organised labour* LaRRI, Windhoek.

Offiong, Daniel A. (2001): *Globalisation: Post-Neodependancy and poverty in Africa*, Fourth Dimension Publishing Co: Enugu Nigeria.

Opoku, Agyeman. (1992): *Ghana and East Africa: Pan-Africanism Interinstitute Relations*. Fairleigh Dickinson University Press.

Robertson, Roland. (1992): *Globalization: Social Theory and Global Culture*. London Sage Press.

Said, Edward. (1978). *Orientalism.* London Routledge

Salisu, Suleiman (2004): *Globalization as Neo Colonialism. Human Rights,*

*Neo Colonialism and Imperialism in Nigeria*. Unpublished

Senkoro, F.E.M.K. (1982*): Fasihi.* Dar es –Salaam. Press and Publicity Centre.

Shakespeare, William. (1969). *Tufan:* (Mfasiri S.S. Mushi).

Dar- es –Salaam. Tanzania Publishing House.

........ (1594) *Mabepari wa Venisi* (Mfasiri: Julius Nyerere).

New York. Oxford Unuversity Press.

Toynbee, Arnold. (1938). *A Study of History*, Vol. VIII.

New York: Oxford University Press.

TUKI (1981): *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar –es –Salaam Oxford.

........ (1990): *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar –es – Salaam Oxford.

........ (2004): *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar –es –Salaam Oxford.

Wafula R.M na Kimani Njogu (2007). *Nadharia za Uhakiki Wa Fasihi*.

Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Wa Thiong'o Ngugi (1993), *Moving the Centre*. London Heinman.

Wamitila, K.W. (2002): *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*.

Nairobi, Phoenix Publishers Ltd.

..................... (2002): *Bina –Adamu*. Nairobi Phoenix publishers Ltd.

..................... (2003): *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*.

Nairobi. Focus Publications Ltd.

Wesa, W. (2005): *Uhakiki na Uchambuzi wa kifani katika utenzi wa Mwana Fatuma na Siri la Asirale*". M.A chuo kikuku cha Nairobi (Haijachapishwa).

## KIAMBATANISHO CHA I

### RATIBA YA KAZI

| MWEZI | | KAZI |
|---|---|---|
| Juni/Julai 2012 | : | Kuandika pendekezo la utafiti |
| Agosti/Septemba 2012 | : | Kupitia na kurekebisha pendekezo la utafiti |
| Oktoba/Novemba 2012 | : | Kutetea pendekezo la utafiti |
| Desemba 2012 | : | Kuandika upya sura ya kwanza |
| Januari 2013 | : | Kusoma na kuchambua vitabu teule |
| Februari/ Marchi 2013 | : | Kuandika ripoti na nakala ya mwisho |
| Aprili/Mai 2013 | : | Kuandika nakala ya mwisho baada ya kufanyiwa marekebisho. |
| Juni 2013 | : | Kufuzu na kupewa shahada ya uzamili |

## KIAMBATANISHO CHA II

### MAKADIRIO.

| | |
|---|---|
| Mawasiliano | Shillingi 5,000 |
| Uchapishaji | Shillingi 40,000 |
| Gharama ya kusafiri | Shillingi 15,000 |
| Matumizi ya mtandao | Shillingi 10,000 |
| Matumizi mengine | Shillingi 10,000 |
| ***Jumla*** | **Shillingi 80,000** |

**KIAMBATANISHO CHA III**

**HOJAJI**

A. Jina lako ........................................................

Tarehe ya kuzaliwa ......................... Kata ndogo ...................

Kata ......................................... Tarafa ...........................

Wilaya ....................................... Kaunti ...............................

**B. HISTORIA YAKO YA MASOMO.**

i. Shule ya msingi ..........................................................

-

-

ii. Shule ya upili ..........................................................

-

-

iii. Chuo Kikuu ..........................................................

..............................................................................

..............................................................................

**C. BAADHI YA TUZO ULIZOTUNUKIWA.**

..................................................................................

..................................................................................

**D. MAISHA YAKO YA UANDISHI**

(Lini uliingia katika uwanda wa uandishi na baadhi ya vitabu vilivyochapishwa?)

**E. MAONI YAKO JUU YA UTANDAWAZI NA UKOLONI MAMBOLEO.**

(Je, ni uhusiano gani uliopo baina ya utandawazi na ukoloni mamboleo?)



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY